

9 NOVEMBA, 2022

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Nane – Tarehe 9 Novemba, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ikupa.

Na. 107

Kuundwa Kamati za Watu Wenye Ulemavu

MHE. STELLA I. ALEX aliuliza:-

Je, ni Mikoa mingapi, Wilaya, Vijiji na Vitongoji wameunda Kamati za Watu wenye Ulemavu?

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uundwaji wa Kamati za Watu Wenye Ulemavu katika Ngazi ya Mkoa, Wilaya, Vijiji na Vitongoji ni kwa mujibu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na.9 ya mwaka 2010 kifungu cha 14(1) ambacho kimeelezea juu ya uundwaji wa Kamati za Watu Wenye Ulemavu katika ngazi ya Kijiji, Mtaa, Wilaya, Mkoa pamoja na majukumu ya kila Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, imetekeleza kwa kiwango kikubwa uundwaji wa Kamati hizo. Mchanganuo wa idadi ya Mikoa, Halmashauri na Vijiji/Mitaa ya Tanzania Bara iliyounda Kamati za Watu wenye Ulemavu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mikoa yote 26;
- (ii) Halmashauri zote 185;
- (iii) Vijiji 7,483 kati ya 12,319; na
- (iv) Mitaa 2,284 kati ya 4,263.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha na kufuatilia Vijiji na Mitaa yote inaunda Kamati za Watu Wenye Ulemavu, Serikali imeandaa mikakati mbalimbali ikiwemo kuingiza masuala ya Kamati za Watu Wenye Ulemavu kwenye Mwongozo Kabambe wa Upangaji wa Mipango na Bajeti ya Huduma za Ustawi wa Jamii kwenye Halmashauri (*Council Comprehensive Social Welfare Operation Plan – CCSWOP*) ambapo utekelezaji wake utaanza mwaka ujao wa fedha 2023/2024. Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia Watendaji wa Vijiji au Mitaa ili kuhakikisha Kamati za Watu Wenye Ulemavu zinaanzishwa katika maeneo yao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ikupa.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru na kuipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa maeneo ambayo Kamati hizi zimekwishaundwa hazifanyi kazi kwa mujibu wa Sheria Na.9 ya Mwaka 2010. Je, ni sababu zipi zinazosababisha Kamati hizi kutokufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; naipongeza pia Serikali kwa mikakati mizuri ambayo imewekwa kwa ajili ya ukamilishwaji wa kuundwa kwa Kamati hizi. Kutokana na umuhimu wa Kamati hizi na hasa ikizingatiwa kwamba zoezi hili limechukua muda mrefu kukamilika, je, ni lini Kamati hizi zitakamilika kuundwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo ambapo Kamati hizi pamoja na kuundwa hazijawa na utekelezaji mzuri wa ufanyaji kazi. Changamoto hii siyo ya kisheria zaidi, sheria imeelekeza ziundwe na tayari zimekwishaundwa, changamoto iko katika eneo la kwanza ni elimu kwa wahusika wenyewe walio kwenye Kamati, lakini sehemu kubwa ni uwajibikaji wa wale ambao wamechaguliwa kuzihudumia Kamati hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni usimamizi wa Kamati zenyewe. Jambo hili naomba nitumie Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Waziri Mkuu kuwaomba na kuwaelekeza pia Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala, pamoja na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala wa Wilaya waweze kusaidia na kusimamia utekelezaji wa sheria hii ili kuweza kuhakikisha inaleta ufanisi kama jinsi ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza ameuliza kuhusu utekelezaji, kwamba lini tutakuwa tumekamilisha zoezi hili. Nieleze tu kwamba Serikali tunaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu kuweza kuhakikisha Kamati hizi zinafanya kazi *effectively* na wale ambao hawajaunda kupitia Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wahakikishe kwamba Kamati hizo zinaundwa na ufanisi upatikane.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, itambulike kwamba suala la kutekeleza Sheria Na.9 ya Mwaka 2010 ya Watu Wenye Ulemavu sio suala la hiari, ni suala kisheria na ni la haki za binadamu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kwa kifupi malizia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Shonza.

Na. 108

**Hitaji la chumba cha upasuaji Kituo cha Afya
Itaka – Wilaya ya Mbozi**

MHE. JULIANA D. SHONZA aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kujenga chumba cha upasuaji kwa ajili ya Wajawazito katika Kituo cha Afya cha Itaka Wilayani Mbozi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

9 NOVEMBA, 2022

Juliana Daniel Shonza, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepeleka shilingi milioni 300 kwenye Kituo cha Afya Itaka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Fedha hizo zinatumika kujenga jengo la wazazi, na jengo la upasuaji. Ujenzi wa majengo hayo upo katika hatua ya msingi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shonza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nimekuwa nikiuliza swali hili mara kwa mara na nishukuru sana Serikali kwa sababu imetupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha upasuaji kwa ajili ya wanawake. Swali la kwanza; kwa kuwa Kituo hiki cha Afya cha Itaka kinatumika kama Kituo cha Afya cha Tarafa, kutokana na kwamba kata zote zinaunda Tarafa ya Itaka hazina vituo vya afya. Naomba kufahamu sasa ni lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi za kawaida za watoto, wanaume pamoja na wanawake?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan alipokuja kwenye kampeni mwaka 2020 katika Kata ya Mlowo...

NAIBU SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa Shonza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Naomba kufahamu sasa, ni lini Serikali itatekeleza

9 NOVEMBA, 2022

ahadi yake aliyoahidi Mheshimiwa Rais wa Awamu ya kutujengea kituo cha afya katika Kata ya Mlowo?

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Shonza amekuwa akiulizia sana suala la Kituo cha Afya cha Itaka akishirikiana na Mheshimiwa Mbunge Mwenesongole, lakini nimhakikishie Serikali sikivu ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, imepeleka fedha hizo na kazi ya ujenzi wa jengo la upasuaji inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba Serikali inajenga vituo vya afya hivi kwa awamu, tumeanza majengo hayo ya awali, lakini fedha itatafutwa kwenda kujenga wodi ya wanawake, watoto na wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ahadi ya Mheshimiwa Rais, kujenga Kituo cha Afya katika Kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, nimhakikisie kwamba ahadi za viongozi wetu ni kipaumbele. Kwa hiyo, Serikali tayari imeshaanza kufanya michakato ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha afya. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Engineer Ezra, Mbunge wa Biharamulo.

9 NOVEMBA, 2022

Na. 109

**Vifaa vya upasuaji kwa Vituo vya Afya
Rukaragata na Nemba**

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA aliuliza:-

Je, ni lini Vituo vya Afya vya Rukaragata na Nemba vitapewa vifaa vya upasuaji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023, imetenga shilingi bilioni 69.65 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Kati ya fedha hizo Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo imetengewa shilingi milioni 250.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imepeleka vifaa vya upasuaji ikiwemo kitanda, taa ya upasuaji na *X-ray machine* kwa ajili ya Kituo cha Afya Nemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kituo cha Afya Rukaragata hakina jengo la upasuaji, Serikali kupitia

9 NOVEMBA, 2022

mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo katika mwaka wa fedha 2023/2024, itatenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na hasa fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuhudumia vituo vya afya vilivyobaki. Kwa Kituo cha Nemba nashukuru kwa ajili ya vifaa vilivyopokelewa. Hata hivyo, nina swali moja la nyongeza; Kituo cha Afya cha Rukaragata ndicho kinachohudumia Wilaya ya Biharamulo Mjini, kwa sababu hatuna hospitali ya wilaya, kwa sababu hospitali iliyojengwa iko Kata jirani ya Lubungo. Sasa swali, kwa sababu tuna akinamama ambao wanajifungua pale na wanapata shida na hamna jengo la upasuaji na wametuingia tutapata pesa katika mwaka 2023/2024, ni mbali sana kwa sababu akinamama wanaendelea kuzaa na wanahitaji huduma. Sasa kwa sababu Waziri wa Fedha yuko hapa na Waziri ametuingia twende huko mbele, naamini Serikali inaweza ikapata fedha katika vyanzo vingine tukapata hii fedha katika mwaka huu wa fedha. Je, Waziri haoni haja ya kumpa nafasi Waziri wa Fedha aweze kutusaidia kwenye hili ili tuweze kupata fedha hii na akinamama wa Biharamulo waweze kunufaika na hili? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Biharamulo kwa swali lake na kwa kweli amekuwa akifuatilia

9 NOVEMBA, 2022

sana wizarani fedha ya hospitali ya wilaya ambayo ni takribani milioni 204, pamoja na hili suala ambalo anasema hospitali yake ya wilaya, *I mean* kituo hiki cha mjini kinafanyika kama hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe na nimwombe Mheshimiwa Mbunge aridhie tulichukue jambo hili Wizara ya Fedha ili tuwasiliane na wenzetu wa TAMISEMI, pamoja na yeye na Mkurugenzi wake, tuweze kuona namna ya kuliharakisha kwa ajili ya maisha ya Wanabiharamulo kama ambavyo amesema. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Rashid Abdallah Rashid.

Na. 110

Kuwezesha Vikundi vya Ushirika vya Uhifadhi wa Mazingira – Kiwani

MHE. RASHID ABDALLA RASHID aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaviwezesha vikundi vya uhifadhi mazingira Vijiji vya Chwaka, Kiwani, Jundamiti, Mwambe, Nanguji na Kendwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kiwani. kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeshachukua hatua za kuvijengea uwezo vikundi vyote vilivyotajwa ili viweze kukua na kujiendesha vyenyewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuvipatia mafunzo ya awali yanayohusu taratibu za uendeshaji na uendelezaji wa vikundi vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali kupitia Idara ya Vyama vya Ushirika, Zanzibar imepanga kutoa mafunzo kwa Baraza la Wanaushirika la Wilaya ya Mkoani katika robo ya pili ya mwaka huu wa fedha (Oktoba – Disemba 2022).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar imekuwa na utaratibu wa kutoa mafunzo mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira kwa vikundi vya mazingira pamoja na kuwapatia tunzo ya mazingira na vifaa vya usafi kwa vikundi vinavyofanya vizuri katika uhifadhi wa mazingira, Unguja na Pemba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid.

MHE. RASHID ABDALLA RASHID: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali la nyongeza. Ni kweli vikundi vimepatiwa mafunzo haya na vinapatiwa tunzo, lakini ni lini vitapatiwa fedha ili ziweze kuwasaidia katika shughuli zao badala ya

9 NOVEMBA, 2022

kukaa na mafunzo kwa takribani miaka miwili bila kupata fedha? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Abdalla Rashid, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali tayari imeshafanya mafunzo kwa vikundi hivi vya uhifadhi wa mazingira na tayari tumeshafanya uwezeshaji wa wataalam, hivyo Serikali sasa kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Zanzibar watafanya uwezeshaji wa vikundi hivi ili viweze kutekeleza miradi hii.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Lucy John Sabu.

Na. 111

Kuongeza magari RUWASA-Simiyu

MHE. LUCY J. SABU aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza magari RUWASA – Simiyu ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kujengea uwezo *RUWASA*, Mkoa wa Simiyu ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya magari 37 yalinunuliwa ambapo gari moja lilikabidhiwa *RUWASA*, Mkoa wa Simiyu na gari nyingine ilipelekwa Wilaya ya Itilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika jitihada za kuendelea kuboresha mazingira ya kazi ya *RUWASA* nchini, Serikali itanunua jumla ya magari ya 86 kwa ajili ya *RUWASA* na magari hayo yatapelekwa kwenye wilaya mbalimbali nchini ikiwemo Mkoa wa Simiyu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sabu.

MHE. LUCY J. SABU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini hasa magari mapya ya Wilaya zingine za Mkoa wa Simiyu yatapelekwa ili kuweza kusimamia miradi ya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Mkoa wa Simiyu una changamoto kubwa ya vyanzo vya maji, je, *RUWASA* wamejipangaje, kupeleka mitambo ambayo itasaidia katika kunusuru changamoto kubwa ya maji huku tukisubiri Mradi Mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria?

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa ameuliza lini haswa, mara baada ya magari kufika Mheshimiwa Mbunge magari yatafika sisi ni watu wa kuahidi na kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyanzo vya maji Mkoa wa Simiyu, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge, kwa Mkoa wa Simiyu tuna mradi mkubwa zaidi ya bilioni nne ambao unatekelezwa kwa mabadiliko ya tabia nchi. Kwa hiyo, Mkoa wa Simiyu tayari umeshatupywa jicho la kipekee kabisa na tayari miradi hii imeanza kutekelezwa. Vilevile vyanzo vya maji na kwa kutumia magari haya ambayo Mheshimiwa Rais ametupatia fedha nyingi, tayari ni tarehe 11 magari yatazinduliwa na tayari utaratibu wa kufika katika mikoa mbalimbali utaendelea.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Felista Njau.

Na. 112

Kuajiri Maafisa Habari Katika Balozi zetu

MHE. FELISTA D. NJAU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaajiri Maafisa Habari katika Balozi zetu ili kuutangaza nchi na vivutio mbalimbali?

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Maofisa wanaopelekwa Ubalozini, moja ya majukumu yao ya msingi ni kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ambayo imeweka msisitizo katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi. Miongoni mwa majukumu ya kila Ofisa na kila Ubalozi ni pamoja na kutangaza vivutio vya utalii wetu, kubidhaisha Kiswahili, kuvutia wawekezaji na kutafuta fursa za masoko kwa bidhaa zetu. Aidha, Wizara ina utaratibu wa kuwajengea Watumishi uwezo kupitia mafunzo ili waweze kufanya kazi zaidi ya moja ikiwemo kuwa na uwezo wa kutoa habari muhimu kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Njau.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Balozi nyingi nje ya nchi hazifanyi vizuri kwa ufanisi katika kutangaza fursa za nchi yetu vivutio pamoja na utalii.

9 NOVEMBA, 2022

Nini mkakati madhubuti wa Serikali kuhakikisha Balozi hizi zinafanya vizuri?

Swali la pili, kwa kuwa balozi zetu nyingi nje ya nchi hazina watumishi wa kutosha hasa balozi za kimkakati kama Congo na kwingineko, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama nilivyoelezea katika swali la msingi, kwamba utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ni kipaumbele muhimu cha Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba sera hiyo inatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ambayo inafanya kwanza ni Wizara ni kukiimarisha Kitengo chetu cha Mawasiliano ya Serikali ili kuhakikisha kwamba kinatoa taarifa zote muhimu kwa wadau kuhusu fursa zinazopatikana nje ya nchi na pia fursa ambazo zipo katika nchi yetu na hiyo imefanyika kwa ufanisi sana kwa sababu mfano Ubalozi wetu wa China ni ushahidi kwamba kitengo chetu kinafanya kazi vizuri kwa sababu ni taarifa nyingi ambazo Ubalozi wetu wa China zinapatikana kule na pia Serikali hapa na wananchi kwa ujumla wanapata taarifa nyingi za Ubalozi wetu na China na Balozi nyingine pia.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la watumishi, ni kweli kwamba ninaungana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hapo nyuma kidogo hilo tatizo la ukosefu wa wafanyakazi lilikuwepo na lilikuwa ni kubwa, hata hivyo kwa hivi sasa tayari Serikali imechukua juhudi maalum za kuhakikisha kwamba suala hili halipo. Mfano, katika mwaka uliosha wa 2021/2022 jumla ya wafanyakazi 140 walipelekwa kwenye Balozi zetu mbalimbali nje ya nchi na suala hili ni endelevu, na tayari hivi sasa Wizara yetu imepata kibali cha kuajiri Maafisa wengi tu ambao watakuwepo Makao Makuu kwa ajili baadaye miaka ya mbele huko waweze kwenda kutumikia katika Balozi zetu.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Asenga.

MHE. ABUBAKARI D. ASENKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba swali la yongeza katika swali Namba 122.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

Na. 113

**Hitaji la mbegu za Soya kwa wakulima wa
Jimbo la Newala Vijijini**

MHE. MAIMUNA S. MTANDA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha mbegu za Soya kwa Wakulima wa Jimbo la Newala Vijijini hasa katika Kata za Tarafa ya Chilangala?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

9 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Newala imetenga shilingi 6,000,000 za kuwezesha ununuzi wa kilo 3,000 za mbegu bora za soya. Mbegu hizo zitasambazwa kwa wakulima wa soya katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala ikiwemo Tarafa ya Chilangala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania kituo cha Utafiti (TARI) Naliendele kilo 2,260 za mbegu ya msingi ya soya itakayotumika kuzalisha tani 90 za mbegu iliyohibitishwa ubora ili kuimarisha upatikanaji wa mbegu katika Mikoa ya Kusini kwa msimu wa mwaka 2023/2024 na kulifanya zao hilo kuwa la tatu kwa wakulima wa kusini baada ya korosho, ufuta na sasa Soya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtanda.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Je, Serikali imejipangaje kuhusu masoko ya ndani na nje ya nchi ili wakulima walime wakijua kwamba masoko watakata baada ya mazao kuvunwa?

Swali la Pili, kwa kuwa hali ya hewa ya Tarafa ya Chilangala, kwa leo hii imebadilika siyo kama ile miaka ya 1970 na 1980 wakati zao hili linalimwa. Je, Serikali

9 NOVEMBA, 2022

imejipangaje kwenda kutoa elimu kwa wakulima hawa ili waweze kulima kilimo chenye tija? Ahsante.(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi, Wizara kupitia *TARI - Naliendele na Mlingano*, sasa hivi wanafanya *mapping* ya soil na kuweza kutoa elimu kwa wakulima kutokana na ekolojia ya maeneo husika na hili zoezi ni *on going*, tutakapoanza *program* ya soya katika Mikoa ya Kusini, *TARI Naliendele* moja ya jukumu lao la msingi itakuwa ni kutoa elimu kwa wakulima ili tuweze kupata tija, na ndiyo maana tunaanza eneo dogo la Wilaya ya Newala Vijijini *and then* baada ya hapo mwaka unaofuata wa 2023/2024 kulifanya hili zao kuwa ni zao la tatu katika Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masoko changamoto masoko ipo hasa kwa mazao ambayo siyo ya msingi ya chakula kwa binadamu, kama mazao ya korosho na mazao mengine. Kwa hiyo, hatua ambayo tunaifanya kama Serikali sasa hivi na mtaona mwaka kesho, ni Serikali kuweka nguvu kubwa katika kuongeza thamani kwa mazao ambayo tunayazalisha ndani ya nchi na kuwasaidia *private sector* ambao wamewekeza katika maeneo hayo kuwapa nguvu na kuwasaidia *infrastructure development* ili waweze kuongeza thamani katika mazao yetu na kuhakikisha kwamba tunapata zile *international certification* ili tuweze kumaliza hayo matatizo.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante amekuelewa vizuri Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Mheshimiwa Waziri huu ni msimu wa kilimo kwa Mkoa wa Rukwa na Nyanda za Juu Kusini lakini mpaka sasa nazungumza, upatikanaji wa mbolea na mbegu bora Wilaya ya Nkasi na Mkoa mzima wa Rukwa una changamoto.

Ni nini mkakati wa Serikali ili msiwe kikwazo kwa wakulima hawa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Aida, nadhani jana wakati tunafanya semina aidha hakuwepo tulitoa majibu yote ya kina kuhusu hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo lake, Wilaya yake, jana nimeongea na Mkuu wa Wilaya, tumeongea namna gani baadhi ya maeneo ambayo ni Tarafa zinazo wakulima wengi ziweze kufikiwa mbolea, tumeiomba Halmashauri yake iweze kutusaidia kupata usafiri ili sisi tuweze kuwasaidia mafuta waweze kusambaza mbolea maeneo ambayo mawakala hawafiki. Lakini wakala yupo Jimboni kwako na anauza mbolea. Tatizo lililopo ni mbolea kufika vijijini jambo ambalo tunashirikiana na ofisi ya Mkurugenzi na DC kwa ajili ya kufanya hivi baada ya wewe kuleta hili lalamiko kwetu. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Chumi.

Na. 114

Ukusanyaji wa asilimia tano ya zawadi kwa michezo ya kubashiri

MHE. DAVID C. CHUMI aliuliza:-

Je, Serikali inakusanya kiasi gani cha asilimia Tano ya zawadi ya washindi wa mchezo wa kubashiri na kimechangia kiasi gani kukuza michezo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 mpaka mwezi Septemba mwaka 2022, Wizara imepokea kiasi cha Shilingi za Tanzania Bilioni 3.4 ikiwa ni asilimia Tano ya mapato yatokanayo na michezo ya kubashiri. Kwa mujibu wa muongozo wa mfuko wa Maendeleo ya Michezo fedha hizi hutumika kuhudumia Timu za Taifa, kutoa mafunzo kwa wataalamu wa michezo na wanamichezo, kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo

9 NOVEMBA, 2022

pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Timu za Tembo *Warriors* na Serengeti *Girls* ni miongoni mwa wanufaika wa hivi karibuni wa fedha hizo katika maandalizi na ushiriki wao kwenye mashindano ya Kombe la Dunia la mpira wa miguu kwa Walemavu na Wanawake chini ya miaka 17 ambapo zilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali na kuipandisha daraja nchi yetu katika nafasi za soka Duniani. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chumi.

MHE. DAVID C. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na ninakuomba kwa ridhaa yako kabla ya maswali yangu mawili ya nyongeza nitumie nafasi hii kuwapongeza Serengeti *Girls* na Tembo *Warriors* kwa kufika hatua ya robo fainali, lakini pia kuwapongeza Simba Queens ambao leo wanacheza hatua ya nusu fainali na Mamelodi Sundowns na kuwapongeza Simba kuingia hatua ya makundi na kuwaombea Yanga leo dhidi ya Club Africain waweze kushinda na kuingia hatua ya makundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo nina maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali iko tayari kuona kwamba sehemu ya fedha hizi inatumika pia katika kuboresha mchezo wa riadha ambao unaweza kutusaidia katika kujitangaza kwa umadhubuti katika kushiriki michezo kama vile Tokyo Marathon, New York Marathon, Bostin Marathon na kadhalika?

9 NOVEMBA, 2022

Swali la pili, kwa muda mrefu mojawapo ya shida katika michezo yetu hasa mchezo wa soka ni kiwango duni cha waamuzi.

Je, Serikali iko tayari kutenga sehemu ya fedha hizi kufanya mafunzo maalum kwa ajili ya waamuzi ili waamuzi wetu kuwajengea uwezo na hivyo kuwawezesha kushiriki katika kucheza michezo ya *AFCON, World Cup* na kadhalika? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza Mheshimiwa Chumi amependa kufahamu kama Serikali ipo tayari sasa kutenga sehemu ya fedha hizi kuhakikisha pia wanaweza ku-*support* riadha. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sisi kama Wizara tunayo michezo Sita ya kipaumbele ikiwemo riadha. Kwa hiyo, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ku-*support* riadha ili iendelee kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, amependa kufahamu kama fedha hizi pia zitatumika katika kuwezesha waamuzi. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania pia kwamba chini ya *BMT* wameendelea kusimamia kwamba vyama vya michezo waweze kuwaandaa waamuzi. Na niwapongeze *TFF* wiki hii iliyopita walikuwa na programu ya vijana 30 pale Uwanja wa Taifa

9 NOVEMBA, 2022

wakishirikiana na FIFA kuhakikisha kwamba tunapata waamuzi kwenye michezo hii. Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Wizara ya mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Charles Mwijage.

Na. 115

Mlalamikaji kumsafirisha mahabusu – Kamachumu

MHE. CHARLES J. MWIJAGE aliuliza:-

Je, ni kwanini katika Tarafa ya Kamachumu mlalamikaji hulazimishwa kumgharamia mahabusu kwa kumsafirisha kwenda na kurudi rumande?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Polisi (*Police Force and Auxiliary Service Act*) Sura ya 322 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 na Kanuni 353 na 354 ya Kanuni ya Jeshi la Polisi (*Police General Order*) zinazosimamia watuhumiwa/mahabusu walioko kwenye Vituo vya Polisi, utaratibu wa kuwasafirisha watuhumiwa/mahabusu kwenda Mahakamani hutekelezwa na Jeshi la Polisi. Pia jukumu la kuwasafirisha

9 NOVEMBA, 2022

watuhumiwa/mahabusu toka rumande Gerezani kwenda Mahakamani ni jukumu la Jeshi la Magereza kwa mujibu wa Kifungu cha 75 cha Sheria ya Magereza Sura ya 58 ya mwaka 1967 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha mlalamikaji kulazimishwa kugharamia usafirishaji wa mtuhumiwa/mahabusu kwenda na kurudi rumande ni kukiuka Sheria na Kanuni zilizopo na kinatakiwa kuachwa mara moja. Wizara imefanya mawasiliano na Wakuu wa Vyombo vyetu, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) na Mkuu wa Jeshi la Magereza (CGP) ili wawaelekeze wasaidizi wao ngazi za Mikoa na Wilaya kuzingatia sheria hiyo. Ninashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mwaka jana Oktoba, Bibi yangu Ndugu Juliana Leo Gaesha, alitwa kituo cha Polisi na kupelekwa Mahakama Kamachumu, Hakimu alimueleza mlalamikaji kwamba Bibi huyu apandishwe pikipiki na mlalamikaji akalipa fedha, Bibi yangu na watu wawili wakafungwa mshikaki kwenye pikipiki wakaenda Muleba, kufungwa Muleba magereza. Sasa kwa majibu yako Waziri ni lini mamlaka yako Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Sheria na TAMISEMI, mtatengeneza Tume ya Kitaifa, yaani ngazi ya Taifa muende mpeleleze tukio hili la Juliana Gaesha? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage swali! Mheshimiwa Naibu Waziri.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tukio hili lililotokea Muleba, kwa kweli hatuhitajiki kuunda Tume, badala yake wale ambao wako kule wanaosimamia utekelezaji wa sheria wazingatie sheria, labda kama jambo lingekuwa limepitiliza sana hiyo ipo haja ya kufanya hivyo. Lakini kwa kiwango hiki ninaamini wasaidizi wetu walioko ngazi hizo watazingatia na kuanza kutekeleza. Kama linaigusa Mahakama, wenzangu wa Mahakama wapo wamesikia litatekelezwa Mheshimiwa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Olelekaita

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali dogo tu. Kijiji cha Magungu wamejenga jengo la Kituo cha Polisi tangu mwaka 2016, nini kauli ya Serikali katika kuwasadia kumaliza lile jengo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze wananchi wa Kijiji hicho cha Magungu, kwa kufanya jitihada na juhudi kujenga Kituo cha Polisi. Tutakachofanya ni kufuatilia kiwango kilichofikia hilo jingo, linahitaji kiasi gani ili liweze kukamilishwa na tuone uwezekano wa kuingiza kwenye mpango wa ujenzi kutegemea upatikanaji wa fedha. Kama tulivyoongea juzi wakati wa ziara yangu nitafikia kwenye kituo hicho ili kuweza kuona hatua iliyofikia. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dokta Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kuwasaidia wananchi wa Kata ya Mwika Kaskazini kumalizia kituo muhimu sana kwenye Soko Kuu la Mwika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kimei, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama wananchi wa Kata hiyo wameshajenga kituo wanahitaji kupata msaada wa Serikali kukamilisha tutahitaji tu uongozi wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro waweze kufanya tathmini kuona jengo limefika kiwango gani ili waweze kuliingiza kwenye mpango wa ujenzi kama tunavyofanya kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Kimei, tukupongeze kwa kuhamasisha wananchi na sisi tutakuunga mkono baada ya kupata uthamini huo.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

9 NOVEMBA, 2022

Na. 116

Ukarabati wa Kituo cha Polisi Matangatuani - Micheweni

MHE. ASYA SHARIF OMAR aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati katika Kituo cha Polisi Matangatuani Wilayani ya Micheweni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naenda kujibu swali la Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi cha Matangatuani kilichopo Wilaya ya Micheweni ni kituo kilichojengwa siku nyingi na jengo lake ni chakavu. Katika tathmini iliyofanyika jengo hilo halifai kufanyiwa ukarabati kutokana na udhaifu wa kuta za jengo hilo. Serikali ina mpango wa kujenga Kituo kipya cha Polisi cha daraja "C". Michoro na makadirio yameshafanyika na kiasi cha Shilingi 427,604,929 kinahitajika kwa ajili ya kujenga Jengo la Kituo pamoja na nyumba mbili za makazi ya Askari. Fedha za ujenzi zinatarajiwa kuombwa kwenye Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 kutegemea na upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asya.

9 NOVEMBA, 2022

MHE. ASYA SHARIF OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini bado naona iko haja ya Mheshimiwa Naibu Waziri kulipa kipaumbele suala la kwenda kukiona kituo kile kwa sababu Askari wale wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Je, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda katika eneo hilo la Kituo cha Polisi cha Matangatuani ili kuweza kutoa msukumo zaidi katika bajeti hiyo 2023/2024 kufanikisha ujenzi huo wa kituo kipywa lakini pia na nyumba za makazi ya Askari Polisi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ambayo kwa kweli yanakaribia kufanana ya Mheshimiwa Asya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba eneo hilo halina Kituo cha Polisi lakini jambo kutia moyo wananchi hawa tayari wametenga eneo la kutosha kujenga kituo na nyumba za watumishi upande wa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaahidi kwamba niko tayari kukitembelea ili kuona kiasi gani kinahitajika na pia kuweka msukumo ili jengo hilo likamilishwe kwa haraka baada ya kutolewa kwa fedha hizi. Kwa hiyo, kuongozana naye wala halina tatizo. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Maryam Mwinyi, jiandae Mheshimiwa Ritta Kabati.

9 NOVEMBA, 2022

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kituo cha Polisi kilichopo wilaya ya Mkoani mkoa wa Kusini Pemba kipo katika hali mbaya.

Je, ni lini Serikali itakifanyia ukarabati kituo hicho japo kwa dharura?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Mwinyi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba maeneo ya Pemba vituo vyake vingi vya Polisi vimechakaa vinahitaji kufanyiwa marekebisho au kiujengwa vipya. Tumeanza na majengo ya Kamanda wa Polisi wa mkoa miwili ya Pemba, lakini tutaendelea kujenga hivi vya ngazi ya wilaya na vingine vidogo ili hatimaye maeneo yote yaweze kupata vituo vinavyostahiki. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ziara nitakayoifanya huko Pemba, moja ya maeneo ni kuzingatia maeneo haya ambayo hayana kabisa vituo vya Polisi ili na wao waweze kupatiwa vituo hivi kwa ajili ya usalama wa raia na mali zao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati maeneo mengine wanazungumzia habari ya ukarabati wa vituo vya Polisi, kwenye Mkoa wetu wa Iringa katika wilaya ya Kilolo bado Serikali haijajenga Makao Makuu ya Jeshi la Polisi ngazi ya

9 NOVEMBA, 2022

wilaya ilhali ni zaidi ya miaka ishirini sasa Serikali imekuwa ikitoa ahadi.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga makao makuu ya polisi Wilaya ya Kilolo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yaliyotangulia, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba wilaya zote zinapata vituo vya polisi vyenye hadhi ya wilaya. Hivyo kutokana na upatikanaji wa fedha tunakwenda kwa awamu. Nimuahidi tu Mheshimiwa Ritta kwamba Wilaya ya Kilolo ni miongoni mwa wilaya zitakazozingatwa hasa ukizingatia kwamba kuna uharibifu mkubwa wa mazingira yanayohitaji usimamizi wa sheria kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo itapewa kipaumbele katika bajeti zetu.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Dkt. Tecla naona umesimama.

MHE. DKT. TECLA M. UNGELE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa umbali kutoka Nachingwea – Liwale ni zaidi ya Kilometa 130 na Kilwa – Liwale ni zaidi ya kilometa 260.

Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya polisi pale Kibutuka Wilaya ya Liwale na Njinjo kule Wilaya ya Kilwa? Ahsante sana.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Ungele kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umbali alioutaja Mheshimiwa Mbunge kwamba kutoka eneo moja hadi kituo cha Polisi ni zaidi ya kilometa 100 ina-*justify* kabisa umuhimu wa uwepo wa kituo cha Polisi. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutaelekeza Kamanda wa Polisi Mkoa na Jeshi la Polisi kwa ujumla wake kufanya tathimini ya uhitaji wa kituo cha Polisi maeneo hayo uliyoyarejea ili mpango wa ujenzi wa vituo hivyo uweze kutekelezwa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Maige Almasi.

Na. 117

Sheria ya kusimamia Kampuni Binafsi za Ulinzi

MHE. ATHUMAN A. MAIGE auliza: -

Je, Serikali ni lini italetwa Bungeni Muswada wa Sheria ya Kampuni Binafsi za Ulinzi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa

9 NOVEMBA, 2022

Athuman A. Maige Mbunge wa Tabora Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa Sheria inayosimamia kampuni binafsi za ulinzi. Kwa sasa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kutunga Sheria ya Huduma za Sekta Binafsi za Ulinzi umekamilika, na utawasilishwa katika Baraza la Mawaziri kwa ajili ya Maamuzi baada ya kupata maoni ya kina ya wadau wa pande zote mbili za Muungano juu ya rasimu ya sheria hiyo. Baada ya kukamilika kwa hatua hizo, Muswada wa Sheria hiyo utawasilishwa Bungeni. Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Almasi.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali inakiri kuwa muda wa miaka sita tangu ichukue Muswada huu ni mrefu sana kutoletwa Bungeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wakati tunajadili kupata maoni ya Muswada huu tuligundua kwamba kipengele kile cha kubeba silaha Upande wa Zanzibar kisingekubaliwa. Je, tukiongeza maneno "isipokuwa Zanzibar" katika kipengele kile kitafanya Muswada huu uamke na kuletwa Bungeni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima naomba arudie swali la kwanza sikulisikia vizuri nijibu kwa ufasaha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Athuman Maige, hebu rudia swali lako la kwanza.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeuliza Je, Serikali inakiri kwamba muda wa miaka sita tangu Muswada huu uchukuliwe na Serikali ni mrefu sana kutoletwa Bungeni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu mawali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maige kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uandaaji wa sheria, hasa hizi ambazo zinahitaji ushirikishwaji mpana wa jamii hususani kwenye hili ambalo linahusu pande mbili za Muungano ni jambo ambalo miaka sita huwezi ukasema ni muda mrefu sana. Ni muda mrefu lakini ili tupate sheria itakayokubalika kwa pande zote na wadau wote tunaomba Mheshimiwa atuvumilie tuweze kulikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni ya kubeba silaha upande wa Zanzibar kwamba kuna changamoto pengine hicho kipande kiondolewe, naomba Mheshimiwa asubiri michakato ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar na Baraza la Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaweze kukamilisha kazi yake tuweze kuwasilisha Muswada huo.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham Mbunge wa Ulanga.

Na. 118

Kufungua barabara ya kimkakati inayounganisha Mkoa wa Morogoro na Mikoa na Kusini

MHE. ALAUDIN H. SALIM aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itafungua barabara ya kimkakati inayotoka Mahenge mpaka Liwale kupitia Malinyi, Mlimba, Njombe na Songea?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alaudin Hasham Salim, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara inayotoka Mahenge kwenda Liwale ni Mahenge - Mwaya – Ilonga – Liwale ambapo sehemu ya Mahenge hadi Ilonga imefunguliwa na inapitika majira yote ya mwaka. Hata hivyo, kutoka Ilonga kwenda Liwale hakuna barabara kwa vile sehemu hii ipo ndani ya Mbuga ya Wanyama ya

9 NOVEMBA, 2022

Mwalimu Nyerere na itahitaji kufanyiwa upembuzi yakinifu wa awali kuona iwapo inakidhi vigezo vya mazingira kabla ya kufunguliwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salim swali la nyongeza.

MHE. ALAUDIN H. SALIM : Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kwamba Wilaya ya Ulanga ni kitovu cha uchimbaji wa madini, lakini pia kuna miradi mikubwa ambayo inaenda kuanza ya madini ya kinywa ambayo ina manufaa makubwa kwa nchi lakini pia kwa uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Ulanga. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 67 kwa kiwango cha lami ?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Tarafa ya Mwaya ni tarafa inayoongoza kwa kilimo cha pamba pamoja na ufuta.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili wanachi hawa waweze kufikisha mazao yao sokoni kwa urahisi zaidi ?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza sikulipata vizuri ningeomba aweze kulirudia.

NAIBU SPIKA : Rudia tena swali la kwanza.

9 NOVEMBA, 2022

MHE. ALAUDIN H. SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ulanga ni Jimbo ambalo linaongoza kwa uchimbaji wa madini lakini pia kuna miradi mipya ambayo inaenda kuanza ya uchimbaji wa madini ya kinywa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuijenga barabara hiyo ili kuwarahisishia wawekezaji hao kufanya kazi zao kwa urahisi? pia kuhakikisha wananchi wanapata barabara bora ya yenye urefu wa kilometa 67 kwa kiwango cha lami ambayo iliahididiwa kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2015 lakini pia mwaka 2020?

NAIBU SPIKA : Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Alaudini Hasham Salimu Mbunge wa ulanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa barabara ambazo zinarudiwa na TANROAD kutoka Mpilo – Mahenge iko kwenye mpango wa EPC+F na tayari Wakandarasi wameshapita na barabara aliyoitaja ya pili Serikali inaendelea kutafuta fedha ili iweze kuijenga kwa kiwango cha lami ili kurahisisha usafiri na kuwafanya wananchi wa Ulanga waweze kufanya biashara zao kwa urahisi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chaurembo, jiandae Mheshimiwa Parangyo.

9 NOVEMBA, 2022

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni lini ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Mbande - Kisewe mpaka Msongola utaanza?

NAIBU SPIKA : Mheshimiwa waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo Mbunge wa Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja iko kwenye mpango na tunategemea utekelezaji utaanza mwaka huu wa bajeti.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pallangyo.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, barabara ya *USA River* kwenda Oldonyo Sambu kwa kupitia Hifadhi ya Arusha imejengwa kwa kiwango cha lami hadi Getini Ngongongare.

Je, ni lini Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kutoka ngare na nyuki Kwenda Oldonyo Sambu na kuunganisha Barabara ya Kwenda Namanga na Moshi kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali

9 NOVEMBA, 2022

la Mheshimiwa Parangyo Mbunge wa Arumeru kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ipo kwenye ilani na Mpango wa Serikali ni kuijenga kwa kiwango cha lami barabara aliyoitaja. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa jimbo lake kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuijenga barabara hiyo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa swali namba 120 vilevile ni la ujenzi kwa hiyo tutaliruka 119 tunakwenda 120 ili Waziri ajibu kwa Pamoja. Mheshimiwa Gulamali, hayupo? Wapi? amekwenda Tunisia au? kwa niaba?

Na. 120

Hitaji la ujenzi barabara ya Choma – Ziba – Nkinga hadi Puge

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA K.n.y. MHE. SEIF K. GULAMALI aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Choma – Ziba – Nkinga hadi Puge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Barabara ya Choma – Ziba – Nkinga hadi Puge yenye jumla ya kilometa 109.56 ambayo inapita katika maeneo muhimu ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Ndala na Hospitali ya Rufaa ya Nkinga, Serikali kupitia Wakala wa Barabara nchini *TANROAD*, imeamua kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Samwel.

MHE. ENG. SAMWEL X. HHAYUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Haidong - katesh imeshatengewa milkioni 300 kwa ajili ya ujenzi na milioni 280 kwa ajili ya usanifu wa kina. Je, Serikali ina mpango gani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pilli, Barabara ya Nangwa – Kondo ina daraja ambalo limekuwa likikwamisha wananchi, daraja la Munguli, ilitengewa milioni 600. Je, ujenzi wake utaanza lini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika,

9 NOVEMBA, 2022

napenda kujibu swali la Mheshimiwa Xhaday Mbunge wa Hanang kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Hydrom – Katesh ipo kwenye mpango na imepangiwa fedha. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa utekelezaji ni mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Daraja la Munguli linalounganisha Kondo na Hanang pia limetengewa fedha kwa ajili ya kulijenga Mwaka huu wa fedha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunarudia swali namba 119 la Mheshimiwa Deo Mwanyika. Wizara ya Ujenzi na uchukuzi. Mheshimiwa Deo.

Na. 119

Serikali kukarabati Reli ya TAZARA

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati reli ya TAZARA?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa

9 NOVEMBA, 2022

Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha miundombinu ya reli ya TAZARA. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 13.1 kwa ajili ya ununuzi wa mataruma ya mbao kwa ajili ya kufanyia ukarabati madaraja 172 yaliyopo upande wa Tanzania, ununuzi wa mtambo wa kisasa wa kushindilia kokoto kwenye reli, na ununuzi wa mtambo wa kuvunjia kokoto (*secondary crusher*) kwa ajili ya kuongeza kokoto za aina mbalimbali zinazotumika katika kufanyia matengenezo ya njia ya reli kati ya Dar es Salaam – Tunduma na Msolwa - Kidatu. Aidha, fedha hizo pia zitatumika kukarabati mabehewa 21 ya treni za abiria za Udzungwa na treni za abiria za mjini (*commuter*) za Jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mikakati ya muda wa kati na mrefu, Serikali za Tanzania na Zambia zimeandaa mpango wa biashara wa miaka mitano ambao unatarajiwa kupitishwa na Baraza la Mawaziri wa TAZARA mwishoni mwa Novemba, 2022. Aidha, Serikali za Tanzania, Zambia na China zimeunda timu ya pamoja kwa ajili ya kuandaa mkakati wa pamoja kwa kuishirikisha Serikali ya Watu wa China katika kugharamia maboresho ya TAZARA. Ahsante.

NAIBU SPIKA : Mheshimiwa Mwanyika.

MHE. DEOGRATIUS P. MWANYIKA : Mheshimiwa Naibu spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na uwekezaji anaouongelea wa bilioni 13

9 NOVEMBA, 2022

changamoto kubwa ya reli ya TAZARA ni kwamba hata ukiwekeza hizo fedha, uendeshaji kibiashara ni tatizo. Sasa Serikali ina mpango gani wa muda mfupi ili reli hii iendeshwe kibiashara iondoe maroli mengi ambayo yako barabarani badala ya kutumia mzigo uende kwa treni ?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tuliambiwa hapa na kulikuwa na ushauri wa Kamati ya Bajeti, kwamba mkataba wa uwekezaji wa Reli ya TAZARA ndilo moja ya tatizo kubwa sana linalotufanya tusiweze kuitengeneza reli hii vizuri. Sasa swali, Serikali ina mpango gani na imechukua hatua gani mpaka muda huu kurekebisha mkataba huo au kuu-terminate kabisa ?

NAIBU SPIKA : Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI MHE. FREDY MWAKIBETE : Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa ujenzi na uchukuzi napenda kujibu Maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwanyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili la Reli ya TAZARA, pamoja na Wabunge wote wa Nyanda za Juu Kusini wamekuwa kila mara wakifuatilia jambo hili. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Nyanda za Juu Kusini, mpango wa muda mfupi ndio huo ambao tumetenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 13.1 na tutafanya manunuzi ambayo nimejibu kwenye jibu langu la Msingi.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mkataba, mkataba ama Sheria Namba 4 ya mwaka 1995 ya TAZARA ndiyo ambayo inakwamisha tusiendeleo hasa katika uwekekezaji kama nchi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zambia walipokutana walielekeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tukutane na wenzetu wa Zambia. Mikutano hii imefanyika mwezi uliopita tarehe 14/10/2022 mpaka tarehe 15/11/2022 na mimi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri nilimwakilisha Lusaka Zambia kwa ajili ya kujadili Sheria hii. Mwishoni mwa Desemba tutakutana tena ili tuihushie halafu baadae tutaiteta kwenye Mabunge yote mawili ya nchi ya zambia pamoja na nchi ya Tanzania ili sasa kila nchi ipate fursa ya kuwekeza upande wake.

NAIBU SPIKA : Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante.

NAIBU SPIKA : Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu na Sayani. Mheshimiwa Oran Njenza.

Na. 121

**Ujenzi wa Ndaki ya Sayansi ya Afya Chuo Kikuu cha
Dar es Salaam – Mbalizi**

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Je ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Ndaki ya Sayansi ya Afya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika mamlaka ya Mji wa Mbalizi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeanza hatua za awali kwa kuwasilisha kwa Msajili wa Hazina maombi ya kupewa ardhi yenye ukubwa wa hekari 2000 kwenye eneo lililokuwa shamba la *Tanganyika Packers* kwa ajili ya ujenzi. Kwa sasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinaendelea kufuatilia maombi haya kwa Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Ndaki ya Sayansi ya Afya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Mbalizi utanza mara moja pale upatikanaji wa ardhi utakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Njeza.

MHE. ORAN M NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, labda kwa usahihi tu Jimbo linaitwa Mbeya Vijijini na si Mbalizi.

MHE. ORANI M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Labda kwa usahihi tu Jimbo linaitwa Mbeya Vijijini na siyo Mbalizi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Ahsante.

9 NOVEMBA, 2022

MHE. ORANI M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuipongeza Serikali kwa kuanzisha na vile vile kuboresha hii ndaki ya afya ikiwa sehemu ya uboreshaji wa Afya nchini kwetu. Sasa kwa vile kuna ongezeko kubwa sasa hivi la magonjwa yasiyoambukizwa: Je, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hii ndaki ya afya wamejiandaa vipi kukabiliana na hilo ongezeko la magonjwa yasiyoambukizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa hiki chuo kinaonekana kuwa kitakuwa na eneo kubwa sana, kwa hiyo, kinategemea kuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi.

Je, kitakuwa na wanafunzi wangapi na pia wafanyakazi wangapi mara kitakapokamilika kujengwa? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kawaida kwenye vyuo vyetu vikuu, jukumu lao la kwanza ni kuhakikisha kwamba utoaji wa taaluma ya aina mbalimbali au katika maeneo ambayo yanakuwa yameainishwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba chuo chetu cha tiba ya binadamu Muhimbili kinaendelea kufanya utafiti wa magonjwa haya yasiyoambukizwa kwa

9 NOVEMBA, 2022

undani zaidi ili kujua chanzo cha magonjwa haya na namna gani tunaweza kuyaepuka. Kwa hiyo, nimwondoo wasiwasi, na mikakati yetu kama Serikali na kama Wizara ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kufanya tafiti hizo za kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kuhakikisha tunatoa elimu kwa Umma kuhusu namna gani ya kuepuka na kujikinga na magonjwa haya yasiyoambukiza. Kwa hiyo, hilo litakuwa ni jukumu la pili na mkakati wetu wa pili. Eneo la tatu ni kubadili sasa mifumo ya maisha yetu tuliyozoea kuishi ili kuweza kuepukana na magonjwa haya kama vile kubadili milo yetu na kuendelea kufanya mazoezi ya kila siku. Kwa hiyo, hiyo ndiyo mikakati yetu na tutahakikisha kwamba chuo kinaenda ku-emphasize kwenye mikakati ili kuhakikisha kwamba mambo haya yanakaa sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili linahusiana na suala la takwimu. Ameulizia wanafunzi watakuwa wangapi katika ndaki hii pamoja na watumishi watakuwa wangapi? Kwa vile sasa takwimu hizo sina hapa, naomba Mheshimiwa Mbunge aridhie kwamba tukimaliza Bunge hili tuweze kutafuta takwimu hizi na niweze kumpatia rasmi. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Amar.

Na. 122

Hitaji la Chuo cha VETA Nyangh'wale

MHE. HUSSEIN N. AMAR aliuliza:-

9 NOVEMBA, 2022

Je, kuna mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA Nyangh'wale?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Jimbo la Nyangh'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo azma ya kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga Vyu vya VETA katika Wilaya 63 ambazo hazina vyuo hivyo. Kiasi hiki kitatumika pia katika ujenzi wa Chuo cha VETA katika Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyangh'wale ni miongoni mwa Wilaya 63 ambazo zipo kwenye mpango wa kujengewa Vyu vya Ufundi Stadi kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza naipongeze Serikali kwa

9 NOVEMBA, 2022

uamuzi wake wa kujenga VETA katika wilaya 63 ikiwemo Nyangh'wale. Naomba niulize maswali mawili: La kwanza, ni kiasi gani cha fedha ambacho kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa VETA katika Wilaya ya Nyangh'wale? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni lini ujenzi huo utaanza mara moja? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amar, Mbunge wa Nyangh'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo hiki katika awamu ya kwanza kwa sababu vyuo vitajengwa kwa awamu, tumetenga zaidi ya Shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi huu. Suala la lini; hivi sasa tayari Wizara imeshapeleka maombi kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha, tunasubiri upatikanaji wa fedha hizo. Mara tu fedha hizo zitakapopatikana kutoka Wizara ya Fedha, basi huo ujenzi utaanza mara moja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkundi.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa Chuo cha VETA kinachojengwa pale Mhula Jimboni Ukerewe kipo kwenye hatua za mwisho kabisa za ukamilishaji, ni lini Chuo hiki kitaanza kutoa huduma? Nashukuru sana.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swali dogo la Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilikuwa imeanza ujenzi wa vyuo 25 katika wilaya 25 pamoja vile vinne vya mikoa na ujenzi ule upo kwenye hatua za mwisho. Hivi sasa tuko katika ukamilishaji wa vifaa vya kufundishia pamoja na samani ambazo tutapeleka mle madarasani. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka ujao wa 2023 vyuo hivi 25 vya Wilaya na vile vinne vya mikoa vitaanza kutoa mafunzo rasmi.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri: Ni lini Wizara ya Elimu itasaidia kwa dharura ujenzi Kituo cha VETA kule Nyamwaga, Nyamungo, kwa sababu fedha zimeshatengwa tangu mwaka 2021 mpaka sasa hivi imekaa inasubiri tu usaidizi wa Wizara yake? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba ujenzi wa Vyuo vya VETA katika

9 NOVEMBA, 2022

Wilaya 63 tunatarajia kuanza mara tu fedha zitakapopatikana na miongoni mwa maeneo yatakayofikiwa ni pamoja na wilaya yake. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi, ujenzi huo utaanza mara tu fedha hizo zitakapopatikana. Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lemburis, hayupo. Mheshimiwa Furaha.

MHE. FURAHA N. MATONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Ilemela hakuna Chuo cha VETA, lakini wameshaandaa eneo lenye ekari 70.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Ilemela ili kuondoa changamoto kwa vijana wetu ya kukosa ajira? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge anachosema kwamba Wilaya ya Ilemela haina Chuo cha VETA na ni kweli eneo tayari limeshatengwa na tayari tulishakabidhiwa eneo hilo rasmi sisi kama Wizara kupitia wenzetu wa Mamlaka ya VETA. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya hii ni miongoni mwa zile Wilaya 63 ambazo zitapata mgao huu wa fedha hizi awamu ya

9 NOVEMBA, 2022

kwanza kwa ajili ya kuanza ujenzi katika eneo hilo la llemela. *(Makofi)*

Mhesimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asenga, jiandae Mheshimiwa Hassan.

MHE. ABUBAKARI D. ASENKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuzingatia ushauri wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, tayari Kijiji cha Mpanga, Kata ya Kisawasawa, Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Wilaya ya Kilombero, imepata eneo la ujenzi wa Chuo cha VETA.

Je ni lini ujenzi wa chuo hicho utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Asenga, Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spiuka, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya swali la msingi kwamba Wilaya ya Kilombero ni miongoni mwa Wilaya 63 ambazo zipo kwenye mpango huu wa ujenzi wa vyo vya VETA. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, tunasubiri fedha kutoka Wizara ya Fedha. Mara tu fedha zitakapopatikana, basi Wilaya ya Kilombero ni miongoni mwa Wilaya 63 ambazo ujenzi utaanza rasmi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hassan.

9 NOVEMBA, 2022

MHE. HASSAN Z. KUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wilaya ya Tunduru ni kati ya Wilaya ambazo hazina vyuo vya VETA, na eneo la ujenzi wa Chuo tayari tumeshaliandaa na lipo: Je, ni lini Serikali itatujengea Chuo cha VETA katika Wilaya ya Tunduru? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Hassan, Mbunge wa Tunduru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwa wilaya zote 63, ujenzi utanza mara moja mara tu tutakapopata fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Ujenzi huo tunatarajia kuanza kwenye Wilaya zote kwa pamoja ikiwemo na Wilaya ya Tunduru. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Londo.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa nia njema Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilikabidhi Chuo cha VETA pale Mikumi kwa Serikali; na tangu Serikali imekabidhiwa, hakuna ukarabati na Chuo kinaendelea kuchakaa.

Je, ni kanuni au sheria kutowekeza fedha za ukarabati katika vyuo ambavyo Serikali imepewa bure?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri kwa ufupi.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna Chuo cha VETA pale Mikumi ambacho hakijafanyiwa ukarabati na majengo yake ni chakavu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 tumetenga fedha kwa ajili ya ukarabati pamoja na upanuzi kwenye baadhi ya maeneo ambayo vyyo hivi bado havijakamilika au vina miundombinu ambayo ni chakavu pamoja na hiki Chuo cha Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Noah.

MHE. NOAH L. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Je, ni lini Serikali itajenga VETA katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha katika Jimbo la Arumeru Magharibi ambayo tayari tumeshawasilisha eneo kwa ajili ya kujenga VETA?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Mbunge wa Arumeru kama ifuatavyo:-

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi, wilaya 63 ambazo hazina Vyuo vya VETA tunatarajia kuanza ujenzi mara tu tutakapopata fedha ikiwemo na Wilaya ya Arumeru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa George Mwenisongole.

Na. 123

Mgogoro wa mpaka kati ya wananchi na TFS

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa mpaka kati ya wananchi wa Kata ya Itaka na Nambinzo na TFS kuhusiana na Pori la Hifadhi Isalalo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitua Tanzania (TFS) haina mgogoro wowote

9 NOVEMBA, 2022

wa mpaka kati ya msitu wa Isalalo-Lunga na wananchi wa Kata ya Itaka na Nambinzo. Hali iliyopo ni uvamizi unaofanywa na wananchi wachache wanaoingia kwenye hifadhi kinyume cha sheria kwa ajili ya kilimo cha mazao ya muda mfupi. Aidha, ndani ya msitu huu hakuna makazi na Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya msitu kwa kuweka vigingi vikubwa 20 na vinavyoonekana vizuri. Sambamba na hilo, mabango 15 yamewekwa ili kuwakumbusha wananchi kuzingatia sheria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nauliza hili swali hii ni mara ya nne, na kila ninapouliza napata majibu tofauti. Mgogoro huu hauwezi kwisha kwa Serikali kusema kwamba hakuna mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali la nyongeza: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutuma timu ya Maafisa wa Wizara na mimi na yeye kuongozana kwenda kule kuongea na wananchi wa Itaka na Mbinzo na wa Kata ya Isalalo kujua nini kinachoendelea kwa wananchi wale ambao kwa miaka zaidi ya 50 wamekuwa wakilitumia eneo hilo kwa shughuli zao za kilimo? Ahsante (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Sasa umeuliza mambo mawili; atume timu au aende yeye?

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, yote mawili.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Aje yeye, nafikiri ndiyo muhimu. Mheshimiwa Waziri utaambatana naye. Mheshimiwa Condester. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nimesikia majibu ya msingi ya swali hili. Kwanza naomba kabisa kabla sijauliza swali; Mheshimiwa Waziri tunaomba ufanye ziara kwenye vijiji vyetu ili hayo matamko ambayo wewe unayatoa hapa uweze kuwaambia wananchi wenyewe wasikie kama sehemu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu: Je, ni lini Serikali itavimegea nafasi za kulima wananchi wa Itumbula, Ivuna, Mlomba, Itelefya pamoja na maeneo mengine yote ambayo yapo ndani ya Jimbo la Momba ambayo yanahitaji kumegwa kupata maeneo ya kulima kwa sababu maeneo yao yote yamezungukwa na hifadhi na maeneo hayo wananchi wenyewe walitoa kwa Serikali kwa ajili ya kulinda misitu; na sasa hivi wamezaliana? Wataenda wapi ili waweze kulima na kuendeleza shughuli zao?

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni kulinda meneo yaliyohifadhiwa. Kama kuna ombi la wananchi kumegewa, basi walete maombi hayo yataangaliwa, lakini pia na sisi tutaangalia kama maeneo

9 NOVEMBA, 2022

hayo yana vyanzo vya maji, yana shughuli ambazo zinapaswa kuhifadhiwa vizuri, basi tutawataarifu wananchi namna iliyo bora.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Ni bora ukamtembelee kwenye jimbo lake. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Massare.

Na. 124

Kudhibiti Tembo wanaovamia vijiji-Manyoni

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani kudhibiti tembo wanaovamia Vijiji vya Doroto, Kitaraka, Kamenyanga, Gurungu, Muhanga na Njirii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kunusuru maisha na mali za wananchi katika Vijiji vya Doroto, Kitaraka, Kamenyanga, Gurungu, Muhanga na Njirii-Manyoni. Aidha, Wizara imeanza kuimarisha Kituo cha Askari cha wanyamapori kilichopo Kijiji cha Doroto kwa kuongeza Askari, vitendea

9 NOVEMBA, 2022

kazi na kutoa Elimu kwa wananchi juu ya mbinu rafiki za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Doroto ambacho kimetajwa kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kituo kikubwa ambacho kinasimamia *Game Reserve* ya Muhesi lakini hakina gari: Je, Serikali ipo tayari sasa kupeleka gari jipya kabisa katika kituo hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: kuna wananchi ambao walifariki kutokana na wanyama hao wakali katika Kijiji cha Nyabutwa katika Kata ya Mgandu na maeneo mengine mazao ya watu yaliliwa: Je, ni lini Serikali itawalipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa ajili ya kuwafariji wananchi hao kutokana na matukio hayo ya wanyama wakali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshapokea magari 59 ambayo yatasambazwa kwenye vituo vilivyo na athari ya

9 NOVEMBA, 2022

wanyamapori wakali na waharibifu, hivyo nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba *priority* itapelekwa katika Kituo hiki cha Doroto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili lingine la kifuta machozi na kifuta jasho, tulikuwa na changamoto kidogo ya fedha na kufanya tathmini na tayari tumeshakamilisha. Hivyo, wakati wowote tutaanza kulipa wathirika wa changamoto hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mama Kikwete, jiandae Mheshimiwa Malembeka.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa napenda niipongeze Serikali na kuishukuru kwa sababu Bunge lililopita nilieleza kadhia ya tembo ambao wanawaua watu, kula mazao na kuleta uharibifu mkubwa. Naishukuru Serikali kwa kuniletea kile kituo na sasa hivi kituo kimekamilika zaidi ya asilimia 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, niliomba gari na askari. Gari bado sijapata na maaskari bado sijapata, lakini kitu cha kusikitisha, tarehe 6 Novemba, 2022 mwananchi wangu aitwaye Mwanahawa Mohamed Likenge ameuawa na tembo katika eneo la Lucheme Kitongoji cha Ndulima na tarehe 7 Novemba 2022 amezikwa. Sasa kwa kuwa Askari ni wachache, naomba niongezewe Askari ili waweze kufanya *patrol* kuhakikisha wananchi hawa wanapata manusra na hatimaye tujue hatma yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Lindi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitoe pole kwa mwananchi huyu ambaye tulipata taarifa ndani ya siku tatu kwamba ameuawa na wanyama wakali na waharibifu. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maombi yake yote tutayatekeleza kwa wakati; na kwa kuwa tayari tumeshapata magari, basi tutayaelekeza katika eneo hilo na maeneo mengine yenye changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tumeshaanza ku-*train* VGS, hawa Askari wa Vijiji na tayari vijiji tisa tumeshamaliza kuwafanyia mafunzo na hawa wote watapelekwa kwenye maeneo ambayo yana changamoto hii. Tutaongeza askari katika maeneo yenye changamoto na nguvu ili kuhakikisha kwamba tunathibiti wanyama wakali na waharibifu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Malembeka.

MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Manyoni ilitangaza nafasi au fursa ya kuwekeza kwenye Halmashauri yake hususan kwenye zao la korosho, lakini yale maeneo waliyoyapanga ndiyo njia kuu ya kupita tembo. Kwa hiyo, ukipanda, wakipita wanavunja, wakirudi tena wanakula yale majani. Sasa nataka kujua, Wizara hii lini itawasiliana na

9 NOVEMBA, 2022

Halmashauri ya Manyoni ili wale ambao wamepata mashamba kwenye eneo lile ambalo ni njia ya tembo waweze kubadilishiwa? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la msingi sana hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Singida, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uwekezaji wa mashamba ya korosho yaliopo ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa huyu sio Mbunge wa Singida, anaitwa Malembeka, Viti Maalum, ili *hansard* isome vizuri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika,...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malembeka, jina lake ni Mheshimiwa Malembeka.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto ya uvamizi wa wanyama wakali na waharibifu

9 NOVEMBA, 2022

katika mashamba ya uwekezaji yaliyoko Manyoni. Tayari tumeshaanza kuimarisha doria kwa kuanzisha usimamizi wa doria kuzunguka mashamba hayo na tuna mpango sasa wa kuweka kituo ambacho kitakuwa ni kituo cha kudumu kwa ajili ya kudhibiti wanyama wakali na waharibifu.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Juliana Masaburi, kwa niaba Mheshimiwa Katimba.

Na. 125

**Kuwapa vichanja vya kuanikia dagaa wanawake
wajasiriamali – Mara**

MHE. ZAINAB A. KATIMBA K.n.y. MHE. JULIANA D. MASABURI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa Vichanja vya kuanikia dagaa Wanawake Wajasiriamali wa Mkoa wa Mara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kukuza na kuendeleza zao la dagaa na kuliongeza thamani ili liwe moja ya zao kuu la kimkakati litakalochangia katika

9 NOVEMBA, 2022

kuongeza fursa za ajira, usalama wa chakula na lishe na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutimiza azma hiyo, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inatekeleza programu maalum kwa kutumia fedha za mkopo uliotolewa kupitia dirisha la *Extended Credit Facility* kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa; ambapo shilingi bilioni 1.25 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya ubaridi na mitambo ya kuzalisha barafu kwenye masoko saba ya mazao ya uvuvi na ujenzi wa vichanja vya kukaushia dagaa katika mialo mitatu ya kupokelea samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaangalia uwezekano wa kuwajengea vichanja vya kuanikia dagaa wanawake wajasiriamali wa Mkoa wa Mara katika awamu ya pili ya utekelezaji wa programu hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Katimba.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa wanawake wa Kigoma wanaojishughulisha na uvuvi wanahitaji kujengewa uwezo katika mnyororo wa thamani na kuongezewa pia mitaji. Je, ni lini Serikali italeta mradi huu ili uweze kuwanufaisha wanawake wa Mkoa wa Kigoma wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa

9 NOVEMBA, 2022

Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Kigoma na Ukanda wote wa Ziwa Tanganyika, tuna mradi unaoitwa *Fish for ACP* ambao unajumuisha Ukanda wote wa Ziwa Tanganyika. Lengo la mradi huu ni kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi kwenye Ziwa Tanganyika ikiwemo dagaa, migebuka na mazao mengine ya uvuvi yaliyoko kwenye Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Mradi huu unalenga kuongeza ubora, unalenga kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi unaotokea kwenye mialo na kwenye masoko yalioko kwenye ukanda huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tayari, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi huu na mwaka huu tutaendelea; na miaka mingine tutaendelea mpaka ukanda uliye...

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Mheshimiwa Zedi.

Na. 126

Hitaji la Minara ya Mawasiliano ya Simu Kata za Karitu na Ikindwa – Bukene

MHE. SELEMANI J. ZEDI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano ya simu katika Kata ya Karitu na Ikindwa – Bukene?

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) iliifanyia tathmini Kata ya Ikindwa iliyopo katika Wilaya ya Nzega na kubaini kuwa ina changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na hivyo kata hiyo imejumuishwa katika zabuni iliyotangazwa tarehe 24 Oktoba, 2022 kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kata ya Karitu, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote itaifanyia tathmini kata hiyo ili kubaini mahitaji ya mawasiliano na kuiingiza katika zabuni zitakazotangazwa na Mfuko katika awamu zifuatazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa kuiweka Kata ya Ikindwa kwenye mpango wa kujenga mnara katika zabuni iliyopitishwa mwezi Oktoba, lakini nina

9 NOVEMBA, 2022

swali la nyongeza kuhusu Kata ya Karitu. Miaka miwili, mitatu iliyopita, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulifanya tathmini kwenye Kata hii ya Karitu na ukabaini kuna upungufu wa mawasiliano na ukaingizwa kwenye zabuni. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kinachotakiwa kufanywa ni kutangaza upya, kuingiza upya Kata hii ya Karitu kwenye zabuni, badala ya kwenda kufanya tathmini upya kwa sababu kazi ya tathmini ilishafanyika na ndio maana kata hii iliingizwa kwenye zabuni miaka miwili, mitatu iliyopita? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Serikali ilifanya tathmini katika maeneo haya, lakini kulingana na uwekezaji mbalimbali wa makampuni ambayo ni tofauti kabisa na uwekezaji wa Serikali, inawezekana kabisa mahitaji yanayohusika yanaweza kubadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba maeneo ambayo yalikuwa yameshafanyiwa tathmini katika Jimbo la Bukene yalikuwa ni mengi lakini tunaenda hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha. Tayari Kata ya Ikindo imeshaingizwa katika mradi ambao umeshatangazwa tarehe 22 Oktoba. Tunaamini kwamba kulingana na fedha zinavyozidi kupatikana basi na hii Kata ya Karitu na yenyewe itaingizwa katika utekelezaji.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Asia.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika Vijiji vya Katesh, Endagulda pamoja na Yaeda Jimbo la Mbulu Vijijini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi ni lini?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Katesh, Endagulda pamoja na Hhayeda ambayo yanatoka katika Jimbo la Mheshimiwa Flatei Massay, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Asia Halamga kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kufuatilia katika Mkoa wa Manyara, kuhakikisha kwamba huduma ya mawasiliano inaimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, maeneo yote haya yote matatu ambayo ameyataja Mheshimiwa Asia Halamga tayari tumeyaingiza katika mradi wetu wa minara 763.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Hawa, ajiandae Mheshimiwa Kunti.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ujenzi wa Mnara katika Kata ya Itetemia uliokuwa umeanza umesimama kwa takribani miezi mitatu sasa, hakuna mwendelezo wowote. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza ujenzi wa mnara huo ili wananchi wa Kata ya Itetemia waweze kupata mawasiliano? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi sana, muda wetu umeshakwisha, kwa kifupi na maswali yapo mengi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa, Mbunge wa Tabora, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Itetemia na eneo la Itetemia, mradi unaojengwa pale unajengwa na kampuni ya *Halotel* na kwa sababu tulikuwa na changamoto ya vifaa ambavyo vilikuwa vimeletwa lakini vilikuwa vime-miss baadhi ya vipuri. Tumehakikishiwa kwamba vipuri sasa vipo njiani na pindi vitakapofika Kata hii ya Itetemia na mnara wake wa *Halotel* utakuwa kamili na utawashwa kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kunti, ajiandae Mheshimiwa Zaytuni.

9 NOVEMBA, 2022

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Kata ya Kinyamsindo, Lahoda pamoja na Sanzawa zilishafanyiwa tathmini kwa ajili ya kujengewa minara. Je, ni lini sasa wataziingiza kata hizi kwenye zabuni ili zitangazwe na hatimaye wananchi wetu waweze kupata mawasiliano? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Kunti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tuna miradi ambayo inaendelea na pili kuna miradi 763 ambayo tayari Serikali imeshatangza zabuni, lakini vile vile tuna vijiji 216 ambavyo Serikali tayari imeshavifanyia tathmini. Kwa hiyo, tunaamini kwamba kwa kadri fedha itakapokuwa inapatikana, tunaamini kwamba vijiji hivyo, ikiwa pamoja na kata hiyo itaingizwa katika utekelezaji ili kuhakikisha kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi ianendelea kutekelezwa kwa niaba ya Rais wa Tanzania. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Zaytun.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, Serikali haioni haja ya kuimarisha mawasiliano hususan kwenye Wilaya za Mipakani kama Longido na Ngorongoro ambazo bado zina mawasiliano hafifu na muda mwingine wanatumia mawasiliano ya nchi jirani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi sana, jiandae Mheshimiwa Francis.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, samahani sijalisikia vizuri.

NAIBU SPIKA: Hebu uliza tena swali lako.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, Serikali haioni haja ya kuimarisha mawasiliano hususan kwenye Wilaya za Mipakani kama Longido na Ngorongoro ambazo zina mawasiliano hafifu na muda mwingine wanatumia mawasiliano ya nchi jirani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Arusha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi wa *Special Zone and Borders* ambao tayari unaendelea katika utekelezaji wake, labda tutajiridhisha katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema. Tutatuma wataalam wetu kwenda kuangalia kama halipo ndani ya mpango unaoendelea wa utekelezaji wa miradi ya *Special Zone and Borders*. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Francis, jiandae Mheshimiwa Midimu.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Naomba kujua ni lini Wizara itajenga

9 NOVEMBA, 2022

minara katika Kata ya Kikonda, Kinampundu na Mwangeza, ukizingatia Mwangeza wanavamiwa na tembo kila wakati, kwa hiyo wanahitaji mawasiliano kwa ajili ya kuomba msaada? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema hapa awali katika majibu yangu ya msingi ni kwamba kuna miradi mbalimbali inayoendelea. Niwaombe Wabunge, kuna miradi 763 ambayo imeshaletwa Bungeni, lakini pia tuna hayo maeneo ambayo ni 216 ambayo yameshafanyiwa tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliombe Bunge lako Tukufu, wajaribu kupitia katika ile miradi pale ambapo Mheshimiwa Mbunge atagundua kwamba maeneo anayoyasema bado hayajaingizwa katika mpango wa utekelezaji, basi Serikali tutayapokea kwa ajili ya kufanya hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Midimu, jiandae Mheshimiwa Genzabuke.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kata ya Nyaruhande, Shigala, Wilaya

9 NOVEMBA, 2022

ya Busega hazina minara ya mawasiliano, je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika kata hizo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi ni lini? Jiandae Mheshimiwa Genzabuke

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Mkoa wa Simiyu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Nyarukande tayari imeingizwa katika utekelezwaji wa miradi 763. Kwa hiyo tuombe tu kwamba utaratibu utakapofika katika maeneo hayo, basi wananchi waandaliwe kwa ajili ya kutoa maeno kwa ajili ya ujenzi wa minara hiyo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Haya. Mheshimiwa Genzabuke wajiandae Mheshimiwa Maleko na Mheshimiwa Gwajima.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina swali moja; je, ni lini Serikali itaweka minara ya mawasiliano kati ya Manyoni na Tabora?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, lini kati ya Manyoni na Tabora?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Maleko kama ifuatavyo:-

NAIBU SPIKA: Sio Maleko ni Genzabuke.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Genzabuke, kama ifuatavyo:-

NAIBU SPIKA: Au umemuona Mheshimiwa Maleko kule? Ni Mheshimiwa Genzabuke, endelea tu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba eneo la Manyoni - Tabora bado lina changamoto ya mawasiliano na kwa sababu tunatekeleza kwa kadri fedha inavyopatikana, tunaamini kabisa kwamba katika eneo hili, tunalichukua na tunahakikisha kwamba tunaenda kulifanyia tathmini na tuangalie upana wa tatizo jinsi lilivyo ili tukachukue hatua ya kuhakikisha kwamba mawasiliano katika eneo hilo yanapatikana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Malleko.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Mamba Kusini iliyopo katika Jimbo la Vunjo, kuna shida kubwa ya mawasiliano.

Je, ni lini Serikali inaweza kurekebisha tatizo hili?
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupokea changamoto ya mawasiliano katika Kata ya Vunjo

9 NOVEMBA, 2022

ili tukaifanyie tathmini ili sasa tuweze kufikisha mawasiliano katika eneo hilo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gwajima.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na juhudi nzuri za Serikali za kujenga minara, badala ya kujaza Tanzania na utitiri wa minara, ni lini sasa itakuja na teknolojia ya kutumia mnara mmoja ili kuepusha nchi nzima kuwa na utitiri wa minara? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Askofu, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari teknolojia ya kutumia mnara mmoja inatumika hapa nchini. Tunaita *core location*, *core location* maana yake kwamba *Tigo* inakuwepo pale pale, *Airtel* inakuwepo pale pale, *Voda* inakuwepo pale pale, kampuni zote zinakuwepo pale pale. Changamoto inayokuwepo ni katika maslahi ya hizo kampuni wanaposhare wanaona kama vile wananyang'anyana wateja. Kwa hiyo, hii ni changamoto ambayo inawahusu *mobile network operator* moja kwa moja, ambapo wao ndio wanaweza kuamua kwamba waende ku-share ama kutoku-share, kulingana na maslahi ya kibiashara zaidi. Ahsante.

9 NOVEMBA, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliopo Jukwaa la Spika; wageni wa Bunge ambao ni viongozi wa *USAID* wanaondesha Programu ya *Data for Development Project- DDP*, Ndugu Bahati Tenga, Ndugu William Walwa, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Kata ya Bonyokwa wakiongozwa na Diwani wa Kata hiyo, Mheshimiwa Tumike Malilo, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; mgeni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ni Ndugu William Dominician kutoka Karatu Mkoani Arusha, karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt, Dotto Biteko, Waziri wa Madini ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimboni kwake Bukombe, Ndugu Magambo Machimu, karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Deogratius Ndejembu, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utawala Bora ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Chamino, Ndugu George Malima, karibu. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, ambao ni viongozi wa CCM Wilaya ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

Wageni wanne wa Mheshimiwa Angelina Melembeka ambao ni wa familia yake kutoka Msalato, Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 27 wa Mheshimiwa Janeth Mahawanga, kutoka Taasisi za Wanawake na Mabinti Wajasiriamali *(Women Supporting Women and Tuamke Pamoja Tanzania)* kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Stella Mwakibete, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni Wanne wa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, ambao ni wajasiriamali kutoka Jijini Dodoma, karibuni. Mgeni wa Mheshimiwa Daniel Awack, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimbo la Karatu Mkoani Arusha, Ndugu Balele Kilangi. Karibu sana. Wapo wageni Wawili wa Mheshimiwa Juma Hamad Omar ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Ole Mkoa wa Kusini Pemba, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wazee Nane kutoka Mtaa wa Mahomanyika Kata ya Nzuguni Jijini Dodoma. Karibuni sana Dodoma na Bungeni.

Mheshimiwa Agness Hokororo Katibu Mkuu Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania anaomba kuwatangazia Wabunge wanawake TWPG kuwa leo tarehe 09 Novemba, mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge Saa Saba Mchana, kutakuwa na mafunzo kwa Wabunge Wanawake wote. Mafunzo hayo yameandaliwa na Benki ya NBC na yatafanyika katika Ukumbi wa *Four Point Hall* uliopo Kisasa karibu na *Perugina Club*, Wabunge wanawake wote

9 NOVEMBA, 2022

mnaombwa mhudhurie kuanzia Saa Saba baada ya Bunge kuahirishwa. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI-KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Mwijage, ajiandae Mheshimiwa Makoa, na Mheshimiwa Gwajima ajiandae.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia mada iliyoko mbele yetu. Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kukubaliana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mapendekezo haya ya mpango. Mapendekezo haya akizingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, hao ambao nimewasikiliza utakuwa mpango mzuri, tutatoka na mpango mzuri ambao tukijituma, na tutajituma na kuutekeleza tutaweza kutimiza malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na mchango wangu, nichukue fursa hii kutoa pole kwa Watanzania na wananchi wa Kagera kutokana na ajali ya

9 NOVEMBA, 2022

ndege ya Shirika la *Precision Air*, Sina zaidi nianze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili Mpango wa Tatu katika mipango Mitano ya mwaka mmoja mmoja, inayokamilisha Mpango wa Tatu wa miaka Mitano na huu ndiyo mpango wa tatu wa miaka mitano unaomalizia mipango mitatu ya miaka mitano mitano tukiwa tunafikia Dira ya Taifa ya 2025. Kumbé huu mpango wa tatu ndiyo dira yenyewe ya 2025. Ninapochangia nitajaribu kurejea dhima ya mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya mpango wa tatu wa miaka mitano ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Uchumi shindani ni upi? Uchumi shindani ni ule ambao shughuli zake zinatawaliwa na tija kubwa, shughuli zote zinatawaliwa na tija kubwa. Uchumi shindani ni ule ambao una ujumuishi, umma umejumuishwa, lakini shughuli ya ushindani na ujumuishi inakuwa endelevu. Pamoja na uchumi shindani tunajenga viwanda kwa maendeleo ya watu. Hili la maendeleo ya watu niliseme kidogo, watu wengine huwa na kigugumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya watu kuna vigezo vingi lakini kuna hili la afya, tunalisema sana, kuna hili la elimu tunalisema sana, lakini kuna lile la kipato. Unasikia watu wengine wanazungumza sasa tunapojipima lazima tujipime kwa vigezo vyote. Baada ya kueleza hayo, mimi nitajikita zaidi kwa sababu natambua mchango wa walionitangulia hususani Prof. Muhongo, nizungumzie utatuzi wa changamoto za kibajeti na mipango au mikakati ya kukabiliana na changamoto na vihatarishi.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetengeneza mapendekezo ya mpango tutakuja na mpango lakini huenda tusifikie mpango. Ni kitu gani Wachumi wanaita *ceteris paribus* yaani unaweka *assumption* ambazo kama zisipokudhuru unaweza kutekeleza mpango wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie namna ya kukabili vihatarishi. Mojawapo ya vihatarishi Waheshimiwa Wabunge, wengine wamevisema ni suala la mazingira na hali ya hewa. Tumeona nguvu za kidunia mojawapo ikiwa vurugu ya vita ya Ukraine na kupanda kwa bei ya mafuta. Napenda nishauri kwamba Serikali yetu pamoja na kutoa ruzuku lazima tuongeze kasi ya kutumia gesi asilia. Moja, tutumie gesi asilia sana, lakini pamoja na agizo la Mheshimiwa Rais alilolitoa la kutumia gesi kwenye taasisi za Kiserikali, tutumie gesi asilia kwenye taasisi za Kiserikali. Hii itatupunguzia mzigo wa ku-*import products* hali ambayo itaongeza *import bill*. Kwa hiyo gesi asilia ni rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimanjaro Hotel Dar es Salaam wanabeba mitungi kutoka kwenye kituo mama (*mother station*) ya *natural gas*, wanaleta ile mitungi, wanakuja kutumia wanairudisha. Ni mtungi mkubwa, tunaweza kufanya hivyo kwa *radius* ya kufika mpaka Dodoma, tukaweza kufanya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ni hili la mazingira na tabianchi. Kuna suala moja, kuna presha za mazingira zinazotoka nje ya nchi lakini kuna presha za mazingira zinazotoka hapa nchini. Ulilidokeza jana, kuna matatizo yanayotupata sasa kwa sababu tumeharibu mazingira. Katika mapendekezo ya mpango huu, vidokezo vilivyotolewa na Serikali haviwezi kutatua tatizo hili.

9 NOVEMBA, 2022

Mojawapo ya eneo nataka kupendekeza, lazima tuje na sera na sheria ya kuiondoa Tanzania katika utaratibu wa uchungaji wa mifugo, tuende kwenye ufugaji ni suala gumu lakini lazima tulizungumzie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la mikakati ya kuongeza mapato. Kuongeza mapato ni muhimu na suala mojawapo la kuongeza mapato ni ku-*invest* kwenye *re-export*. Tuna *VISA re-export* kutoka Tanzania, lakini tuwekeze kwenye viwanda. Ujenzi wa uchumi shindani na viwanda. Viwanda tunavyovilenga ni viwanda vya Kitanzania, siyo viwanda vya Tanzania, viwanda vya Kitanzania. Mheshimiwa Kakosa alisema jana kwamba tutengeneze mamilionea wa Kitanzania – ndiyo! Tutengeneze viwanda vya Kitanzania kwa sababu hawa wawekezaji wanaotoka nje ni watoto wa kufikia, watarudi kwao wakati ukifika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kusimamia matumizi yetu. Kuna haja ya kuimarisha Idara za Kiukaguzi. Hii idara ya kiukaguzi ipewe uhuru zaidi, rasilimali, itungiwe sheria kusudi Mkaguzi awe na nguvu za kumsimamia yule anayemsimamia. Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri hawezi kusema juu ya Mkurugenzi wake. Hata yule wa Mkoani hawezi, hata Mkaguzi wa Wizarani hawezi kusema kwa Katibu Mkuu. Lazima hii taasisi tuitengenezee sheria, sera na mamlaka na tu-*train* watu wetu kwenye ukaguzi wa leo, waweze kukagua mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakaguzi wetu wamesomea kukagua makaratasi, *hard papers*, wafundishwe zaidi kukagua mifumo hii. Kenya wanao Wataalam wa namna hii karibu 1,800,000 sisi tunao Wataalam kama 200. Kwa hiyo,

9 NOVEMBA, 2022

lazima tuende kwa teknolojia, ndiko hali inakokwenda. Fedha nyingi zinakuja, zinakusanywa lakini namna ya kusimamia hayo matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni Tume ya Mipango. Tunahitaji Tume ya Mipango, moja ni kwamba tunamahitaji mengi lakini tunahitaji kwenda kwa kasi kubwa. Baada ya hayo, naunga mkono hoja naona mapendekezo haya ni mazuri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Makoa, Mheshimiwa Gwajima, ajiandae Festo Sanga halafu atafuata Mheshimiwa Hawa Chakoma.

MHE. ALLY J. MAKOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia huu mchango. Awali ya yote mimi nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukamilisha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi, kwa sababu zoezi hili litatufanya sasa sisi Wasaidizi wake na Viongozi kuweza kutumia vizuri takwimu za watu katika kuhakikisha tunapanga maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye maeneo matatu. Kwanza kwenye sekta ya ardhi. Kutokana na ukuaji wa idadi ya watu kama tulivyoona kwenye taarifa ya sensa, tunagundua kwamba tumeweza kuongezeka kutoka miaka 10 iliyopita kwa asilimia Tatu. Watu wameongezeka kwa idadi ya zaidi Milioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watu wameongezeka kwa kiasi hiki ni lazima Taifa tuweze kuweka mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba mipango ya ardhi inawekwa sawa

9 NOVEMBA, 2022

kwa ajili ya matumizi ya leo na kesho. Kama hatukuweka mipango mizuri ya matumizi ya ardhi leo, huko tunapokwenda kutakuwa na vurugu na migogoro mingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu, ninashauri kwamba mpango ujikite sana katika kuiwezesha Wizara ya Ardhi hasa kule kwenye Tume ya Mipango ili iweze kuongeza kasi ya ukuaji wa upimaji wa viwanja na maeneo ili kuweza kupanga Watanzania na kuondoa migogoro. Leo migogoro mingi inasababishwa na eneo kubwa la nchi yetu kutokupimwa na kupangwa. Kwa hiyo, napendekeza mpango uweke nguvu kubwa katika Wizara ya Ardhi hasa kule kwenye Tume ya Mipango ya Ardhi ili tuweze kufanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwenye sekta ya maliasili. Leo utaona wananchi wengi na Waheshimiwa Wabunge, wakilalamika kuhusiana na migogoro baina ya wanyama na wanadamu. Sasa kutokana na hilo, iko haja sasa mpango wetu ukajikita sana katika kuhakikisha wanaiwezesha Wizara ya Maliasili katika kuhakikisha kwamba wanakabiliiana na majanga kama hayo. Tunapaswa kupanga mipango na tunapaswa kuiwezesha Wizara, kiwango kile ambacho kinaweza kunufaisha Taifa. Mfano, leo Wizara ya Maliasili inachangia asilimia 17 kwenye Pato la Taifa, lakini kiuhalisia ukiangalia vyanzo vya utalii vilivyomo katika nchi haviendani na kiwango cha mchango wa Pato la Taifa la asilimia 17. Hivyo tunataka tuone kwamba tunaweka mipango thabiti kuhakikisha kipato kinachochangiwa na sekta hii ya utalii kinaongezeka kulingana na ukubwa wa vyanzo vyetu vya utalii. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaliwezaje hili? Ni pale Serikali itakapokuwa tayari sasa kuhakikisha wanaweka nguvu kwenye sekta hii. Serikali imefanya vizuri sana katika kuiwezesha Wizara ya Maliasili. Mfano, wamegaiwa magari ya kuweka miundombinu katika mbuga zetu na hifadhi mbalimbali. Je, baada ya mradi ule kuisha, yale magari tunaweza kuyaendesha vizuri yakaendelea kukaa muda mrefu katika maeneo yetu ama kwa ukosefu wa bajeti inawezekana magari yale yakaharibika muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, TANAPA mwanzo ilikuwa inasimamia hifadhi 16, bajeti yao ilikuwa ni Shilingi Bilioni 100. Miaka kadhaa baadae ikaongezewa hifadhi nyingine kufikia hifadhi 22, lakini bajeti ilibaki vilevile. Zoezi la kusimamia hifadhi hizi kwa vyovyote lazima litakuwa ni gumu kwa sababu wameongezewa idadi ya maeneo. Mfano, mwanzo walikuwa na kilometa za mraba 57,333, wameongezewa kilometa za mraba 47,471 lakini bajeti katika kipindi cha miaka mitatu imebaki hiyo hiyo Bilioni 100. Kwa hiyo, ili tuweze kuwasaidia watu hawa wa maliasili waweze kukabiliana na tembo na wanyama waharibifu lazima tuone uwezekano wa kuisaidia Wizara hii ili kuondoa migogoro baina ya wanyama pamoja na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia migogoro ya ardhi baina ya hifadhi na vijiji. Mheshimiwa Rais ametuma Kamati ya Mawaziri Nane katika kuhakikisha wanatatua migogoro. Sasa sijajua huko maeneo mengine lakini juzi mimi nilihudhuria kwenye kikao kimoja cha utatuzi, nilichokigundua, kama Mawaziri Nane hawajachukua lile jukumu lao kikamilifu, wakawaachia watu wa ngazi za

9 NOVEMBA, 2022

Wilaya, migogoro hii haitaisha na itaendelea kuwa mikubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawatasimamia wenyewe wakawaachia kule Wilayani, tutajikuta kwamba migogoro hii haitaisha. Mfano, nimepokea taarifa ya Halmashauri mbili, Halmashauri ya Chemba na Halmashauri ya Kondoa na Halmashauri ya Mji, mapendekezo yaliyotoka Wilayani yana-*double standard*. Mfano wanatoa kaya 411 zote zitoke halafu hazielekezwi kaya hizo zenye watu zaidi ya 1,700 waende wapi. Taarifa inasema waende kwenye Kijiji Mama. Ukienda kwenye Kijiji Mama unakuta kila mmoja ana eneo lake. Sasa kaya hizi kwa taarifa nyepesi nyepesi kama hizi itakuwa hatusaidii badala ya kutatua mgogoro, tutazalisha migogoro mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bado ninatoa rai kwa Serikali iweze kulisimamia hili vizuri ili kuhakikisha inatatuliwa kwa sababu migogoro pia inakwamisha mipango ya Serikali hasa kwa mtu mmoja mmoja na uchumi wa nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye sekta ya uchukuzi. Nilizungumza Bunge lililopita hapa. Barabara hii ya Handeni ambayo nimeikuta pia hapa kwenye mpango huu. Kwa sababu Ilani ya CCM ilitaja barabara hii lazima ifike Kondoa halafu utekelezaji inapitia Chemba. Kwa sababu mipango yote, mpango wa miaka mitano na mpango huu ulielezea barabara hii ipitie kule, basi Serikali ikumbuke jambo hili. Mpango ule wa awali na Ilani inavyosema barabara hii ipitie Kondoa, halafu hii barabara mpya waliyoichonga waiingize kwenye Mpango huu ili na

9 NOVEMBA, 2022

yenye iwe inatekelezwa kwa mujibu wa Mpango na Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyaseama hayo, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gwajima, ajiandae Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwanza ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini kwa maksudi ya kuokoa wakati, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa bidii yake anayoifanya kutusimamia Watanzania na kuhakikisha ndoto ya Watanzania inatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nichukue nafasi hii kuwashukuru vijana wa kutoka Jimbo la Kawe, Kata ya Mabwepande ambao vijana hawa walitembea kwa mguu kutokea Dar es Salaam mpaka Bukoba kwa kusudi la kum-support Mheshimiwa Rais katika juhudi zake. Shukurani zangu ni kubwa sana kwao kwa sababu wametembea kilometa 1,382 kwa siku 35. Wakati wana wa Israel walipokuwa wanatoka katika nchi ya Misri, walisafiri kilometa 405 kwa miaka 40, lakini hawa vijana wamesafiri kilometa 1,382 kwa siku 35, hawa ndiyo mashajaa wa Jimbo la Kawe. Vijana hao ni Abiudi Maugo, Alinda Albert, Saidi Apollo, Idrissa Rajabu, Mossi Fikiri, Kassim Kidole na Bura William, nawashukuru sana hawa vijana wa Jimbo la Kawe. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Nitachangia mchango huu tena na tena mpaka Yesu Kristo atakaporudi tena kama haijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ieleweke kwamba, *Friction* au msugvano ni sehemu mojawapo ya ujenzi, na tujue kwamba msugvano au *friction* ndio ulileta ufumbuzi wa kwanza wa moto. Kutofautiana kimawazo ni jambo la kawaida kama lengo lenu ni kujenga nyumba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaza kwamba pamoja na mpango mzuri ambao Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango aliuwasilisha lakini tunahitaji Mpango wa muda mrefu. Nataka nikubaliane na Mheshimiwa Shabiby aliyechangia jana, kwamba hakuna nchi duniani, narudia tena *there is no country on global* ambayo imeweza kuwavusha watu wake au kuleta maendeleo kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote ambazo zimevusha watu wao zilikuwa na mipango ya muda mrefu na zikaisimamia. Kwa mfano tunakumbuka baada ya vita vya kwanza vya dunia, nchi za Ulaya zote zilifilisika; ni kwa sababu tu Marekeni haikupigana vita hivyo katika nchi yake; lakini zaidi ya nchi 16 Ulaya zilifilisika na zilikuwa zimekwisha kabisa kiuchumi. Kipindi kile alikuwepo Rais wa Marekani anaitwa Truman na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje George Marshall akaweka mpango wa kuziokoa nchi 16 za Ulaya kiuchumi na zikapewa fedha. Na katika mpango wake zikaambiwa kwanza ziandae Mpango wa Maendeleo wa muda mrefu. Nchi zile zikaanda Mpango wa Maendeleo wa muda mrefu katika nchi 16 za Ulaya, ikiwemo Ujerumani na Swaziland.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi yake ya Mpango wa muda mrefu na fedha zilizopata kutokea Marekani wakavusha nchi zao mpaka leo ni nchi za ulimwengu wa tatu, zilikuwa zimefilisika kabisa. Ukimwona mwenzako anatumia farasi fulani wa kumkimbiza kwenda kwenye hatma na wewe ukimtumia farasi huyo huyo atakufikisha kwenye hatma hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashangaa kwa nini sisi pamoja na mipango mizuri ya mwaka mmoja, miaka mitano tunashindwa nini kuwa na mipango ya muda mrefu miaka 60 ya maendeleo ya Tanzania au miaka 70 ya maendeleo ya Tanzania na hii mipango ikavunjwa kwenye vipande vidogovidogo kwa malengo ya kuitimiza. Kwa mfano tumejenga SGR ni jambo zuri na ni safi kabisa. Lengo la SGR ni kwamba tubebe mzigo wa kutosha ili tuiongezee nchi yetu kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mzigo unatokea wapi? Mzigo unatokea bandarini. Kwa hiyo lakini bandari haijapanuliwa bado; tumeanza na SGR na bandari bado ile ile. Kwa hiyo kama tungekuwa na mipango tungekuwa tumeanza kupanua bandari kwanza ili kusudi hii bandari SGR itakapokamilika tuweze kubeba mzigo mkubwa tuupeleke mpaka Kigoma na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa unaona ukweli wenyewe kwamba SGR inaelekea Kigoma, Bandari ya Dar es Salaam ni hiyo hiyo, tumehamia tena Bandari ya Bagamoyo mahala ambapo SGR haipo. Kitakacholazimisha kufanyika tena itabidi tujenge kipande kingine cha kutokea Bagamoyo kwenda kuunga kwenye SGR ili tuwe na uwezo

9 NOVEMBA, 2022

wa kubeba mizigo mikubwa na kuiongezea uchumi nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lisingekuwepo kama tuna mipango. Wakati huo huo hii mizigo mingi ambayo tunataka tubebe inaelekea wapi? tunakwenda mpaka Kigoma tuivushe kwenda Congo. Je, tumeshajiandaa kuivusha mizigo hiyo kutokea Kigoma ama kwa njia ya Ziwa Tanganyika kwenda Congo? hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya muda mrefu ya nchi ndiyo njia peke yake ambazo nchi zilizoendelea zilitumia kuzitoa nchi zao zilipokuwa na kuzipeleka mahala ambapo nchi hizi zilikwenda. Nitoe mfano mwingine, ya kukufanya Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wenzangu kuwafikirisha, kwa mfano tumejenga *Stigler's Gorge* mahala ambapo tutazalisha umeme mwingi ni jambo zuri kwa sababu *power* ndiyo njia pekee ya kuifanya nchi ijenge viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango wa kujenga *Stigler's Gorge* hatukupanga ule umeme tutautoaje hapo *Stigler's Gorge* kuingia kwenye gridi ya Taifa. Mtu yeyote ambaye ni *genuine* nimuulize, je, wakati mnapanga ujenzi wa *Stigler's Gorge* je, kuna bajeti ya kutoa umeme pale *Stigler's* kuingiza kwenye gridi ya Taifa mpango haukuwepo. Hii ni kuonesha kwamba, nasema sisi simlaumu mtu, ni kuonesha kwamba matatizo yetu yanatokana na kukosa mipango ya muda mrefu. Tunapopanga mipango ya muda mfupi *there is no country on the global will ever develop* kwa kuwa na mipango ya muda mfupi.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja ambalo linaweza likamgusa mtu lakini sio kwa ubaya. Ili nchi iendelee haihitaji tu *natural resources*, hapana, nchi kwa mfano Sweden, Denmark, Sweden wanatengeneza scania hawahimbi chuma kama cha kwetu. Japan ndio *supplier* wa magari, *iron* ya Japan ilikwisha muda mrefu wanaagiza chuma kutoka Australia. Ni mipango tu wanayofanya. Lakini sisi tuna *natural resources* za kutosha ila ile akili ya kugeuza *natural resources* kuwa maisha ya wananchi ndiyo hiyo tunapungukiwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri, namwita Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae Mheshimiwa Asha...

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Mimi nitachangia mambo mawili. Jambo la kwanza ni jambo la ATCL na pili litakuwa ni jambo la kilimo na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa sababu mpango wa kununua ndege tano tayari kuna malipo ya fedha ameshayafanya na ndege tano zinategemea kuingia nchini. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie ATCL kwa maana ni nini inatakiwa tusaidie kwenye mpango na kama ambavyo kamati imeshauri. ATCL ina ndege 11 lakini tuna changamoto kubwa sana katika uendeshaji wa Shirika letu la Ndege la ATCL. Changamoto yetu ya kwanza ni kwenye suala la gharama za tiketi. Gharama zetu za tiketi kwenye Shirika la Ndege zimekuwa ziko juu sana, kiwango ambacho hadi Mbunge anafikiria kusafiri kwa ndege anaona ni bora asafiri kwa gari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza kutolea mfano wa gharama ya tiketi ya ndege kutoka Katavi kuelekea Dar es Salaam. Unazungumzai shilingi za Kitanzania 800,000, 600,000, 700,000. Nauli ambayo unaweza ukaitumia kusafiri kuelekea Rwanda na ukaelekea na mataifa mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe kwenye mpango wa Serikali waweze kuisaidia ATCL na kupunguza gharama za uendeshaji, kwa maana ya hizi tiketi. Tunajua ATCL inakodi ndege kutoka TGFA (*Tanzania Government Flight Authority*), ambapo analipa zaidi ya dola 1,500,000 kila mwezi kwa kukodishiwa ndege. Kwa hiyo ni vyema ATCL ikapewa jukumu la kuendesha hizi ndege *in full capacity* ili hizi gharama ziweze kushuka chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mtanzania ukisimama ukamwambia ATCL nauli zake ziko sawa wakati katika nchi hii na Taifa hili tulishaona *fastjet a private company, a private entity* ilishawahi ku-operate na akarusha airbus kwa 100,000, 90,000, 150,000 lakini leo hii ATCL ambayo ni ndege ya Serikali ni kodi za watanzania ina viwanja nchi hii, inapaki nchi hii bado gharama zake za tiketi ziko juu. Kwa hiyo

9 NOVEMBA, 2022

ninaomba kwenye mpango wa Serikali ione ni namna gani ya kuisaidia ATCL. Kwenye ATCL pia, hii ndege Watanzania wanavyoenda kulala saa tatu usiku na ndege zinaenda kulala kwa sababu hazina viwanja vya kuruka vyenye mataa. Kwa hiyo niombe ATCL isaidiwe kutoka kwenye TAA (*Tanzania Aviation Authority*) waweke mataa kwenye viwanja vingi ili ndege zi-operate zaidi usiku kuliko ku-operate mchana. Haiwezekani ukaona ndege 11 tukienda kulala na zenyewe zinaenda kulala (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwenye Mpango wa Serikali, ni fedha chache, ni fedha kidogo kulisaidia Taifa hili mchana watu wafanye kazi, mtu asiwaze *flight*. Ni jambo linahuzunisha sana. Ukienda Bukoba Kiwanja cha Ndege usiku hakitui, ukija Dodoma unaambiwa Kiwanja cha Ndega usiku hakitui, ukienda Tabora Kiwanja cha Ndege usiku hakitui. Ni vyema tukaondoka kwenye hili ombwe tuisaidie ATCL. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tunaomba ATCL pia wasaidiwe *control tower* ziongezoke. Moja ya changamoto kubwa ambayo ATCL inaipata, Mfano Bukoba hakuna *control tower* ya ndege wanatumia ya Mwanza. Ni vyema ATCL, TAA wakaisaidia ATCL iweze kuongeza Tower kuongozewa ndege kwenye maeneo tofautitofauti kama pale Tabora. Kwa hiyo ninakuomba sana shirika hili la ndege ili liwe na msaada kwa nchi yetu, liwe msaada kwa Watanzania na watu waendeleo kupanda ndege kama walivyokuwa wanapanda kwenye Fastjet, wajisikie amani kwenye Taifa hili. saidieni hili shirika, geuzeni madeni yaliyoko kuwa mtaji ili shirika lisonge mbele, wasitumie sehemu ya tiketi kuwa ndiyo sehemu ya kutengeneza faida. *Oncourse* lazima watengeneze faida lakini hatuhitaji muda

9 NOVEMBA, 2022

wote wawe wana-*maximize super profit* kwa kuwaumiza Watanzania ambao walitegemea kodi zao ziweze kuwasaidia kwa ajili ya Taifa lao, huu ni mchango wangu kwenye suala la ATCL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo mengine ni kwenye mpango wa mambo ya kilimo. Tunakubaliana kabisa tuna hekta zaidi ya milioni 29 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Naomba nisema, hatujaona mpango mkakati wa Serikali wa kusaidia kuboresha mazingira. Leo hii tunazungumzia mvua hakuna, hali ya hewa imebadilika. Lakini hatuzungumzii upandaji wa miti kwenye Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tunaenda kuzungumzia umwagiliaji, maji mtatoa wapi kama mvua hakuna? Maana yake ni kwamba lazima tupande miti, ni lazima tuhamasishe Watanzania kupanda miti. *Otherwise* tuseme kwamba tunamsubiri Mheshimiwa Rais aanzishe kampeni ya kupanda miti nchini, wakati Rais anahangaika kutafuta fedha kuna mambo kama Taifa, tuamue tukiwa ndani, Rais ashtukie watu tunafanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mmoja. Tunajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, mimi ni Mbunge wa Makete, Jimbo la Makete ndilo linalo-*offer* maji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tunamwaga maji kuelekea Mbarali, yanatoka Mbarali yanaelekea Ruaha, yatoka Ruaha yanaingia Rufiji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini hakuna mti hata mmoja mliohamasisha, *then* mnategemea mkifukuza wananchi kutoka kwenye mita 60 ndiyo itakuwa *solution* ya kutunza vyanzo vya maji? siyo sahihi. Lazima tuhamasishe upandaji wa miti kwenye Taifa

9 NOVEMBA, 2022

letu. Anzeni kampeni hii mapema, huu ni mpango, tengeni bajeti, na fedha ziko nyingi. Kusafisha *Coco beach* si usafi wa mazingira tu ni kazi ya Halmashauri ya Kinondoni. Kamam Taifa lazima tuwe na mpango mkakati kwa ajili Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili liende sambamba na timu ya Mawaziri nane walivyoenda Mbarali, wamesema kuanzia leo vijiji 48 vilivyoko karibu na Hifadhi ya Ruaha viondoke. Nataka kuita hii *as a Mbarali crisis*, kwa nini? leo hii unaenda kuondoa vijiji 48 kwa sababu tu unasema wako karibu na vyanzo vya maji na wananchi hao kupitia Ilani ya CCM tuliwaambia kwamba tutali-solve hilo tatizo kwa kukaa nao mezani tukiwaambia wanambarali kwa sababu nyie mnalilisha Taifa, kwa mwaka jana tu Mbarali imelisha ekari tani 600,000 za mchele...

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunawaambia watu wa Mbarali vijiji 48 waweze kuondoka...

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, hata kule KIA - KADCO inataka kufuta kijiji kimoja chenye ekari 15,000 na vijiji vingine viwili kwa madai kwamba wako kwenye eneo la Kiwanja cha Ndege na kiwanja hiki kinadai eneo lake ni

9 NOVEMBA, 2022

kilomita za mraba 110,000. Lakini ukubwa wake ni kilomita za mraba 12...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pallangyo sasa unachangia naona.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake. Mbarali vijiji 48 unaviambia viondoke kwenye hifadhi ya maji. Wananchi wamesema tuko tayari kukaa mita 100 ili maji yaendeleo kupita tunajua uhitaji huo. Lakini nizungumze hivi, leo hii tunazungumzia mgao wa umeme kwa sababu ya kupungua maji, leo hii tunazungumzia mgao wa maji kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Leo hii na kesho tunaenda kwenye *Dinner table* ya nchi yetu kwa mgao wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbarali anayelisha tani 600,000 za mchele kwa mwaka unamwambia leo akusanye virago aondoke. Huyu Mbarali ana viwanda visivyopungua 30, huyu Mbarali ana ajira za Watanzania zisizopungua 100,000, huyu Mbarali unayemzungumzia ana makazi ya watu na watoto wako pale, huyu Mbarali amekutwa na GN ya mwaka 2008 wakati wao walikuwepo toka mwaka 1972. Huyu Mbarali unayemzungumzia ni Mtanzania mwenzangu, ana familia na watoto anaosomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri nane wanaoenda kuzunguka kwenye kijiji hiki wanatumia ripoti za maeneo yale ndio wanaenda kuamulia. Tunawaomba msitengeneze vidonda mnakokwenda, nendeni mkaponye matatizo ya Watanzania. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mheshimiwa Mwigulu umesaini mikataba 15 Mbarali yenye thamani ya shilingi bilioni 54 ya umwagiliaji, mmesema yakajengwe mabwawa Mbarali, Waziri wako ameenda kufuta hivyo vijiji 48, mpo mnaleta hapa mpango wa kwamba nyie mmesaini mikataba ya umwagiliaji 48...

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kule mmenda kufuta...

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaenda kujenga wapi hayo mabwawa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sanga kuna taarifa.

T A A R I F A

MHE. ASKF. JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji kwamba kile kitendo cha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kusaini mikataba ya kuwasaidia wananchi, halafu mwingine akaja kukifuta ndicho nachoita kukosa mipango ya muda mrefu. *(Makofi)*

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa. Waziri wa Fedha nachokwambia mikataba 15 uliyosaini yenye thamani ya shilingi bilioni 54 Kamati ya Mawaziri nane imeenda kufuta hilo eneo unalokwenda kujenga hayo mabwawa. Kwa hiyo ujue

9 NOVEMBA, 2022

kwamba Serikali nyie wenyewe hamuelewani sasa sisi wananchi tutaelewanaje sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliwaambia wale wananchi kuwa tutawalinda maslahi yenu, tutalinda haki zenu, tutalinda kwa sababu Mto Ruaha umesimama nyie mlikuwepo. Leo hii Kamati ya Mawaziri nane inaenda kufuta. *We are going to the dinner table of this country* na watu wenye njaa. Wabunge hatuwezi tukakaa hapa tukajadiliana wakati wananchi wetu wako *under crisis* kule. Wabunge hatuwezi tukajadiliana hapa sisi tumeshiba, wenzetu kule wanafukuzwa wanazalisha tani 600,000 kwa maslahi ya watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri, ninamuomba Mheshimiwa Waziri, ninamuomba Mheshimiwa Waziri!...

MWENYEKITI: Waziri wa Fedha...

MHE. FESTO R. SANGA: ... linda maslahi ya wanambarali...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sanga Waziri wa Fedha kasimama.

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake mzuri ambao unatetea maslahi ya wananchi na unanukuu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha

9 NOVEMBA, 2022

Mapinduzi. Nilitaka tu kuweka kumbukumbu sawa, kwamba kwenye yale maeneo ambayo yana mzozo, vijiji vile anavyovitaja tayari ni eneo ambalo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi pamoja na Serikali iliyoko katika wilaya husika wanaendelea kulifanyia kazi ili kuweza kupata suluhu ambayo itaruhusu uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna kazi inaendelea kwenye maeneo yale ambayo yalikuwa na mzozo. Na GN hiyo ambayo unainukuu ya siku nyingi nimepata kushiriki kikao hicho ambacho kinatafuta suluhu ya hizo tofauti za GN; na ilifanyika ziara katika eneo husika la Mbarali. Wananchi walitoa hoja kwamba hoja yao ni hilo jambo la GN. Kwa hiyo nakupongeza kwa mchango lakini naweka kumbukumbu sawa kwamba lile jambo ambalo linazua taharuki linaendelea kufanyiwa kazi na Waziri wa Kilimo yuko hapa ndiye anayesimama jambo hilo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri...

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Hamna taarifa kwa sababu mchangiaji muda wake umekwisha.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie dakika zangu mbili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sanga subiri, muda wako umekwisha pamoja na kuna *pertinent issues* Waziri ameshaliweka sawa, linashughulikiwa na linafanyiwa kazi. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma,

9 NOVEMBA, 2022

jiandae Mheshimiwa Waitara, jiandae Mheshimiwa Mageasa.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu, nikushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi. Nipende kwa kuanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lake zuri, na mchango wangu wa kwanza nitapenda kuanza kuangazia deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba zote mbili zilizowasilishwa katika Bunge lako tukufu, ile ya Kamati ya Bajeti pamoja na ya Mheshimiwa Waziri zinatambia kwamba deni la Taifa limekuwa likiendelea kukua ama likiongezeka hadi kufikia trilioni 71.56 kutoka ile 64.50. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunaambiwa deni hili ni himilivu kwa viwango vya Kimataifa, ni vema sasa tuka-focus na tukapigia jicho zaidi kwenye miradi ya kimaendeleo na miradi ya kimkakati. Lengo ni kufanya miradi hii iweze kurudisha *return* ya haraka kwa mkopo huu wa shilingi trilioni 71.56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii mikubwa ni miradi itakayosaidia kusimamisha uchumi wa nchi. Kwa hiyo, tukiacha sababu zile ambazo ziko dhahiri shahiri zinaonekana, lakini tuondokane na sababu za hapa na pale zinazopelekea kuchelewesha miradi hii ama sababu zinazopelekea miradi hii kwenda kuongezeka thamani ya fedha ukilinganisha na hile thamani ya mwanzo tuliyongia

9 NOVEMBA, 2022

katika mikataba hii pale awali. Kwa kufanya hivyo tutaweza kukuza uchumi, tutaweza kukuza pato la Taifa na pia tutaweza kukuza ajira na fedha za kigeni. Haya yote kwa pamoja yatafanya uchumi wetu uweze kuwa *stable* zaidi, jambo ambalo litatusaidia sasa kupanga na kubajeti masuala mazima ya elimu, afya pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili upo katika eneo la mfumuko wa bei. Ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wake wa nne, ameelezea kwa namna gani mfumuko wa bei umekuwa ukiongezeka hususan kwenye bei za bidhaa ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko kubwa, tena kubwa sana, kutokea asilimia 3.6 mpaka asilimia 7.8; kilo ya mchele imeongezeka, kilo ya unga na mahindi imeongezeka; hivyo ni vyema sasa tukajikita kwenye mpango huu tunavyopanga mpango huu wa maendeleo, tukaangazia zaidi eneo hili kwani ndiyo eneo linalowagusa Watanzania wengi. Mtanzania wa leo anahitaji unga, maharage na mchele, lakini ndiyo sehemu ambayo bei imekuwa ikiongezeka kwa kasi. Kwa maana hiyo, hapa Mheshimiwa Waziri ni lazima afuate ushauri uliotolewa na Kamati juu ya suala zima la kuanza kutumia gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine namwomba Mheshimiwa Waziri, hebu atusaidie na alisaidie Taifa, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, kila mwezi anatoa ruzuku ya Shilingi bilioni 100 ili kwenda kuongezea kwenye bidhaa za nishati pamoja na *fuel*. Jambo la kusikitisha hapa, na kimsingi ni kwamba uongezwaji huu wa hii Shilingi bilioni 100 kila mwezi, ili iende ikapunguze usafirishaji pamoja na

9 NOVEMBA, 2022

uzalishaji, jambo ambalo litasaidia bidhaa sokoni angalau zishuke bei. Cha ajabu bei ndiyo zimekuwa ziki-*shoot* kwa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri akija atuambie nini faida ya hii Shilingi bilion 100 anayoitoa Mheshimiwa Rais kila mwisho wa mwezi kwa ajili ya kwenda kupunguza makali kwenye nishati na kwenye *fuel* ilhali bei za bidhaa ya chakula inapanda kila leo? Kwa hiyo, atakapokuja hapa, naomba anipatie hayo majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusiana na mikopo ya sekta binafsi. Tunakubaliana sote hapa kwamba sekta binafsi ni kichocheo kikubwa na kichocheo kizuri cha uchumi wa nchi yetu. Tunashukuru kuona kwamba mikopo kwenye sekta binafsi imekuwa ikiendelea kukua kutoka Shilingi trilioni 20 mpaka Shilingi trilioni 24. Ila ukija kwa upande wa riba, riba tunashukuru inapungua, lakini inapungua kwa kiasi kidogo, asilimia 0.19. Sasa kwa mipango na maendeleo tunayotaka kupanga ya nchi yetu, kwa upunguaji huu wa riba tutasababisha kukosa wawekezaji wa kutosha na wakopaji wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikuwa tunaiomba Benki Kuu na mabenki kukaa na kuangazia tena namna bora ya kuendelea kupunguza kiwango cha riba ili tupate wakopaji na wawekezaji wengi. Nia na madhumuni ni ku-*boost* uchumi wa nchi yetu, ajira zipatikane kwa wingi, kuingiza fedha za kigeni na katika yote tuweze kulisaidia Taifa hili kuweza kuwa na uchumi *stable* katika kupanga maendeleo endelevu.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu Bandari ya Bagamoyo. Sote tunafahamu kwamba bandarai ndio lango kubwa la uchumi na upanuzi unaofanywa kwenye Bandari ya Dar es Salaam imeishafika mahali, wanasema *point of no return*. Kwamba mbadala wa Bandari ya Dar es Salaam ni Bandari ya Bagamoyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa SGR unaoendelea unahitaji Bandari ya Bagamoyo. Uchimbaji wa Makaa ya Liganga na Mchuchuma utahitaji Bandari ya Bagamoyo, ukuaji wa uchumi wa nchi yetu unahitaji Bandari ya Bagamoyo, yaani ni Bandari ya Bagamoyo, Bandari ya Bagamoyo. Tukilala Bandari ya Bagamoyo, tukiama Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri, nimepitia Mpango nimeona tu nyota nyota. Nataka uje uniambie Mpango unasemaje kuhusiana na masuala mazima ya Bandari ya Bagamoyo? Vilevile nataka uje uniambie kuhusiana na kulipa fidia ya watu wa Bagamoyo ili tukawekeze kwenye Bandari ya Bagamoyo. Naomba unipe majibu, kwa sababu mradi huu wa Bandari ya Bagamoyo tayari kulishakuwa timu, tayari kulishakuwa na kikosi kazi na makubaliano, nitapenda uje uliambie Taifa, ile timu ya *negotiation* iliishia wapi? Tunataka tupate maelezo ya kina kuhusiana na Mradi wa Bandari hii Bagamoyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bagamoyo utaenda uta-boost uchumi wa hii nchi, utateka masoko ya Jirani na utafungua ajira pamoja na kufanya tupate fedha za kigeni za kutosha. Tukiimarika hapo, hatutakuwa

9 NOVEMBA, 2022

tunajenga madarasa halafu tunashindwa kuwaboresha walimu stahiki zao. Ili tuweze kuwa na elimu bora, tunapaswa tujenge madarasa, mishahara ya walimu tuiboreshe, ndivyo tutakapoweza kupata elimu bora. Suluhisho ni huu mradi wa Bagamoyo utakaotuletea uchumi kukua kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaenda na vyote; tunajenga zahanati, tunapata vifaa tiba na *at the same time* stahiki za watumishi zinaboreshwa, lakini tukiwa tunafanya mipango yetu, eti tunajenga tu zahanati halafu vifaa tiba hatuna, *work done is equal to zero*. Tukiwa tunafanya mipango yetu, tunajenga madarasa halafu walimu hakuna, *work done is equal to zero*. Kwa hiyo, lazima mipango hii iende sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza napenda sana kuipongeza Serikali na kuiomba ipokee ushauri huu ambao tunaweza kuipatia ili kuweza kusongesha maendeleo ya Taifa letu mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushuru, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara, jiandae Mheshimiwa Tumaini Magessa na Mheshimiwa Kawawa ajiandae.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, pia na mapendekezo kwamba ataendelea kumaliza miradi ile ya

9 NOVEMBA, 2022

kimkakati kama SGR, Bwawa la Mwalimu Nyerere na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ya maendeleo ya nchi yetu, ni vizuri tukatumia fursa pia ya kuwa na watu wengi. Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 inaonesha kwamba tuna Watanzania milioni 61.34 ambao wanawake ni milioni 31.24 sawa na asilimia 50.9 na wanaume tupo milioni 30.1 sawa na asilimia 49.1; na nguvu kazi ya Taifa ni asilimia 55.9; na ndiyo maana tunazungumza hapa, kuna njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba ukifuatilia hata katika familia zetu, jamii zetu za kawaida, ni watu wachache sana wanafanya kazi. Kama kuna mtu ni mtumishi au mfanyabiashara, unakuta watu wengi wanamtegemea. Sasa hao watu ambao wameongeza ni vizuri ukawatumia kama fursa pia. Maana yake tuwekeze kwao kwa kuwawezesha kufanya kazi ambazo angalau hata pato la mtu mmoja mmoja ataweza kujitegemea na kuchangia kidogo katika pato la Taifa ili kupunguza mzigo kwa watu. Hatuwezi kuona watu wameongezeka, watu milioni 61 halafu tunapata njaa na watu wapo mtaani wanazurura tu. Watu wanakaa vijiwani tu, wanataka tu kupiga mzinga, nipe mia tano, nipe buku, na maisha yanaenda. Sasa nadhani ni muhimu tuangalie jambo hili na kujua kwa nini watu hawafanyi kazi? Nini kifanyike ili watu waweze kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watu wa kutosha, wana nguvu, wala hata siyo wagonjwa; wagonjwa ni wachache, lakini kwanini kuna njaa? Nadhani jambo hili lichukuliwe hata nje ya mpango huu lijadiliwe. Ukitembea mtaani watu

9 NOVEMBA, 2022

wapo saa mbili asubuhi wanazurura, hawafanya kazi, tunagombana bure tu. Hata ukienda ukaombwa hela usipotoa maana yake ni adui yako. Sasa hili siyo jambo ambalo kwa kweli tunaweza tukalifanya liendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata watu wa kutosha, wafanye kazi, wajilisce wenyewe, wachangie, na walipe kodi. Ndiyo maana watu hawalipi kodi, kwa sababu kama mtu hafanyi kazi, ukimdai kodi atalipa nini? Wanakamatwa vijana wenye nguvu, wenye utashi, eti ni wazururaji; kwanini? Hana kazi ya kufanya? Nadhani hili jambo lifanyiwe kazi vizuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kuna Watu wa TASAF. Mpango wa Serikali ulikuwa ni kuwawezesha watu ambao ni kaya masikini, wanawezeshwa fedha kidogo kila mwezi, lakini wa-graduate kutoka hatua ya kuwa masikini zaidi. Kulikuwa na miradi midogo midogo; miradi ya kilimo cha umwagiliaji, ili mwisho wa siku hii tabia iishe. Siyo sawa, ukienda kwenye kata zetu, kwenye vijiji siku ambazo zimepangwa akina mama, vijana, wazee vikongwe wanakaa wanasubiri fedha, shilingi 30,000 mpaka shilingi 35,000 kwa mwezi mzima. Ukikaa pale ukaangalia, yaani Tanzania hili jambo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu ambao wana uwezo wawezeshwe watoke kwenye hiyo hali, tusaidie watu ambao kweli wana uwezo mdogo na tuweze kuwa-*monitor*. Kuna mchezo ambao wale ambao hawana uwezo hawapewi fedha, wale wenye uwezo wanapewa pesa. Majina yamegeuzwa chini juu. Hili nalo lifanyiwe kazi vizuri sana. Huwezi kuwa na Taifa ambalo watu wao wanasubiri mwezi mzima waende kupiga foleni eti wapewe shilingi

9 NOVEMBA, 2022

30,000, inatosha kitu gani? Hivi kwa mfano kiroba shilingi ngapi unanunua? Zaidi ya shilingi 50,000! Haisadii! Ni hela kidogo sana, lakini udhalilishaji ule; kwa sababu mtu anakaa pale; kwa kweli hili tuliangalie, lifanyiwe kazi. Taifa ili liweze kuendelea ni lazima watu wafanye kazi na mtu wa kusaidiwa kweli atambulike na anayepaswa kupewa msaada, apewe msaada. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge mchangiaji. Nadhani jambo analolisema Serikali imekusudia kufanya hivyo hivyo. Naomba tu nimpe taarifa kwamba Mpango huu wa Kaya Masikini lengo lake ni hilo hilo, kwamba ni kuziwezesha zile kaya masikini, lakini baada ya muda zina-graduate; na zikisha-graduate zinatoa fursa kwa wengine ili waingie na mwisho wa siku wengi watakuwa wameboresha hali zao za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Ushahidi, nataka tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kufanya utafiti na kufanya tathmini ya Mpango wa *TASAF* mpaka sasa tayari tunazo kaya zaidi ya 1,000 zinazoanza kuandaliwa ku-graduate kutoka katika Mpango wa *TASAF* kwenda kujitegemea hili kaya nyingine zisizokuwa na uwezo

9 NOVEMBA, 2022

ziingie na mwisho wa siku ziweze kujitegemea. Hizi kaya zinazopewa hizo shilingi 30,000, shilingi 12,000, shilingi 22,000, upo uthibitisho wa wanakaya wameweza kuanzisha miradi ya kimaendeleo na ya kiuchumi ambayo imeweza pia kusaidia kwenye jamii.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara, muda wako umelindwa.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Waziri nimekusikia, naomba uchukue mawazo yangu yafanyiwe kazi. Bado kazi iliyofanyika ni ndogo sana sehemu kubwa watu wetu kuna hiyo hali ambayo nimeizungumza. Sitaki kubishana na Serikali, nakubaliana kwamba tuendeleo kufanya kazi na ni-recognize kwamba kuna maeneo wame-graduate na kuna watoto wamesaidiwa na wamesoma. Nikasema ukienda kuangalia namna ambavyo wamekaa pale, wanasubiri hicho kiasi kwa kweli, bado inabidi tufanye kazi zaidi na Serikali itoe ushirikiano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwenye mpango zimetajwa baraba za vijijini na mijini kwa maana ya TANROADS na TARURA. Nilikuwa nataka nishauri kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ukienda kwenye Majimbo yetu Vijijini, Barabara za Vijijini nyingi hazihitaji hata kuwekwa lami. Unakuta Mbunge anakosa hata grader aweke mafuta hata Mfuko wa Jimbo au dau aweze kulima barabara, lakini barabara moja kila mwaka inatengewa fedha nyingi sana shilingi milioni 500, shilingi milioni 300 au shilingi milioni 700 wanalima, kila mwaka au kila baada ya miezi sita, na malalamiko ni mengi sana. (Makofi)

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini msitenge fedha hiyo mnunue magreda na ma-*compacter* mgawe kwa kila Jimbo ili wale ma-*engineer* wa *TARURA* walime barabara kwa bei nafuu, unaweza ukapata mdau ukajaza mafuta kwenye *grader* badala ya kukodi. Hapa tunapiga *mark time*, nunua magreda mpe kila Mbunge kwenye Jimbo aajiri ma-*engineer* walime barabara kwa gharama ndogo. Halafu kama ni mpango mkubwa wa kuweka lami au changalawe, tangaza mkandarasi afanye kazi hiyo. Utaokoa fedha nyingi sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na pia huduma itapatikana katika Majimbo yetu na malalamiko mengi ya Wabunge yatapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, katika hotuba ya Mheshimiwa ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 27 amezungumzia uchumi shindani na shirikishi. Mheshimiwa Waziri, kwa mfano ukienda kule Sirari, tuna eneo tumetenga muda mrefu kwa ajili ya Soko la Kimataifa la Mabwe. Huduma zote kutoka Kanda wa Ziwa zinatoka katika mpaka wa Sirari. Ukijenga pale soko, bidhaa zote kutoka Kenya utapata mapato na fedha hiyo itaraudi haraka sana na uchumi utapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuomba ukienda kule Nyamuhonda, mpaka Sirari, na Itiru kumtoa mwananchi wa kawaida ambaye anataka mifuko miwili ya *cement* au mabati aende kulipa ushuru Sirari ni mbali sana. Tuwee fedha ndogo ili watu waweze kulipa kodi, tuweze kupata fedha katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumze katika huu uchumi shirikishi, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Watanzania na Serikali, ni

9 NOVEMBA, 2022

kwamba Wizara ya Maliasili ina lugha yake, Wizara ya Maji ina lugha yake, Wizara ya Kilimo wana lugha yao, Wizara ya Ardhi wana lugha yao. Tunazungumza uchumi shirikishi; mimi nina mfano, halafu tunajadili hapa mambo ya Watanzania watu wanaongea Kichina, Kihindi, kama Wamarekani au Wacanada, kama wamezuka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, mfugaji ukienda ukachukue ng'ombe zake 30 ambapo ng'ombe mmoja ni Shilingi milioni tatu, unazungumza karibu Shilingi milioni 90 umemnyang'anya, halafu umeenda umetaifisha, na eneo hilo huyu mtu hana sehemu ya kunywesha maji ng'ombe zake, hana sehemu ya malisho, hana sehemu ya soko, mifugo hiyo ndiyo benki yake. Huu uchumi unaozungumzwa shirikishi siyo sawa. Hapa kila Mbunge ana malalamiko. Nimefuatilia sana ziara za Waheshimiwa Viongozi wetu, wanatoa maamuzi kana kwamba wao sio Watanzania. Hivi unafuta Kijiji, halafu wale wananchi wanaenda wapi? Huyu Mbunge aliyempigiwa kura wanakwambia tulikuchagua wewe halafu tumefutwa, turudishie kura zetu; unafanyaje? Hili jambo naomba Serikali ilichukue *very serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza mwezi wa Tisa uliopita, kule katika Jimbo langu wamekusanya ng'ombe kutoka Nyanungu, Nyarokoba, Kuyancha wameenda wametaifisha ng'ombe, wanasema hazina mwenyewe, watu wangu wanalia; halafu tena tarehe 15 mwezi wa Kumi wamekusanya nyingine, na ninapozungumza ziko hifadhini. Jua limekausha maji, *only source* ya maji ni Mto Mara, hakuna sehemu ya kunywesha wale ng'ombe, wamewekwa pale ndani; kuna maji ya chumvi, hawasikilizwi, hawaendi. Sasa huyu mwananchi wa

9 NOVEMBA, 2022

kawaida ambaye mtoto wake yupo sekondari, yupo chuo, angeuza mfugo amsaidie, sasa hawezi; chakula hana, angeuza ng'ombe apate chakula; anaishije ndugu zangu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Viongozi na Mawaziri mtusikilize. Mnaenda kwenye Majimbo, sikilizeni watu. Hawa sio Wanyama, tuzungumze na Watanzania wenzetu, haitafurahisha; kuna watu hapa wanaitwa chawa, ukichangia jambo hapa badala yakujadili hoja, wanakujadili wewe. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaombe, mlinda uchumi wa Watanzania, halafu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara! Mheshimiwa Waitara!

MHE. MWITA M. WAITARA: *(Hapa Mheshimiwa Waitara aliongea nje ya microphone)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara! Mheshimiwa Waitara kaa chini!

MHE. MWITA M. WAITARA: *(Hapa kipaza sauti kilizimwa)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara kaa chini. *(Makofi/Kicheko)*

9 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Mkianza kutumia muda wa watu wengine, makofi haya mliyopiga nyie mtakosa nafasi kuchangia ya kwenu. Mwelewe vile vile, kama Mbunge kapangiwa dakika kumi, ni dakika kumi. Kama ana ziada, anaandika, anampa Waziri mhusika. Kwa sababu akitumia dakika 13 mtapunguziwa ninyi kuchangia. Sasa nikimpunguzia Mheshimiwa Kawawa muda wake atakubali kweli! Mheshimiwa Kawawa, utakubali?

MHE. VITA R. KAWAWA: Sikubali!

MWENYEKITI: Eeh, lazima tuwe na nidhamu. Kanuni hizi lazima tuzifuate. Kama hatuzifuati kanuni hizi, hatuna Bunge hapa. Mpira dakika 90, wewe unataka ufunge goli dakika 91; unashikilia tu ufunge goli, *it doesn't work in that way*. Pamoja na kwamba hoja unayozungumza ni ya msingi, tuheshimu kanuni tulizojiwekea wenyewe humu ndani. Sawa Mheshimiwa Waitara!

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa, nimeheshimu kiti.

MWENYEKITI: Haya sawa, ahsante, kaa. Mheshimiwa Magessa, jiandae Mheshimiwa Kawawa. *(Makofi)*

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipatia nafasi hii. Vilevile namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Mwaka 2023/2024. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kutuletea Mpango huu.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kabisa, kwa sababu Dira ya Taifa ya 2025 inaenda kwisha nilitegemea nione kuna mahali panaonesha kwamba sasa tunaanza Dira ya Taifa nyingine mpya ambayo wengine wanaiita ya muda mrefu, wengine sijui wanaita nini; kama ni ya miaka 50 ndiyo tutafanya *break down* ya namna gani tutafanya kazi. Hii ishirikishe wananchi na wadau mbalimbali ili kusudi tuwe na dira ambayo itakuwa ni shirikishi. Kwa hiyo, naomba sana kwenye Mpango huu nione mahali ambapo kwenye bajeti zetu tunaingiza hiki kitu kwasababu tumebakiza nafikiri mipango miwili na hii itakuwa inakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukurasa wa nne wa Mpango wa Mapendekezo tuliyoletewa hapa, utagundua kuna takwimu za ukuaji wa uchumi katika Mataifa yetu haya kwa maana ya *East Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukienda ukurasa wa nne wa Mpango wa Mapendekezo tuliyoletewa hapa utagundua kuna Takwimu za Ukuaji wa Uchumi katika mataifa yetu haya kwa maana ya *East Africa*. Kumbukumbu zangu ambazo nimezitoa hapo zinanionesha Kenya mwaka 2019 uchumi wao ulikuwa unakua mpaka 4.9, mwaka 2020 ikaenda *negative* 0.3, mwaka 2021 wameenda 7.2, maana yake waemsukuma kwa nguvu 7.2 unaongeza na 0.3 wameenda 7.5. Nchi ya Rwanda walikuwa 9.5 ilivyofika 2020 wakaenda *negative* 3.4, lakini 2021 wakaenda 10.2. Ukienda Sudani walikuwa 0.9 wakaenda mpaka *negative* 6.6 kwa sababu ya corona, lakini wamekwishajivuta wamekwenda mpaka 5.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tulikuwa 7.0 hatukwenda kwenye *negative* tulikwenda mpaka 4.8 na

9 NOVEMBA, 2022

tumejivuta tuko 4.9 maana yake tumeongeza 0.1. Uganda walikuwa na 7.2 wakaenda mpaka *negative* 1.4, sasa wamefikia 5.1 maana yake wamekwishakwenda kama 6.5. Burundi walikuwa 0.8 wakashuka mpaka 0.3 sasa hivi wamekwenda 2.4 maana yake wameenda 2.7. Sisi tunakua kwa 0.1 mpaka 0.4 maana yake kuna tatizo hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuunge mkono ndugu yangu jirani yangu hapa Mheshimiwa Mwijage anaposema tuwe na Tume ya Mipango. Jana Mheshimiwa Ndugulile alisema Tume ya Mipango, maana yake hatujagusa mahali ambapo uchumi wetu unaweza kuchangamka, tunagusa, lakini tunagusa kwa kukua kwa 0.1, maana yake *data* haziwezi kudanganya ukuaji wetu ni mdogo kulinganisha nan chi zote za *East Africa*. Maana yake tunachokifanya sisi hatujagusa mahali pake. Ni wapi hatujagusa, ni kwa sababu hatujaingiza pesa ya kutosha kwenye *productive sectors*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na majibu rahisi kwenye maswali magumu. Tunatakiwa kwenda na wenzetu kwa sababu tunaenda kwenye mikutano, tunazungumza nini wakati wao wamekuza kwa 7.5 sisi tumekua kwa 0.5 au 0.4? Maana yake sisi tunavutwa badala ya kuendelea kutembea na wenzetu, sisi tunavutwa nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika robo ya kwanza ukuaji wetu wa pato la Taifa unaonekana umekwenda kwenye 5.2, maana yake tuna-*predict* kwenda kwenye 5.3 ndio maoteo yanavyoonesha. Kwa hiyo, hata malengo yetu ya ukuaji ni madogo, yaani ukijiwekea malengo madogo unategemea *process* yako nayo itakwenda kwenye

9 NOVEMBA, 2022

malengo madogo. Kwa mfano, tunategemea kuona Ziwa Viktoria linashughulikiwa kufanya umwagiliaji wa kilimo chetu. Sijaona mahali popote tumeanza kumwagilia kwa Ziwa Viktoria. Tunasema tu mvua hainyeshi, kule maji yapo, kwa nini tusianzishe skimu ambazo zinatoa maji Ziwa Viktoria, zinatoa Nyasa, zinatoa *Lake Tanganyika* badala ya kuanza kushughulika na maji ambayo ni *non predictable?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu wazi Mpango huu naomba uangaliwe vizuri tunapoenda kwenye utekelezaji wake, lakini Mpango huu umekuwa mara nyingi Mipango yetu ya Miaka Mitano, hoja yetu kubwa ilikuwa ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani. Tuna miradi mingi sana tumeisema, iko mingi sana ambayo imefanyika ya barabara na niseme tu wazi kama kuna mahali ambapo pamoja na mambo tuliyoyafanya mwaka jana na bajeti yetu bado ile ahadi ya kuongeza mtandao wa umeme kwenye vijiji vyetu ya kilometa mbili haijafanyika. Kwa hiyo, uwezo wa wananchi wetu ku-access umeme bado ni kilometa moja ile ya kwanza, tuwaongezee hizo kilometa mbili ili uchumi huu uweze kuchangamka, bila hivyo hauwezi kuchangamka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile vijiji ambavyo tuliona bado havina umeme vipate umeme. Yako mambo mengi ambayo yameandikwa kwenye ripoti yako kwenye *page number 21* na TEHAMA. Watu wamekuwa wanazungumza hapa, inaonekana kilimo wanasema neno lao, tunataka Wizara hizi zisomane, *zi-communicate*. Kwa mfano, unachimba bwawa la maji, bwawa la maji tunategemea mtu wa kilimo atafanyia *irrigation*, wananchi watakunywa maji, lakini mifugo watawekewa sehemu zao za kunywa

9 NOVEMBA, 2022

maji. Utakuta Wizara ya Mifugo inashughulikia bwawa lake, Wizara ya Kilimo bwawa lake, *there is no communication*, hawa watu wa-*communicate* ili matumizi ya Serikali yaende chini. Nategemea haya mambo niyaone kwenye hiyo nani hii iliyoletwa hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na moja, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma, hapa ndio kuna changamoto. Natoka kanda ya ziwa, naomba niseme ukweli, tulikuwa na *ginnery* 11 kule NCU, hakuna hata moja inayofanya kazi. Unategemea tunaposema tunataka tuuze *processed goods* kutoka kwa hawa watu ambao viwanda vyote 11viko chini watafanya nini? Kwa hiyo, kuna kitu cha kufanya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri niseme tu kama *story*, nilipita juzi mahali fulani kwenye *ginnery* nikakuta usiku saa 4.00 wanafanya harusi, yaani sehemu ambayo walikuwa wanazalishia pamba, kuna harusi na watu wanastarehe, yaani inaonekana kabisa tumekwishatoka kwenye reli tuko mahali pengine. Turudi kwenye reli sasa kwamba, *at least* huko tunakotoka kwenye *ginnery* 11 angalau *ginnery* tatu zifanye kazi, tuwe na mambo ambayo sasa yanaonekana tunaweza kujenga uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza nimeisikia imelia, niseme wazi kwenye *production sector*. Wenzetu Waganda, nilikuwa namsikia ndugu yangu hapa, hata uki-*surf* kwenye *internet* utagundua kwamba, wao kwenye *diary export* yao wana dola kama milioni 220 ambayo ni milioni 500 wana-*export* kwa mwaka mmoja, sisi tuna-*export zero* na tunataka tuchangamshe uchumi. Wale ambao

9 NOVEMBA, 2022

wanajua nilikuwa natembea juzi nafanya mazoezi, ofisi ya watu wa maziwa Tanzania iko pale kama unaenda stendi ya hapa Dodoma hapa, ukifika tu unajua hapa hamna kitu hapa, ukiiona tu ofisi unajua hamna kitu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme wazi kuna kitu cha kufanya. Lazima tukubali tunakwenda ku-*invest* ili tupate kitu fulani kwa sababu, wenzetu kama wanauza bilioni 500, sisi tunauza sifuri halafu tunategemea huu uchumi wetu utakua haraka, haitawezekana. Kwa hiyo, niwaombe sana kwenye mipango hii sasa tujue kabisa tunekwenda kufanya nini kwenye *productive sector* na ionekane na haya tukayatekeleze, tutaona uchumi huu ukiwa umechangamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema kuna kuimarisha mifumo ya upatikanaji kwenye kilimo na sasa wanasema kule kwamba, kuna *guarantee scheme* ya wakulima wadogo, mimi sina uhakika, labda ninakotoka Wabunge wenzangu wanaweza kusema; wanasema wameandaa *guarantee scheme*, yaani skimu inayoshughulika na wakopaji wadogo kwa ajili ya kilimo, sijaiona hii, lakini kwenye mpango huu naiona imeandikwa kwamba, inaonekana kuna mpango huo. Kwa hiyo, haya mambo mengi mazuri yaliyoandikwa yawe *implemented...*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa sasa ni nafasi ya Mheshimiwa Kawawa, Mheshimiwa Mkumbo hayupo ataendelea Mheshimiwa Bonnah, akitoka Mheshimiwa Bonnah ni Mheshimiwa Zaytun.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nichangie mchango wangu kwa kuanza kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na mambo mbalimbali ya msukosuko wa uchumi duniani, lakini inafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli takwimu hapa zinaonesha kwenye ukuaji wa uchumi wa mwaka 2020/2021, nchi yetu ilikua kwa asilimia 4.9, lakini mpaka Juni, 2022, takwimu zinaonesha kwamba, unakua kwa asilimia 5.2, lakini ugumu wa uchumi huu ukuaji wake ukiangalia uchumi wa dunia utauona unasinyaa. Uchumi wa dunia una-*deteriorate* na wote tunajua sababu kubwa ya msingi hapa ni *Covid-19*, lakini pia kabla hatuja-*recover*, dunia haija-*recover* kutoka kwenye hii *pandemic effects* hizi, tukaja tukaingia hii vita ya Ukraine. Kwa hiyo, sasa imekuja imechanganya *economic destruction* hii vita ya Ukraine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imejionesha pia huko duniani ambako kuna *high inflation rate* ambayo imefikia mpaka *double digit*, lakini sisi tumeweza ku-*control* bado tuna *single digit* mpaka sasa hivi. Mpaka sasa hivi tuko kwenye *four point something*, lakini wenzetu duniani huko

9 NOVEMBA, 2022

labda tuchukulie mfano *European Union*, kwa nini nasema tunafanya vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *European Union*, *inflation rate* yake kuna nchi pale zimefikia mpaka asilimia 25.5 na nchi ya chini kabisa ambayo inafanya vizuri, Ufaransa, iko 6.2 *inflation* yake. *Data* zilizokuwa *revealed* na *Eurostat* zinasema kwamba, kwa wale *giants* kwa mfano, Netherlands wana 13.7 ya *inflation*, Greece wana 11.2, Belgium 10.5, Spain 10.5, Denmark 9.0, Cyprus 9.0, Sweden 9.5. Kwa hiyo, hawa wote hawa ndio ambao wanatuchangia na sisi pia katika miradi mbalimbali, lakini wana *high inflation rate*, sisi tumeweza ku-control, bado tuko kwenye chini ya tano. Sasa ni lazima tujipongeze katika hili, tusikate tamaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza sana Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake katika eneo hili, lakini sisi sio kisiwa, duniani *projections* zinaonesha kwamba, ukuaji wa uchumi utashuka kutoka kwenye 6.1 mpaka 3.2. Kwa hiyo, sisi sio kisiwa, ni *part* ya dunia. Kama ilivyojionesha huko kwa wenzetu ulaya, *European Union*, *inflation* ilivyokuwa juu sasa bado sisi tuendeleo kuhakikisha kwamba, Mpango wetu huu tujiwekeze sana katika kuhimili hali ya mtetereko wa uchumi duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie; Mpango huu tujielekeze sana kwenye uhimili wa hali ya mtetereko wa uchumi duniani kwa sababu, tunapoelekea tumeambiwa pia, takwimu zinatwambia kwamba, tutakapofika *half* ya pili ya bajeti hii hali ya uchumi itashuka, ukuaji wa uchumi hapa kwetu nchini. Sasa tuwe na mpango wa kuhakikisha sekta za uzalishaji, kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, biashara

9 NOVEMBA, 2022

zinakuwa na tunaziwezesha na kusimamia utekelezaji wake na masoko yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima tumalizie miradi yetu ya kimkakati, reli SGR tuimalizie, umeme vijijini tumalizie ili wananchi wetu waweze ku-add value mazao yao, lakini LNG, mradi ya gesi lazima tuhakikishe unajengwa na unakamilika, lakini miradi ya gesi ambayo ile ya kuzalisha umeme tuhakikishe kama ilivyopangwa katika bajeti hii nayo pia inakamilika, lakini Bwawa la Mwalimu Nyerere tulisimamie kwa karibu sana ili liweze kukamilika. Hii itasaidia uchumi wa jumla kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu hawa nimeonesha mfano wa data hapa, wa Eurostat data, inaonesha European Union nchi ambayo uchumi wake, high inflation rate yake iko chini Ufaransa, wao waliwekeza sana kwenye energy. Waliwekeza kwenye energy kupitia hii nuclear, sasa hivi wao wameshindwa kubabaika, hawajababaika kabisa na hili tatizo lililokuwepo la Russia kukata au kupunguza umeme na gesi katika Nchi za Ulaya ambalo limesababisha high inflation rate. Hii ni kwa sababu, wao walikazana na wakawekeza kule. Sasa sisi tukazane tukamilishe hii miradi mikubwa ya kimkakati ili uchumi wetu usibabaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, pia hali ya uchumi ya dunia inavyokwenda itatuathiri na sisi uchumi wetu katika nusu ya pili, naomba sana ili isituathiri sana tuwekeze kwenye kilimo. Leo kwenye kilimo Serikali iliwekeza bilioni 150 za ruzuku, lakini katika utekelezaji wake huu unasuasua practically kwa maana kwamba, Serikali imetuambia mpaka leo hii, leo asubuhi imetuambia itatufikishia mpaka kwenye makao makuu ya wilaya au tarafa,

9 NOVEMBA, 2022

hautasambazwa vijijini. Kilichonishangaza ni kusikia kwamba, halmashauri ndio zisambaze Serikali itazipa mafuta. Halmashauri hizi zinatoa wapi magari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mkulima kwangu tarafa ya mwisho iko kilometa 220, kata ya mwisho iko kilometa 254. Mkulima kuifuata mbolea huko iliko kilometa 254 inabidi asafiri kwa gharama ya 40,000/= kwenda na kurudi, alale hapo, anunue mbolea, asafirishe na mbolea aipeleke kule, gharama inazidi. Kwa hiyo, ushauri wangu, lazima Serikali watafakari upya au watuachie kule wilayani, Mwenyekiti wa Kamati ya Pembejeo Mkuu wa Wilaya asimamie, basi wawaachie wafanyabiashara wa maeneo yale wasafirishe kwa gharama ambayo atailipia mkulima isizidi hata 5,000/=. Nawaomba sana wafanyabiashara tuwaachie kuliko sisi leo tuwaambie halmashauri tutawapa mafuta, magari watatoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaachie wafanyabiashara waifanye kazi hii. Mkulima yuko tayari kuongeza hata shilingi 5,000 kwa ajili ya usafiri ili mbolea imfikie pale. Serikali tunafanya kazi nzuri sana, tumempunguzia nusu, mwaka jana tulikuwa tunanunua mbolea shilingi 130,000, leo tunanunua shilingi 60,000 mkulima sidhani kama atashindwa kulipia shilingi 5,000 kwa ajili ya usafiri. Naomba Serikali walitafakari sana na msimu ndio huu hapa, wakati umeshafika wa maandalizi ya kilimo, watu wanababaika wanasafiri, wanapambana, wanalala siku tatu, siku nne, kutafuta mbolea, mnyonge wa kawaida anayeishi Magazini au anayeishi Lingusanguse, anayeishi Msisima kuja kufuata mbolea Namtumbo, kilometa 284, hawezi, kwa hiyo, ni lazima tusaidie hili. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Vita Kawawa. Jambo la Nkansi na *arrangement* ya Nkansi ni maamuzi na ushauri uliotoka kwenye Halmashauri ya Nkansi. Haina maana kwamba, *modality* tunayoifanya Nkansi ni *uniform* kwa nchi nzima, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimesema kwamba, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wa Wilaya, maeneo ambayo wanashauri kufunguliwe vituo sisi kama Wizara tuko tayari ku-*facilitate* kwa sababu, tunatumia taasisi zetu mbili maeneo ambayo wafanyabiashara hawaoni faida ya kwenda. Sisi kama Serikali tunatumia *TFC* na Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa ajili ya kufikisha mbolea katika maeneo hayo, ili wakulima waweze kununua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *modal* ya tatu ambayo tunaifanya kama Wilaya ya Rorya, Halmashauri inakusanya mahitaji yote ya vijiji vyake halafu tunachagua kampuni inayopeleka katika eneo lile kutokana na orodha ya wakulima. Kwa hiyo, kila eneo lina jiografia yake, lina tabia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho. Hatuzuwii wakulima kuchangia gharama ya kusafirisha pale ambapo wao wenyewe wanaamua. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kawawa na muda wako umekwisha. (*Makofi*)

9 NOVEMBA, 2022

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kawawa, muda wako umekwisha.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, aah, daah.

MWENYEKITI: Wakati unapewa Taarifa na muda ulikuwa umeshakwisha.

Mheshimiwa Bonnah, jiandae Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bonnah. Mheshimiwa Zaytun ameomba kuchangia jioni, baada ya Mheshimiwa Bonnah, atakuwa ni Mheshimiwa Hawa.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa 2022/2023. Kabla ya hapo, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na niwaombe tu Watanzania wenzangu tuendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Rais anaanza kujiandaa kugombea miaka kumi au miaka mitano, lakini

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa wetu, Mheshimiwa Rais hajajiandaa na amekabidhiwa nchi na nchi inakwenda vizuri. Kwa hiyo, ni jambo zuri sana la kumtia moyo pamoja na kumpongeza, hakujiandaa, lakini ameweza kufanya mambo yote ambayo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kitendo ambacho kinaendelea kwenye jimbo langu, ambapo wanafanya tathmini, lakini naomba, ikumbukwe kwamba, hii tathmini inayofanyika hili zoezi limechukua muda mrefu sana tangu mwaka 1997. Kwa hiyo, naomba Wizara watakapomaliza kufanya tathmini, hawa watu walipwe. Naiomba Serikali kabisa iwalipe hawa watu isije ikawafanyia tathmini halafu ikawaacha tu hivyohivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kuchangia Mpango wa Maendeleo; ukurasa wa 78, Biashara na Uwekezaji. Tukiongelea Mkoa wa Dar-es-Salaam sehemu yoyote ambako tunahitaji Serikali uchumi ukue ni lazima kuwe na usalama. Mkoa wetu wa Dar-es-Salaam kwa muda mrefu umekuwa na matukio mbalimbali, hasa matukio ya *panya road* na kuna sehemu mikoa mingine inawezekana ikawa na mambo hayo, lakini sisi tuna hao *panya road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali katika mpango huu wa 2022/2023, kuwe na mpango maalum ambao utakuja kuwafanya wananchi ambao wanakaa Mkoa wa Dar-es-Salaam au na majiji mengine, mfano kama Mbeya, Arusha, Mwanza, waangalie watafanya mpango gani ili kuona kwamba, hawa vijana kwa sababu, vijana wengi ambao wanashiriki kwenye haya

9 NOVEMBA, 2022

mambo ya *panya road* au na wizi mwingine mbalimbali ni vijana wengi ambao hawana kazi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aje na mpango ambao unaweza kuwasaidia vijana wetu waweze kupata kazi waachane na haya mambo ya *panya road*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na Mkoa wa Dar-es-Salaam pia, hapo hapo. Mkoa wetu wa Dar-es-Salaam mwaka 2018 kwa sababu, sehemu yoyote ambayo tunahitaji uchumi ukue ni lazima tuwe na usalama. Mwaka 2018 kulikuwa kuna mchakato unaendelea kwamba, wanataka waanze sasa kuweka kamera za barabarani na wenzetu wa Zanzibar tayari wameshaweke. Hili jambo limeshapita siku nyingi, lakini leo ni 2022 hizi kamera hakuna, wala hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Dar Es Salaam kama kungekuwa na usalama wa kutosha ina maana wafanyabiashara wengi wangukuwa wanaweza kufanya biashara zao masaa 24 lakini sasa hivi ukiangalia Mkoa wa Dar es Salaam, mtu ambaye anafanya biashara yake ya M-Pesa biashara tu ya kawaida ni lazima Saa 12 awe amefunga kwa sababu usalama ni mdogo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iingize kwenye mpango huu wa maendeleo ni jinsi gani itakuja na mpango wa usalama katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia Mkoa wa Dar es Salaam ni Mkoa ambao ni lazima utofautishwe na Mikoa mingine, kwa sababu huwezi kusema inafanana na Mkoa wa Iringa au Mkoa wa Dodoma. Dar es Salaam ndiyo unaoongezea Serikali mapato. Kipato cha Taifa kwa asilimia

9 NOVEMBA, 2022

Themanini kinatoka Dar Es Salaam. Kwa hiyo ni lazima tunaposema Dar es Salaam ni Mkoa ambao kwanza una watu wengi na ndiyo Mkoa ambao umeongoza katika sensa kwa watu wengi. Ni Mkoa ambao una watu waliotoka sehemu mbalimbali, ukiachilia hilo ndiyo Mkoa ambao una *airport* kubwa ya Kimataifa, Bandari na Reli. Kwa hiyo, tunaomba katika mchakato huu wa maendeleo Mkoa wa Dar es Salaam utengenezewe *page* yake tofauti kutokana na unyeti wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es salaam ni Mkoa ambao una mambo mengi na una biashara kubwa na wafanyabiashara wengi. Sisi hatulimi, watu wetu wanategemea kufanyabiashara ndogo ndogo, biashara kubwa pamoja na wafanyakazi. Kwa hiyo, tunapouangalia Mkoa wa Dar es Salaam tuungalie kwa mambo tofauti tusije tukauweka uwe sawa na Mkoa kama wa Mkoa wa Singida au Mkoa wa Dodoma, ni Mkoa tofauti na naomba uwe na mambo yake tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 104, umeongelea ardhi na makazi. Mkoa wa Dar Es Salaam mvua zikinyesha...

MHE. SALIM MUSSA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. SALIM MUSSA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kwenye suala la usalama na *comfortability* ya

9 NOVEMBA, 2022

Wawekezaji ndani ya Jiji la Dar es Salaam. Pia suala la *fire* ni tatizo kubwa sana. Dar es Salaam wanayo magari matatu tu ambayo yana umri sawa na umri wangu zaidi ya miaka 30 hadi leo. Ipo haja Serikali kuweza kuweka mkakati madhubuti wa kuweza kuongeza magari ya *fire*.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante taarifa naipokea. Nilikuwa naongelea kuhusu suala la ardhi na makazi ukurasa 103 hadi 104. Mkoa wa Dar es Salaam tukienda kwenye masuala ya miundombinu labda na Mkoa wa Mbeya na Arusha. Dar es Salaam kutokana na geografia ya Mkoa wenyewe ulivyo na wingi wa watu, ukienda kwenye masuala ya makazi naomba Mheshimiwa Waziri aangalie ni jinsi gani watakuja na mkakati katika suala la miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe ni mkazi wa Dar es Salaam unajua kwamba hakuna Mwekezaji atakuja wakati wa masika Dar es Salaam, pale Mnazi mmoja pamejaa maji ndiyo anatoka *airport* mvua ambayo imenysha saa moja, aje aseme kwamba hii ni sehemu nzuri ambayo mtu anaweza kuwekeza haiwezekani! Kwa hiyo, ni sehemu ambayo mvua ikinyesha ni taabu na isiponyesha ni taabu. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri aangalie ni jinsi gani kutakuwa na mkakati wa kuiwezesha Dar Es Salaam iweze kupendeza, hata mvua ikinyesha isionekane imenysha na hata isiponyesha ionekane haijanyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linahusiana na suala la *DMDP*, mwaka jana hapa tulikaa tukaongea suala la *DMDP* ni jinsi gani Serikali inaenda kujenga Bonde la Mto Msimbazi, tukaambiwa kwamba huu mradi unaanza mwezi Machi, lakini mpaka leo huu mradi haujaanza na wala huo

9 NOVEMBA, 2022

mpango sijajua umefikia wapi, tumeongea hapa mara nyingi tu kuhusiana na masuala ya *DMDP*. Kwa hiyo, mimi nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba hili suala la *DMDP* na miundombinu ya Dar es Salaam asilifananishe na Mikoa mingine, kwa sababu hata hizi fedha zitakazokopwa kwa Dar es Salaam kurudishwa haitachukua muda kama Mikoa mingi ukizingatia Dar es Salaam wafanyabiashara ni wengi, pia watumiaji barabara ni wengi na magari mengi ambayo yanapita, kwa hiyo ni rahisi sana kurudisha hizi pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri amalize huo mchakato ambayo walikuwa nayo kwa ajili ya hiyo miradi ya *DMDP* ili Bonde la Mto Msimbazi liweze kujengwa, pia barabara za *DMDP* ambazo tulikuwa tumezipanga tangu mwaka jana kwamba sasa zinaenda kujengwa barabara za *DMDP* ziweze kujengwa, maana tangu tumeongea mpaka sasa hivi hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kamoli kengele hiyo ya pili. Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga jiandae Mheshimiwa Almas Maige.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mpango huu wa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wowote wa uchumi katika nchi yoyote unategemea mipango thabiti ambayo mmejiwekea kama Taifa. Siku za nyuma kidogo kulikuwa na

9 NOVEMBA, 2022

filamu ya *Royal Tour*. Tumeona ni kwa namna gani mafanikio makubwa ya filamu ya *Royal Tour* yanakuja katika nchi yetu, lakini kama Taifa tumejiandaa namna gani kukabiliana na wimbi la wageni ambalo litakuja katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango au katika mpango huu sijaona sehemu yoyote ikisisitiza kwamba kama Taifa tunategemea kuongeza mapato yetu kupitia utalii. Utalii kwa Tanzania unakua kwa kasi ya hali ya juu, lakini mpaka sasa kama Taifa tunategemea kupata mapato ya asilimia 17 tu kutoka katika suala zima la utalii. Tuna uwezekano mkubwa sana wa kuongeza mapato yetu kupitia sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vitu vingi sana, tuna vivutio vingi sana, tuna mambo mengi sana katika nchi hii ambayo tukiyatangaza tukiyaweka vizuri katika Taifa letu haki ya Mungu utalii utakuwa unaongoza kwa zaidi ya asilimia Thelathini katika mapato ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na hifadhi 16, leo tunapozungumza Tanzania tuna hifadhi 22. Hifadhi hizi 22 bado kama Taifa hatujaona umuhimu wa kutengeneza mpango madhubuti wa kuhakikisha hifadhi zote hizi angalau hata nusu ya hifadhi hizi zinaingiza kipato cha kutosha. Leo ninapozungumza na Bunge hili ni kwamba, bado watalii wanapokuja kwenye nchi yetu, wanatamani kwenda Serengeti na Zanzibar, lakini tunahifadhi na vivutio vingi kweli kweli ambavyo watalii hawa ama wananchi wa Tanzania ambao wanapenda kwenda kutalii wakitangaziwa nchi hii itakuwa inaongoza kwa mapato.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara haitakuwa na mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba inaongeza bajeti kwenye sekta hii ya utalii tutaendelea kupiga *mark time* na badada ya hii asilimia 17 tutashuka asilimia 15 mpaka asilimia 10 kwa sababu hatuko *serious* kwenye jambo hili la utalii. Shida yetu ni kwamba tunagusa kila kitu hatuangalii zile sekta muhimu ambazo zinaweza zikifufua uchumi wetu na uchumi ukapaa ukawa mkubwa kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo hifadhi ya TANAPA ambayo inasimamia hizi hifadhi 22, lakini bajeti waliyonayo tangu wanasimamia hifadhi 16 mpaka leo ni ileile Biloni 1.5 wanaendelea kuwa nayo mpaka leo. Hivi kutoka hifadhi 16 mpaka leo 22, bajeti ni ileile hivi kweli tuko *serious*, tunataka utalii wa nchi hii ukue? Ningeomba sana katika mpango huu ambao tunakwenda kwa ajili ya kuandaa bajeti, hebu watuletee bajeti ya maana katika Wizara hii ya Maliasili ili tuweze kukuza utalii wetu. Tunahitaji kuwa na asilimia za kutosha katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusiana na suala la Bandari Kavu. Mimi ninatokea Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Tabora ni eneo ambalo reli ya SGR inapita. Kama ulivyoona hata katika sensa Tabora ni moja kati ya Mikoa mikubwa sana na ina maeneo makubwa sana, mimi ningeomba Serikali iache kigugumizi wapeleke Bandari Kavu katika Mkoa wa Tabora. Watakapopeleka Bandari Kavu katika Mkoa wa Tabora sisi tutafanya biashara na nchi za Maziwa Makuu kwa urahisi zaidi. Ukitoka Tabora kwenda Katavi, Mpanda na Kigoma ni rahisi kuliko maeneo mengine yoyote na tutaweza kufanya biashara na nchi Mbili mpaka Tatu kwa pamoja, kuliko ambavyo sasa hivi

9 NOVEMBA, 2022

kumekuwa na kigugumizi tunataka huku tunataka huku. Serikali ifanye maamuzi katika Mpango mnaokuja nao, tengeni fedha ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga Bandari Kavu katika Mkoa wa Tabora na kama kuna nia thabiti ya kuinua Mikoa ya pembezoni basi fanyeni hili. *(Makofi)*

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti,taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumpa taarifa mchangiaji Mheshimiwa Hawa Mwaifunga Dada yangu kuwa Serikali ya Mkoa wa Tabora chini ya Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Batilda Burian umeshatenga eneo kwa ajili ya kujenga Bandari Kavu hii ambapo Serikali ikiwa tayari basi watapatiwa eneo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kwa taarifa yake maana kutenga ni jambo moja lakini utekelezaji ni jambo lingine. Kwa hiyo, hapa tunachofanya ni kuhakikisha kwamba tunasisitiza kwa sababu tayari kumeshakuwa na mvutano, Mkoa wa Tabora tayari umeshatoa heka zaidi ya 1,000 bila fidia yoyote. Kwa hiyo, mimi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri tusaidieni hii Mikoa ya pembezoni inahitaji kuendelea, ili tuweze kuendelea na wananchi wetu waweze kuwa na mafanikio

9 NOVEMBA, 2022

katika uchumi wao tunaomba sana mtusaidie, hii Bandari kavu itakapokuja pale Tabora itasaidia sana wananchi wetu pia itasaidia kukuza uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie upande wa Kilimo, ni ukweli usiopingika kwamba Mkoa mingi inalima mazao ya biashara lakini sisi ambao tunatoka Mkoa wa Tabora zao kubwa la biashara ambalo tulikuwa tunalitegemea wakati wote ni zao la Tumbaku. Tabora ni Mkoa ambao umeonekana kwamba unao uwezo wa kulima mazao mengi ya biashara na yakastawi vizuri. Tabora tunalima alizeti, korosho, tumbaku, mahindi, maharagwe na kadhalika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kazi kubwa ambayo anaifanya nasi tunamuahidi kumpa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha kwamba nchi yetu tunakwenda kuingia kwenye kilimo cha kisasa badala ya kutegemea zaidi mvua na jembe la mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono suala zima la *block farming*, lakini ninaiomba Serikali iliangalie hili jambo kwa jicho la tatu, iwe ni lazima kwenye kila Mkoa na Wilaya kutengwe maeneo kwa ajili ya hizi *block farming* ili wananchi wetu waweze kunufaika na kilimo kwenye suala zima la *block farming*. Kama Tabora tunao uwezo wa kulima korosho, lakini wanapotokea wateule wakasema kwamba hatuwezi kulima korosho kwa sababu yataharibu zao la asali. Mimi nimezaliwa Tabora nimekua Tabora, lakini sijawahi kuona tajiri wa asali zaidi ya watu wanaovuna asali hela wanayopata ni kwa ajili ya watoto kusoma, chakula na mambo mengine madogo madogo.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kwenda mbali zaidi ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu wawe na tija. Kwa mfano, likija zao la korosho baada ya miaka mitano au kumi watu wakaanza kuvuna korosho, Mkoa ule utabadilika na mwisho wa siku watu wetu wakawa matajiri na kufanya kazi kubwa. Kwa hiyo, ninaomba sana kupitia mipango hii kwenye suala zima la kilimo tusaidiane kuhakikisha kwamba angalau hawa wateule, kila mteule ajue kwamba katika Mikoa hii tuweke hizi *block farming* na katika Wilaya hizi ambazo tunaweza kuweka basi iweze kufanyika hivyo, ikiwepo Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nizungumzie suala zima la afya. Wakati nikipitia mpango nimeona kwamba wanazungumzia suala zima la kupunguza vifo vya watoto na mama wajawazito, lakini hizi takwimu zinasema sahihi? Je, hizi takwimu si ni zile ambazo zinakuwa *recorded* vipi kuhusu zile takwimu ambazo haziko *recorded*? Wanawake wengi sana wanajifungulia nyumbani na barabarani. Je, hawa nao takwimu zao tayari zinakuwa zimeshaorodheshwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza kwamba vifo viumepungua kwa asilimia hizi lazima tuwe na uhakika wa kuona hata kwenye yale maeneo ambayo wanawake wengi wanajifungulia majumbani na barabarani taarifa zake zinakuwa *recorded* na zinapelekwa na zinakuwa taarifa sahihi ili tuweze kujiridhisha na kuona kwamba ni ukweli kama Taifa tumepunguza vifo vya mama na mtoto, kuliko hivi sasa tunazungumza vitu kinadharia na vitu vile ambavyo tunaviona viko pale lakini kiuhalisia siyo sahihi. Kwa sababu sisi tunaotoka kwenye maeneo ya vijijini

9 NOVEMBA, 2022

ambayo ni mbali na hospitali tumeshakutana na kadhia hizo nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta Mama ameshajifungua, wameshamfanyia kila kitu pale kamaliza biashara, lakini saa zingine unaweza kuta mtoto amepata athari au amekufa ama mama amekufa taarifa hizo hazitoki. Kwa hiyo, mimi niombe sana kama Wizara katika mpango wenu muangalie na muone namna gani ambavyo mnaweza kujua kwamba wanawake wangapi kwa mwaka wanakufa katika nchi hii kwa ajili ya uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilishamtaja Mheshimiwa Almas Maige, ajiandae Mheshimiwa Justin Nyamoga, ajiandae Mheshimiwa Eng. Mwanaisha, ajiandae Mheshimiwa Deo Mwanyika.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mpango wa Maendeleo lakini pia Mpango wa Bajeti 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye miradi ambayo ninafikiri ni ya kimkakati na nianze na Reli ya Kati - SGR. Reli hii inakusudiwa kuunganisha Tanzania na nchi jirani, ibebe mizigo ya nchi jirani ili tupate uchumi kwa nchi yetu lakini lazima reli hii ikamilike. Mimi nimeona mpango unavyoendelea kwamba Reli hii ya Kati itajengwa na tayari sehemu ya kwanza ile ya Dar es Salaam - Morogoro imekamilika na Morogoro - Makutupora iko asilimia Fulani

9 NOVEMBA, 2022

lakini ninaomba Serikali iweke nia sana. Hatuwezi kuwa na mpango wa ujenzi wa reli ambayo hatujui itakamilika lini. Tungependa kujiwekea mpango kwamba reli hii itaisha lini ili ilete faida nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ningependa kuongelea ni ukamilishaji na ununuzi wa ndege Tano, ni wazo zuri sana kuongezea uwezo ATCL na hasa ile ndege ya mizigo ambayo itabeba mizigo yetu kupeleka nje ya nchi moja kwa moja. Sasa hivi tunapata taabu ya kupeleka mizigo yetu kupitia nchi za Jirani, ni wazo zuri lakini Serikali isimame na tuipongeze iweze kukamilisha mradi huu wa ATCL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa kufua umeme kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere kule Rufiji, napata kidogo matatizo, kila siku ng'ombe wanakamatwa kwenye vyanzo vya maji na ule mradi unatumia maji, maji yasipopatikana ya kutosha kujaza Bwawa lile kule kwa sababu yoyote ile, mradi ule utakuwa '*White Elephant*'. Yapo Mabwawa ya namna hiyo yalijengwa katika nchi zetu za Afrika mfano kule Ghana na lile Bwawa halina maji mpaka leo. Mimi sitaki kuona uchungu wa tunavyojibana kuitafuta hela ya kujengea Bwawa hilo halafu watu wanakwenda kwenye vyanzo vya maji yanayokwenda Rufiji wanaharibu! Iko haja ya Serikali kujikita kindakindaki kuzuia kabisa uharibifu wa vyanzo vya maji yanayokwenda Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa REA, mradi huu utafanya kazi vizuri sana kama Bwawa wa Mwalimu Nyerere litazalisha umeme wa kutosha lasivyo vijini umeme hautatosha. Tulionao sasa hivi hautoshi kuendesha vijiji

9 NOVEMBA, 2022

vyote Tanzania nzima. Chanzo cha Mwalimu Nyerere ni muhimu sana kutunzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwambie tu Waheshimiwa Wabunge, umeme vijijini huleta maendeleo makubwa sana. Badala ya watu kulala mapema na kuogopa giza, sasa kuna vituo wanaangalia *centers* nyingi za *television*, vile vile umeme wanachomeleaji *grill* wanazalisha kutokana na umemea ambao umewekwa vijijini. Kwa hiyo mradi huu ambao unaanza kusuasua tena, sehemu yangu katika vijiji vingi Wakandarasi wamedolora. Iko haja ya kuwasimamia ili ahadi ya Serikali kama ilivyo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba vijiji vyote vitapata umeme mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia pia mpango huu unaelezea ujenzi wa barabara na madaraja makubwa ambayo yataleta mhemuko wa kukua kwa uchumi kwa kusafirisha mizigo na watu. Madaraja mengine yanaunga nchi jirani na kadhalika. Kwa hiyo Serikali ikazane kumalizia madaraja na meli ambazo zinajengwa sasa hivi kwenye maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo, kila mtu anajua kwamba kulima kama biashara au kulima kama shughuli unagusa asilimia 67, kwa sababu kila mtu hapa anakula, na tunamalizia mkutano hapa tukale, kwa hiyo kilimo ni jambo muhimu sana. Serikali katika mpango wake huu imekuja na wazo zuri sana la kutoa ruzuku kwa ajili ya wakulima wote na kusajili wakulima wako wangapi; na sasa tumeshapata wakulima 2,118,911 mwanzo. Hata hivyo mbolea ya ruzuku imeshaagizwa ya kutosha na inagawiwa.

9 NOVEMBA, 2022

Jambo hili litakuza uchumi na litakuza tija ya mazao shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo kadhaa ambayo mengine yameelezwa katika mpango huu hasa maji. Maji ni kikwazo kikubwa sana cha maisha vijijini. Hata hivyo mpango unaelekezea kukuza mpango wa maji mpaka asilimia 74.5, vile vile asilimia 86.5 mijini. Jambo hili si dogo ni jambo kubwa sana. Tunaishukuru pia Serikali imejiandaa kununua mitambo kwa ajili ya kuchimba malambo, Mabwawa na vile vile kuchimba visima. Jambo hili linastahili pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, mpango unaelezea kuendelea kupata elimu msingi bure, vile vile pamoja na elimu msingi hii tumejenga madarasa, tumejaribu kujenga maabara katika sekondari zetu. Kwa hiyo mpango uko vizuri kwa njia hiyo na elimu ndio ufunguo wa Maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchumi wa bluu yako mambo mengi ambayo yameelezwa kwenye uchumi wa bluu. Hapa Tanzania bara kulikuwa na shirika kubwa sana linaitwa *TAFICO*, lilikuwa shirika ambalo linajiendesha vizuri na ambalo lilikuwa ndilo chanzo cha mlango wa boiashara ya uchumi wa bluu. *TAFICO* ikauzwa, baadaye ikarudhishwa sasa hivi inajikongoja, hamna chchote. Naomba Serikali katika mpango wake isisahau uchumi wa bluu ili tuweze kuvua samaki. Pia tutumie mpango huo kwa ajili ya kupata fedha na kupata maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi huko Lindi. Hivi karibuni tulipata meli

9 NOVEMBA, 2022

kubwa ya kwetu, kibiashara tumeipeperusha bendera ya Tanzania. Ile meli haiwezi kuteremsha Samaki hapa Tanzania, na tulikuwa na mgao wa Samaki karibia tani 300, sasa inaenda kuteremsha Samaki *seashells* zitiwe kwenye kontena ndio zije hapa Dar es salaam. Jambo hili linawashangaza hata tuliowapa hiyo meli, kwamba hatuna pakuteremshia Samaki wala hatuna bandari. Kwa hiyo katika mpango huo wa maendeleo nimeona tuna mpango wa kuendeleza ile Bandari ya Uvuvi Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulikuwa na mpango wa kununua meli nane; lakini siuni ule mpango na kulikuwa na meli moja kwa ajili ya *TAFICO*, meli nne ilitakiwa ziende Zanzibar na meli nne zibaki Tanzania Bara kwa ajili ya kukuza uchumi wa bluu, lakini sizioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la mradi wa gesi asilia. Mimi sitaki mambo ya kujifikirisha Mwenyewe kwamba tutapata. Tunataka kujenga *LNG* pale Lindi, mimi nilikwenda kutembelea mradi wa *LNG* ughaibuni kule, na jana tulikuwa na wenzetu wa Mozambique hapa tukawauliza wenzetu vipi *LNG*? Majibu niliyoyapata kule nje yalikuwa ni kwamba wananchi hawanufaiki na *LNG*. Kama ambavyo watu walivyochimba malori na malori ya dhahabu hapa hatukupata hata senti tano mpaka tulipobadilisha sheria. Naogopa Mradi wa *LNG* huu, kama hatutakuwa na sheria ambazo zitatulinda, watu watachimba gesi na kuzipeleka nje. Kama vilivyo vitalu vya gesi huko *high seas* hatufaidiki sisi. Naogopa sana kuutia mpango wa *LNG* kwenye mpango wa Serikali bila kuwa na uhakika kwamba utatuingizia hela au la.

9 NOVEMBA, 2022

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya mwisho hiyo naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Nyamoga, jiandae Mheshimiwa *Engeneer* Mwanaisha, jiandae Mheshimiwa Mwanyika.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafsi ili na mimi niweze kuchangia mapendekezo ya mpango. Nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwenye majimbo yetu ikiwemo jimbo la Kilolo. Pia niishukuru Serikali kwa wasilisho la mpango ambao mmeuwasilisha. Huu ni wakati wetu ili sisi tuweze kutoa maoni na mapendekezo ambayo yatasaidia katika kuboresha mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianze kwa kuzungumzia mashirika ya umma na namna ambavyo yanafanya kazi zake na jinsi ambavyo tunaweza tuyakaboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina zaidi ya mashirika ya umma 200, sina idadi yake kamili, lakini sina hakika kama mashirika haya yote yana ufanisi na tija ambazo tunazihitaji. Ninaona kwamba kuna haja huu mpango wa Serikali ukaja na tathimini ya mashirika ya umma ili kujua kama yote yanahitajika na kama kweli yote hayafanyi vitu vinavyojirudia.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano; nimesoma kwenye taarifa nikaona kuna mashirika mawili na nikaangalia kazi yalizozifanya kwa mwaka uliopita. Shirika la kwanza linaitwa CAMARTEC. Kwenye taarifa yake wametaja vitu walivyovifanya mwaka jana. Kwanza, wametengeneza tella moja, IKINI sijajua ni tella la nini? Pili, wametengeneza mashine mbili za kubangua korosho, kingine walichotengeneza ni mikokoteni 10 ya kuvutwa na Wanyama, pia wametengeneza mashine nne za kupura mtama. Naomba niishie hapo, na kuna vingine pia wamefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mawazo yangu nafikiria, hivi vitu ndivyo vinavyoweza kufanywa na SIDO na Mashirika mengine. Sijajua kama hii ni taasisi ya ubunifu au ni taasisi ya uzalishaji? Kama ingekuwa ni ya ubunifu mashine moja ya kupura mtama ingetosha ku-*display* ili wengine nao watengeneze. Pia kama ni ya uzalishaji kwa nini wazalishe nne? Kwa hiyo kwa kifupi ni kwamba zipo baadhi ya taasisi hazihitajiki au kama zinahitajika kuna namna ya kujirudia katika utekelezaji wake. Kwa hiyo ni muhimu kufanyia tathimini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaenda kwenye shirika lingine la umma linaitwa TEMDO, nikasoma. Kitu kilichofanyika ni kukamilisha kwa majokofu mawili ya kuhifadhia maiti. Sasa haisemwi baada ya hayo majokofu mawili tunafanyaje labda ni kwa ajili ya kuwaonesha wengine ili watengeneze mengi au hayo hayo ndiyo wameyauza au ni kitu gani kimefanyika? Sasa tukienda hivi maana yake ni kwamba tuna *allocate* fedha kwenye makampuni ambayo tija yake ni ndogo halafu hatu-

9 NOVEMBA, 2022

allocate fedha kwenye sehemu ambazo tija ni kubwa na matokeo yake ni kwamba kuna upotevu wa rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kule kuna taasisi hizo zina wafanyakazi, zina namna nyingi, tathimini ingeweza kusaidia kuona umuhimu wa kuendelea kuwepo au kutokuwepo. Hivyo basi mimi nafikiri ni muhimu sana hilo tukaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumza hivyo, kuna shirika hili la Kibaha, hiki kiwanda cha viudadu ambacho tumekuwa tukikizungumzia hapa kila wakati, kimekwishatumia shilingi bilioni 83 na bado hakifanyi kazi. Sasa kama tungekuwa tayari tumesha-*restructure* hizi kampuni zikawa chche maana yake tungeweza kuwa na rasilimali nyingi kuwekeza kwenye hii ya viudadu ambayo sote tunajua kwamba ingeweza kuokoa fedha nyingi kutokana na uwekezaji ambao tungeweza kuufanya kwenye dawa za kuulia wadudu. Hata changamoto ya Malaria ingeweza kupungua na zile fedha ambazo tunatumia kwenye mambo ya malaria zingeweza kuokolewa. Kwa hiyo ningependekeza kwamba, hizi kampuni zaidi ya 200, Serikali kwenye mpango wake iyafanyie tathimini ione kama zote zina tija. Kama kuna ambazo hazina tija ziondolewe ili tusiendeleo kuwekeza kwenye sehemu ambayo hakuna tija yoyote katika kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifano miwili inaweza ikatoa picha halisi ya mengine mengi ambayo unaweza ukakuta kile kinachofanyika hakiwezi kuwa na tija. Huwezi ukawa na tija ya tella moja, huwezi ukawa na tija ya mkokoteni ambao hata watu wengine huko

9 NOVEMBA, 2022

wanatengeneza. Hatuhitaji kampuni ya kiserikali kuanza kutengeneza mikokoteni ya kuvutwa na ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niizungumzie pia benki ya kilimo (TADB). Kwanza niipongeze Serikali imewekeza shilingi bilioni 60 ni jambo zuri. Pia mtaji wake sasa umekwishafikia shilingi bilioni 268, ni hatua kubwa. Hata hivyo hii benki ni *invisible*, haionekani. Hata hapa Dodoma nikiwauliza Waheshimiwa Wabunge hii benki iko wapi hata hapa Dodoma Makao Makuu Hawajui. Mimi nilifanya kazi ya kuitafuta, iko nane nane ndani kwenye *fence*. Sasa benki zote ziko hapa mjini, hii iko nane nane tena kwenye *fence* na wakati huo wakulima wako vijijini. Tufanye tathimini ya hii benki ili kila mkulima aweze kuelewa vizuri hii benki na aweze kuelewa namna anavyoweza kui-access ili wakati tunapokuwa tunafanya *block farming* ziweze kuunganishwa na hii benki ili uwekezaji huo uweze kuwa na tija. Nani atajua kuna benki ya kilimo iko pale nane nane ilhali hata kibao hakipo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwenye mikoa yetu tunayotoka, wengi wetu hapa tumesema, mimi lringa sijaiona, wala Kilolo sijawahi kuiona na kama Mimi Mbunge mwenyewe sijawahi kuiona na hata wakulima wenyewe pia hawajawahi kuiona na hawaelewi. Kwa hiyo, kwa sababu ndiyo benki pekee inayowekeza kwenye kilimo, ukisema benki sio mfuko. Mfuko unaweza ukawa na ofisi mahali lakini benki sisi Watanzania tunaelewa benki utaiona popote pale. Sasa benki gani haionekani? Hii ni changamoto, ipo ina mtaji basi sasa ionekane ili wananchi waweze kufanya uwekezaji. Hilo litakuwa ni jambo la muhimu sana kwa sababu linaweza kusaidia katika kuboresha kilimo katika maeneo yetu.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie jambo la mwisho katika mchango wangu ambalo linahusu mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwanza nipongeze kwa hatua iliyofikiwa. Na mimi ninahakika kwamba mradi huu utafanya kazi vizuri tu. Lakini, ili mradi ule uweze kufanya kazi, *raw material* yake ni maji na haya maji yanatoka kwenye vyanzo na Kilolo ni mojawapo ya vyanzo. Sasa kama wewe unajenga Bwawa lakini huwekezi kwenye kulinda vyanzo vya maji au kuwa na miradi itakayovifanya vyanzo hivyo vya maji viendeleo kuwa endelevu maana yake ni kwamba *raw material* rasilimali ya ule mradi haipo. Sisi tunajua sasa hivi kwa mfano kilimo cha miti kinatakiwa kiwe na tija, sasa kama hakutawekwa ruzuku kwenye kilimo cha miti ili wakulima wa miti kwenye milima ya udzungwa waendeleo kulima miti, mti mmoja uuzwe shilingi 2000 wataikata, watalima mazao mengine na hayo maji hayatakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati huu tunapozungumzia mabadiliko ya tabia ya nchi ni ushauri wangu kwa Serikali, maeneo yote yenye vyanzo vya maji yanayolisha Bwawa la Mtera, Bwawa la Mwalimu Nyerere, Bwawa la Kidatu na Mahali mengine ikiwemo maeneo kama Kilolo, Makete na maeneo mengine yafanyiwe tathimini ya kupewa ruzuku kwenye kilimo cha miti kitakacholinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha, ajiandae Mheshimiwa Mwanyika.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia. Pia

9 NOVEMBA, 2022

nimshukuru Mwenyezi Mungu nwingi wa rehema mwenye enzi na utukufu. Nami naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita kwa mara ya kwanza nilipochangia hapa Bungeni nilinukuu usemi wa Rais wa 35 wa Marekani John Kennedy, aliposema kwamba “uchumi wa Marekani ni mzuri kwa sababu ya miundombinu yake na wala si miundombinu ya marekani ni mizuri kwa sababu ya uchumi wake”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inaamini hivyo pia kwa sababu imetengeneza miradi mingi ikaipa majina ya miradi inayochochea uchumi shirikishi na uchumi shindanishi na imetengeneza miradi ya vielelezo. Kwa hiyo Serikali yetu pia inaamini katika hilo. Hata hivyo tatizo kubwa nililoliona ni kwamba utekelezaji wa miradi ni lazima uhakikishe pia hauongezi Deni la Taifa iwe ni Deni la ndani au Deni la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani? Jambo hili linawezekana kutekeleza miradi bila kuongeza Deni la Taifa, hili linawezekana. Ila, pale tu ambapo hatuna budi ya Kwenda kukopa basi tukope mikopo ambayo ina masharti nafuu. Ambapo kama tunaipata *IMF* na *World bank* mikopo yote ile ina masharti nafuu na ndiyo tunaitumia kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nililoliona ni kwamba, tunahama sasa kutekeleza miradi yetu kwa kutokuongeza Deni la Taifa kwa kiwango kikubwa, tunakwenda kutaka kutekeleza miradi huku tukiliongeza Deni la Taifa kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano; umetanganzwa mradi wa ujenzi wa Barabara ya Kibaha – Mlandizi – Chalinze - Morogoro kwamba utajengwa *under*

9 NOVEMBA, 2022

EPC+ Finance; kwa maana ya kwamba Mkandarasi anafanya usanifu, anafanya ujenzi na analeta mleta fedha ambaye ndiye huyo *Financia*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Waheshimiwa Wabunge wameonesha kweli tunahitaji kujenga miundombinu yetu bila kuongeza Deni kubwa la Taifa letu. Mheshimiwa Shabiby jana alisema ni vizuri tukijenga miradi yetu kwa kutumia *PPP*. Kamati imeeleza vizuri kwamba *PPP* ina changamoto ya sheria yake kwamba masharti ni magumu na mtaji uliowekwa ni kiwango kikubwa. Nafikiri sasa ni wakati sahihi Serikali ikafanya haraka kuirekebisha Sheria ya *PPP* ili tuweze kutekeleza miradi bila kuongeza Deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *PPP* Mbia anajenga halafu ana-*operate* kwa faida baadaye anaturudishia Serikalini wakati huo huo hakuna *interest* ambayo sisi tumeichukua kutoka kwake. Kwa hiyo *PPP* ni njia sahihi nani nzuri kwa ajili ya kutekeleza miradi yetu bila kuongeza Deni la Taifa na *EPC+Finance* tunahitaji tui-*study* vizuri sana kabla ya kuingia kwenye njia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyingine ambayo kama Taifa itatusaidia sana kufanya miradi yetu bila kuongeza Deni la Taifa ni kwa kutumia *infrastructure bond*; na tumekuwa tukilisema hili mara kadhaa. Kwenye *infrastructure bond* tunachochea uchumi shirikishi. Wananchi wenyewe wa Tanzania wanashiriki katika kutekeleza miradi yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenye uzoefu na *treasury bills* wanaweza kusema hapa. Watanzania wapo wengi wenye fedha ambao wanaweza wakatoa milioni kadhaa

9 NOVEMBA, 2022

wakaweka kwa muda wa miaka mitano, kumi au kumi na tano; na sisi kupitia *fuel levy* ambayo tunapata bilioni 900 kila mwaka, tunaweza kutenga bilioni 300 kila mwaka kwa ajili ya kurudisha hizi *bonds* za watu. Kwa nini tusitumie njia hii ambayo itatusaidia Watanzania wenyewe kuweza kujiletea maendeleo wakati huo huo deni la taifa halikui? Hata hivyo tumeitangaza barabara ile kwamba tutaijenga *under EPC+Finance*; je, kiuhalisia tunakopesheka sasa hivi?

Mimi ninavyoona, ni kama tumeshamaliza *quarter* yetu yote. Sasa huyu *financier* anayekuja, tunaendaje kuchukua pesa kutoka kwake wakati tumemaliza *quarter* yetu yote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile huyu *financier* siyo yale mashirika makubwa ya dunia kama vile *African Development Bank*, *IMF* na *World Bank*, tuna uhakika gani na riba yake kama haitakuwa kubwa kuliko ya *World Bank* na *IMF*? Kwa sababu tumekuwa tukitekeleza miradi ya *design and build* kwa kutumia mtindo wa kwamba tuna *design* tuna-*build* halafu tunaomba mkopo *World Bank* au *IMF* au *African Development Bank*, halafu tunaulipa kwa riba ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunarudi kwenye *EPC plus finance* ambako vile vile Mkandarasi anabuni na kujenga, lakini anakuja na *financier*. Je, huyu *financier* riba yake itakuwa ndogo kama ya *World Bank*? Itakuwa ndogo kama ya *African Development Bank*? Itakuwa ndogo kama ya *IMF*? Kwa hiyo, mimi na-*discourage EPC plus finance*, we *better* tukaamua kukaa chini na kuiangalia vizuri *infrastructure bond*. Wenzetu wameweza kufanya haya, kwa nini sisi Tanzania tunaogopa kuingia kwenye *infrastructure bond*?

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ghana wanatekeleza miradi yao kwa kutumia *infrastructure bond*, Kenya imetengeneza sheria ya kufanya hivyo kwa kutumia *infrastructure bond*, sisi tunaogopa nini? Tunahitaji uchumi shirikishi na *infrastructure bond* inamwezesha Mtanzania kuweza kujenga barabara zake na yeye kuchangia maendeleo yake. Inakuwaje tuna-*hesitate* kuingia katika njia hii? Shida iko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yetu ilivyo sasa hivi, mwenye mamlaka ya kukopa ni Wizara ya Fedha peke yake. Wenzetu *South Africa* wanatekeleza *EPC+Finance* lakini wameipa *Road Authority* mamlaka ya kukopa. Maana yake ni kwamba inapotokea hali kama hii ya sasa kwamba *quarter* yetu tumeimaliza, *Road Authority* ana mamlaka ya kukopa; lakini sisi sasa hivi hatuwezi kutekeleza *under EPC+Finance*. Kwa nini tusitumie *infrastructure bond* kutengeneza uchumi shirikishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika nchi zote za *SADC*, ni Tanzania peke yake ndiyo haina *toll road so far*. Ni dhana tu ambayo imejengeka kwamba *toll road* ni mpaka zijengwe na hela za mbia labda *IPP* ndiyo tutengeneze *toll roads*, siyo kweli. Nchi kama Zambia hata madaraja yao ikiwa na *span* zaidi ya 100 tu inakuwa ni *toll*, watu wanalipia. Unaona! Kwa hiyo, pale pale tunakuwa tuna-*generate* mapato ya ndani kuweza kuendeleza miundombinu yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi huko nyuma miaka ya 1990, nimejaribu kutafuta na kupitia, tuliwahi kuwa na *toll gates* Ubungo, Chalinze, Makambako na Segera. Magari yalikuwa yanasimama na yanalipia, lakini sasa hivi

9 NOVEMBA, 2022

tumetengeneza *mentality* ya kwamba mpaka tujenge *under PPP* ndiyo tunaweza tukaweka *toll roads*, siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia Zambia, ukisoma *Road Authority* yake kwenye *annual report* inaonesha wazi kwamba wana-*operate* na *both*. Wanafanya *toll roads* na vilevile wanatumia *fuel levy*. Kwa nini sisi tushindwe kwenda kama nchi za wenzetu za jirani? Nimemaliza hapo na-*insist* tujenge kwa kutumia *infrastructure bond* ili tuweze kuwa na uchumi shirikishi na vilevile tuweze kupunguza deni la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusiana na TAA. Kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa kwa kuanzisha TAA, imepewa jukumu la kuendeleza miundombinu na vilevile kwa maelezo ya ICAO (*International Civil Aviation Organization*) inataka kila Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iwe na chanzo cha mapato; na sisi tumeweka *Passenger Service Charge* ambayo tunapata Shilingi bilioni 65 kila mwaka ili iweze kuendeleza viwanja vya ndege, lakini hii Shilingi bilioni 65 yote inachukuliwa na TRA na mamlaka iliyozalisha haipati hata Shilingi moja; je, tutaendelezaje viwanja hivyo vya ndege?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya kazi nzuri, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kupitia *Royal Tour*, lakini *so far* viwanja vya ndege vina hali duni. Tuwarudishie TAA pesa yao ili waweze kuboresha viwanja vya ndege kwa mujibu wa vikao.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

9 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante, mengine andika.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanyika.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika mapendekezo ya mpango wa 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima nzima ni uchumi shirikishi na shindani. Nami nilikuwa namsikiliza jirani yangu hapa Mheshimiwa *Engineer Magessa* aki-analyze data za kuonesha namna gani uchumi wa nchi yetu unaonekana kwamba kukua kwake ni kwa asilimia 0.1 na amelinganisha sana na nchi nyingine. Nami nakubaliana naye kabisa, lakini mimi naona kabisa sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza inatakiwa tu *interogate statistics* zetu kama zinasema ukweli na ziko halisia kwa sababu kwa kuangalia tu wenzetu walikotoka na walikokwenda, inaonesha kabisa kwamba sisi tuna tatizo. Pia kuna tatizo zaidi katika uchumi wetu, kwa maana ya kwamba bado *productive sectors* hatujaweza ku-*implement* kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwa mifano katika moja ya mapendekezo yangu na nitachangia zaidi kwenye sekta ya kilimo ambayo naielewa zaidi kwa sasa. Tukianza na zao la chai kwa mfano, sisi kama Tanzania bado tupo chini sana kwenye uzalishaji wa chai, na kwa

9 NOVEMBA, 2022

kweli chai inaweza ikatupa faida na ajira kubwa. Zao la chai hata kama hupati kodi kubwa sana, lakini ni zao ambalo linaongeza sana ajira kwa wananchi wetu wa kawaida, na kwa hiyo, linaongeza sana *multiplier effect* kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe tunaendeleza kwa kiasi kikubwa zao la chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea sasa, pamoja na mipango mizuri ya Wizara ya Kilimo, tunatakiwa tujue tunashindana kwenye zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya tayari wanazalisha karibu tani 570,000. Sisi bado tupo kwenye tani 30,000, lakini tuna wakulima wa chai ambao wanalima chai katika mazigira magumu. Naongelea wakulima wa chai wa Njombe, Tarafa ya Egweminyu kuna wakulima karibu 2,189, hao ni wakulima wa kawaida kabisa, *smallholder farmers*, siyo watu wakubwa. Hawa uzalishaji wao wa chai ni kilogramu milioni 3.6, lakini katika miaka mitano watakwenda kuzalisha kilogramu milioni 7.2, lakini ili waweze kufanya hilo wanahitaji kuwa na miundombinu wezeshi, sasa mpango wetu unaongelea vizuri sana kwamba kutakuwa na miundombinu wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalisia ni kwamba wakulima hawa ukiangalia bajeti yao ya barabara za vijijini inaangaliwa kama bajeti ya *TARURA*. Ukienda kwenye *TARURA* wanapogawa bajeti wanasema, tutatoa Shilingi bilioni moja kwa kila Jimbo. Ukweli ni kwamba hatufanyi kazi kimkakati, tunataka wakulima hawa wafike kwenye huo uzalishaji wa chai, lakini ikifika kwenye barabara, hatuwapi fedha za kuwasaidia.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa barabara wa Njombe nzima ni kama kilometa kama 890. Katika 890, hizi za wakulima wa chai hazihesabiwi. Peke yao, mtandao wao mzima wa chai hawa watu 2,100 ni kama kilometa 400. Kilometa 400 hizi hazina huduma, hazina msaada, hivi tutawezaje kuzalisha chai? Tunawezaje kusema kwamba tunaweza tuka-*compete* na Kenya, tunawezaje kuwawezesha watu wetu wakawa washindani kwenye ukulima wa chai? Kwa hiyo, hatufanyi mambo kimkakati ingawa tuna nia nzuri ya kufanya haya mambo kimkakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye zao la *parachichi (avocado)*. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, amekwenda China akaweza kufungua Soko la China kwa maana ya kuanzisha. Hii imetengeneza matumaini makubwa sana kwa Watanzania na wakulima wa *avocado*. Hata hivyo bado kazi ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema, tunapoongelea kilimo shindanishi na uchumi shindanishi katika mazao haya ya kupeleka nje, hapa ndipo ambapo kwa kweli Serikali na mapendekezo ya bajeti lazima yaangalie kwa umakini sana ni namna gani matumaini ya Watanzania ambao wanalima *avocado* kwa kiasi kikubwa sana wamechangamkia zao hili, wataweza kufanikisha ndoto zao kwa kuhakikisha kwamba wanapeleka kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungua soko ni jambo moja, lakini kuna mambo mengine mawili. Kwanza ni ubora, na pili, ni gharama. Kwenye gharama ndiyo hapo pa kuja kwenye mpango. Kwenye gharama za *export* na hasa

9 NOVEMBA, 2022

mazao ya *horticulture* Bandari yetu ya Dar es Salaam ndiyo moyo wa *export* na ndiyo moyo wa uchumi shindanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia na tukilinganisha, kwenye zai la *avocado* unachogombania ni bei nzuri, lakini unachogombania, uwe na zao zuri. Moja ya kitu ambachoni ni cha muhimu sana kukiangalia tunaita *shelf life*. Kwa kweli watu wa *THA* wanatakiwa watusaidie sana kuongeza *shelf life* ya *avocado* yetu Tanzania. Tukilinganisha na Kenya, nitatoa *statistic* kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uki-*export avocado* kutoka Kenya, kwanza unapofikisha mzigo ambao uko kwenye kontena *refrigerated*, inachukua siku hiyo hiyo mzigo unaingia kwenye *dock*, unaondika kwenye meli. Ukichelewa sana ni ndani ya masaa 24. Hapa kwetu ukipeleka mzigo kwenye bandari utakaa kwa siku kumi kabla haujaondoka; kati ya tano mpaka siku kumi. Hiyo yote inakupunguzia *shelf life* ya *product* yako na matokeo yake ni kwamba wenzetu kwenye uchumi shindanishi wanaweza wakafikisha *avocado* kwenye soko zikiwa na *shelf life* ya siku kumi na tano. Sisi tunafikisha *parachichi* kwenye masoko zikiwa na *Shelf Life* ndogo sana ya siku tano mpaka siku nane. Kwa hiyo, matokeo yake itakuwa ni ngumu sana sisi kushindana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye mpango, jambo hili limeelezwa vizuri kwamba tutaangalia miundombinu wezeshi, tutaangalia bandari zetu, lakini mara nyingi tunaongea mambo haya kwa ujumla sana, hatuendi kuangalia ni ni hasa kifanyike ili kusaidia wakulima wengi ambao wanahitaji kufikisha haya mazao na kuondoa umasikini wao.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuangalia hilo, kuna gharama. Kwa miaka mingi tutaendelea kutumia Bandari ya Mombasa tupende tusipende. Pia tuna uwezo mkubwa wa kutumia bandari yetu kuondoa kontena la *avocado* kutoka Njombe, kutoka *southern highlands*, au eneo lolote lile, unatakiwa ulipe zaidi ya mtu anayetoa kutoa kontena kutoka maeneo mengine kama ya Nairobi hata maeneo mbalimbali ya Kenya. Sisi tunatakiwa tulipe Dola 4,000 mpaka 5,000 kwa kontena kuliondoa huku na kulifikisha bandarini. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa *THA* itusaidie kwa kuhakisha kwamba moja, ipunguze angalau zile gharama za pale kwenye bandari, lakini ya pili angalau tuwe na *dedicated berth*, najua inaongelewa siku zote, lakini naomba kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri tuje na mipango kabambe, ioneshe wazi kabisa *plan* yetu ni nini? Inakwisha lini? Lini itaanza kuwa *implemented*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke *shippers* hawana mahusiano na mtu yeyote anayezalisha. Wao wanaangalia biashara yao ya *ku-ship*, wanaangalia *risk* ambayo ikoinvolved kwenye *ku-ship products* zetu, wao wataangalia lini waleteli hapa, na kama kuna mzigo wa kutosha, na kama hakuna *risk* yoyote ya hayo mazao kuharibika kabla hawajayachukua. Kwa hiyo, hayo mambo yanafanyika yote kwa pamoja na tuyaangalie kwa makini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana utaona sisi tunaongelea kwamba uchumi wetu kama vile unakua pole pole, lakini ni kama uchumi umeshikwa, umefungwa, tuna bandari, wengine wameongelea *SGR* hapa,

9 NOVEMBA, 2022

inataengenezwa lakini bado kule hatuungalii itafika wapi? Itatoa wapi mzigo? Haya ndiyo mambo ambayo yanafanya tuseme kwamba uchumi wetu ni mkubwa, mnasema uko *stable*, *microeconomics* ziko vizuri, lakini ni kama uchumi umekamatwa, umeshikwa, haupanuki na hauchechemki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea kidogo tu sekta ya madini. Nilikuwa naangalia hapa kwenye Mpango. Ukiangalia kwenye kilimo, tunaongelea utafiti kwamba utafiti ufanyike kwenye mbegu, masoko na miundombinu, lakini ukija kwenye madini, bado suala la utafiti haliongewi hata kidogo, na ile ni moyo na uhai wa sekta ya madini yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme wazi kabisa kwamba tuna *options* mbili kwenye utafiti, au Serikali *i-invest* kiasi kikubwa kwenye makampuni yetu makubwa ya utafiti ya Kitanzani kama *STAMICO*, lakini tunachokiona, na nimesoma ripoti ya CAG; katika moja ya kampuni au mashirika ya kimkakati ambayo yana ukwasi ni pamoja na Shirika la *STAMICO*. Hawana fedha zozote za kutosha kufanya utafiti. Utafiti unataka fedha nyingi sana. Kwa hiyo, *option* iliyobaki ni kuwa na sekta binafsi iweze kuingia kwa kiasi kikubwa kwenye utafiti. Ila sekta binafsi haina urafiki na mtu, yenyewe inaangalia kwamba inaweza ikafanya hii kazi kwa faida huko mbele ya safari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sheria zetu kwa ujumla pamoja na *improvement* yote kwenye *production*, lakini bado kwenye eneo la utafiti sheria zetu hazivutii utafiti katika sekta ya madini. Kwa hiyo, mpango huu kama Waziri atakubali, wajaribu kuangalia ni kwa kiasi gani tunaweza

9 NOVEMBA, 2022

tuka-*incentivize* zaidi sekta ya utafiti ili tuweze kuchimba madini mbalimbali. Mungu ametujalia madini ya kila aina katika nchi hii, kila kona unakoenda kuna madini.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimwa Mwanyika kwa mchango mzuri.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI: Bunge linarejea.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wanamichezo kuwa kutakuwa na vikao na Mheshimiwa Spika kama ifuatavyo:-

Wajumbe wa Kamati Tendaji na Manahodha wote saa 8.30 mchana katika ukumbi wa Spika. Waheshimiwa Wabunge, Wanamichezo wote saa 9.30 alasiri katika ukumbi wa Msekwa. Hii yote itakuwa ni leo.

9 NOVEMBA, 2022

Katibu wa Bunge anaomba kuwa tangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Watumishi wa Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma wako ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kupokea fomu za tamko la mali zilizojazwa kuanzia leo tarehe 9 hadi tarehe 11 Novemba. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kutumia nafasi hii muhimu iliyotolewa na Sekreteriati ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuwasilisha fomu hizo bila kukosa.

Wachangiaji wetu wa jioni tutaanza na Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mheshimiwa Zaytun na Mheshimiwa Mpina.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.59 Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni jioni, wageni waliopo jukwaa la Spika; Wageni wa Bunge; ni Mheshimiwa Ziya Karahan, Mwakilishi wa Heshima wa Tanzania Nchini Uturuki. Mwakilishi huyu ndiyo alikuwa wa kwanza kufungua ubalozi wetu Nchini Uturuki na ametupa heshima kubwa sana na amekuwa ni Mtanzania kwa ndani ya moyo wake.

Amejenga maabara na ameweka vifaa vya *diagnostic* vya *almost* dola milioni moja. Kwa hiyo, karibu sana Balozi nchini Tanzania na karibu Bungeni, karibu sana. Ameambatana na Dkt. Mbaraka Ahmed Abdallah, Daktari

9 NOVEMBA, 2022

wa Tanzania ambaye yupo Uturuki, lakini sasa yupo Zanzibar ambaye anaisaidia Serikali ya Zanzibar, Ndugu Ozgur Dinler, Msaidizi wa Mwakilishi wa Heshimiwa, *madam welcome to the Parliament* na Ndugu Laurent Ntwale, Afisa wa Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashiriki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kutokana na dharura kuwahi ndege itabidi tuwaruhusu wawahi *airport* waendeleo na safari na Mwenyezi Mungu awajalie mfike salama safari yenu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

NGD. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI: Kamati ya Mipango.

NAIBU SPIKA: Kamati ya Mipango.

KAMATI YA MIPANGO

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mchangiaji wetu wa kwanza ambaye tulimtaja toka asubuhi ni Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, wajiandae

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mheshimiwa Zaytuni na Mheshimiwa Mpina.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache kwenye Mapendekezo ya Mpango wetu wa Maendeleo, ambao utaenda kutafsiri mpango wetu wa bajeti wa mwaka wa fedha 2023/2024. Kutokana na ufinyu wa muda, naomba niende haraka haraka. Kwanza, nataka kupendekeza, Mpango huu, ukiuangalia na ukiusoma ni kama *academic paper*. Ni mpango ambao unatengeneza matarajio na tamaa tuliyokuwa nayo. Tumetohoa kutoka kwenye Mpango Mkuu ule wa Miaka Mitano ambao ni mpango wa mwisho kabisa katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya mwaka 2000 - 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba Dira ya Maendeleo inaisha 2025 na huu Mpango wetu una-*overlap* kwenda 2026. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na mipango ambayo tutakuwa tunajitathmini kila wakati katika kutengeneza ule mpango wa mwisho kabisa. Sasa nimesema kwamba kwa jinsi ambavyo unaonekana ni kama vile tumeorodhesha tu tunachotamani kiwepo, lakini kimsingi hauoni ule mpango ndani ya Mpango huu. Sasa napenda kupendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuweza kutengeneza malengo mapana zaidi, hapa malengo yapo matano tu na ukiuangalia yote ni *macro-economic objectives*. Kwa hiyo, tumefinya mpango huu kwenye kutaka ku-*achieve only macro-economic objectives* na wakati mpango mpana ule tumesema tupate *competitive and industrial economy for human development*. Kwa hiyo tuna mambo matatu pale,

9 NOVEMBA, 2022

tuna *competitiveness*, *industrial growth*, lakini pia kuna *human development*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea kwenye malengo makuu yajigawe katika maeneo yote matatu lakini ukiangalia pia imejifinya kabisa, ni maeneo matano tu ya ukuaji wa uchumi, Pato la Taifa, *tax effort*, *tax to GDP ratio*, imejifunga kwenye maeneo matano tu. Kwa hiyo, naomba tupanue twende kwenye maeneo mengine ambayo yanagusa wananchi. Kwa mfano, tunafahamu Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo imekuwa *referred* humu kama moja ya *reference documents*. Inasema ni lazima tutoe ajira kwa vijana kufikia milioni nane mwaka 2025, lakini kwenye mpango huu huoni mwaka huu kwamba tutatengeneza ajira ngapi? Sasa hivi itatuonyesha tu jinsi ambavyo Serikali kuu itaajiri, sijui vibali vya ajira 32,000, sijui na nini, lakini haifanyi *mirroring* kwenye Mpango Mkuu wa Miaka Mitano, tukijikita kwenye maeneo yale ambayo tumejiwekea sisi kama Taifa kama malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo napenda kabisa kwenye Mpango huu tuonyeshe waziwazi, kwa mwaka huu tutatengeneza ajira ngapi za vijana wetu? Mwakani tukifika, ajira ngapi? Kufika 2025 twende tumesema kwamba okay, hizi *indicators* ni *measurable*, tumeweza kuzi-achieve na kwa kweli tumetekeleza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tumesema tunataka tutanue wigo wa kodi, lakini ukisoma *document* huoni kwamba tutatoka kwenye *tax GDP ratio* ya 11.7 kwenda 12 kwa kutumia njia zipi? Je, kutakuwa na mfumo mpya wa kodi? Pili, tutatengeneza *compliance* mpya ya kikodi? Tatu, tutatengeneza mazingira rahisi zaidi ya kikodi? Nne, *existing*

9 NOVEMBA, 2022

taxpayers watatengenezewa utaratibu wa kulipa vizuri zaidi, tutaenda kwenye *TRAB* na *TRAT* kule kwenda ku -*resolve* zile *disputes* nje ya mahakama au tutaenda kutengeneza *taxpayers* wapya ambayo ni walipakodi binafsi kama *personal income taxpayers* au *corporates*, tunaenda kuzalisha walipa kodi wapya kwa kutumia njia ipi, hatuoneshi moja kwa moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango mpana unasema tutakuza eneo la utaalim wa watumishi wetu. Sasa hatuonyeshwi hapa ule utaalim wa watumishi wetu ambao tunalazimika kutoa vibali vya kazi kwa wafanyakazi kutoka nje ya nchi, tunaziba vipi ile *gap*? Tumeambiwa kwenye Mpango Mkuu hata kwenye ile *preface* ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, anasema kabisa pale, tutakwenda kutengeneza wataalam kwenye maeneo mbalimbali ambayo yanahitajika ku-*respond to the market demand*, lakini ukiangalia hapa huoni kwamba mitaala yetu itaendelea kubaki vile vile au itabadilishwa na kama itabadilishwa, itabadilishwa nini? kwa sababu mpango lazima useme, tunaenda kubadilisha nini ili *sector ministry* iwajibike kupitia Mpango huu. Huu Mpango ni Mpango Mama, lakini huoni hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natamani kuona kilichoandikwa kwenye Mpango Mkuu kinatafsiriwa moja kwa moja huku. Kwa mfano, tumesema reli ya kutoka Mtwara kupitia Masasi kwenda Songea na Mbamba Bay pale Ziwa Nyasa na kuwa na *branch spur* kwenda pale Liganga na Mchuchuma pale Ludewa, ambayo baadaye tumesema tuta-*connect* pia kwenda Makambako kuingia kwenye TAZARA. Huo mpango tumeandika kwenye Mpango wa Miaka Mitano kwamba utatekelezwa *under*

9 NOVEMBA, 2022

PPP program, lakini kwenye mwaka huu haijaoneshwa kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba tunasubiri miaka mitatu iliyobakia labda huko ndio tutaonyesha kama mpango. Kwa hiyo, naomba wenzetu wa Wizara ya Fedha waionyeshe hiyo kama ni mpango ambao tunaanza nao mwaka huu, tuta-*attract expression of interests* waweze kuja, kama tunavyofanya kwenye hizo *EPC+F* kwenye maeneo ya barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia pia sekta za uzalishaji, *of course*, sifurahii sana kuona kwamba kwenye mchango wa Taifa wa *GDP*, sekta ambazo zinaongoza ni sekta ambazo, Sanaa na Utamaduni, sijui Habari, Sekta za Uzalishaji za Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Viwanda zipo chini kabisa. Kwa hiyo, nafikiri mpango huu ungeweza kusema. Tuna Viwanda kwa mfano 11 vya Ubanguaji wa Korosho, vikiwemo vya pale Masasi ambavyo ni vikubwa kuliko viwanda vyote pale. Hivi viwanda havifanyi kazi na korosho sasa hivi tumesikia hata bei ya korosho ni *chaos* kule kwetu, bei sasa hivi imetoka shilingi 4,000 kwenda shilingi 1,400 mpaka shilingi 1,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango gani kwenye mwaka huu tuhakikishe kwamba viwanda vyote vya korosho, vya pamba, vya alizeti, vya nini, vitafanya kazi, tuna mpango upi ambao tutaonyesha humu? Ni vizuri tuonyeshe ili ikifika mwakani tunajipima kwamba kweli *intervention* yetu imefanya kazi. Kwa hiyo, tunakuwa na *indicators* ambazo kweli zinaonyesha sisi tunawajibika. La si hivyo tutajikuta tunakuwa na *natural growth* ambayo ilizungumzwa na Mheshimiwa Magessa asubuhi. Ule ukuaji

9 NOVEMBA, 2022

mdogo mdogo wa asilimia 0.2 ile ni *natural growth* ni ukuaji wa asili. *Whether* umefanya kazi au hujafanya, umepanga hujapanga, utakua tu, kwa sababu watu lazima wazalishe, lazima wale lazima wanywe. Kwa hiyo, kuepuka hiyo ili tuonekane na sisi tumefanya kazi yetu vizuri, tutengeneze a *planned growth* ambayo tutakuwa na *growth* kama za wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natamani sana, eneo ambalo tumeligusa na humu limezungumzwa kuboresha huduma za watumishi wa umma kwenye jamii. Tunaboreshaje? Haisemi! Nina mawazo na nikuombe kweli, hili Bunge letu lazima tufikirie, umefika wakati na hata ukiangalia ripoti za CAG, ile ya PAC na LAAC lakini pia PIC ambayo tumejadili wiki iliyopita. Tumeona kuna *laxity* kubwa kwenye *Public Service Management*. Watumishi wa umma wame-relax kabisa kwa sababu tu wana *security* ya kazi zao. Kumfukuza mtumishi wa umma ni shughuli kweli kweli, natamani kweli kwa sasa hivi tumefikia wakati wa teknolojia, tuwe na utaratibu wa mikataba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, kengele ya pili hiyo.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:...kwa watumishi wa umma ili anayefanya vizuri tumpandishe, anayefanya vibaya aondoke, apishe nafasi kwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Dkt. Chaya, wajiandae Mheshimiwa Zaytuni, Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Profesa Mkumbo.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja. Nitajikita zaidi kwenye suala la kilimo, lakini muda ukiniruhusu nitajikita kwenye jinsi gani tunaenda kusimamia mapato ya ndani ya halmashauri zetu ili yatumike kwenye ile miradi ya maendeleo, ile asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wameelekeza hapa, taarifa ambazo Dkt. Mwigulu ame-present hapa, zinaonyesha kwamba kilimo kinachangia takribani asilimia 3.9 kwenye pato la Taifa lakini sekta ndogo ya sanaa imechangia karibia asilimia 19 kwenye pato la Taifa, madini yanachangia asilimia 9.6 na biashara inachangia asilimia 3.5. *We are not serious. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinachukua zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wameji-engage kwenye kilimo. Sasa hivi watu tulionao ni takribani milioni 61, asilimia 65 ya milioni 61 ni takribani watu milioni 40, wapo kwenye shughuli za kilimo. Sasa kama kilimo kinachangia only 3.9 percent kwenye pato la Taifa maana yake kwa mwaka ni watu milioni mbili tu ndio wanaji-engage kwenye kilimo. Ndio maana nilisema kwamba *we are still not serious*, tunahitaji kuipa kipaumbele Sekta ya Kilimo..

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni siasa, siasa zetu hizi zipo kwenye kilimo, lakini kilimo ni amani, kilimo ni furaha,

9 NOVEMBA, 2022

tukikosea kwenye kilimo, tumekosea uchumi. Kwa hiyo, tunahitaji kuwekeza sana kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe alikuja na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Plan II*). Baada ya ule wa kwanza ulioisha 2014, tukatengeneza mwingine ambao tunao, lakini bado tunaangalia *contribution* ya kilimo kwenye uchumi, *it is only 3.9 percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine watu wengi wapo kwenye kilimo na Mheshimiwa Mwigulu anaposema anataka kukuza uchumi, hawezi kukuza uchumi kama anaacha hawa wakulima ambao ni *more than 65 percent*, hapo tutakuwa tunadanganyana, daktari wangu wa uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tu-*invest* kwa hawa 65 percent, tuta-*invest* vipi, niliwahi kuwasilisha hapa Bungeni, sekta ya umwagiliaji ndiyo sekta ambayo tunaweza tukawakomboa wananchi wetu. Tanzania ukiangalia, kuna matatizo makubwa sana, *climate change, semi-arid and arid areas*, haya yote hayawezi ku-*predict* kama tuna uwezo wa kuvuna au hautuwezi kuvuna. Mheshimiwa Mwigulu lazima awekeze kwenye sekta ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo makubwa matatu ambayo yanafanya sekta ya kilimo isiweze kuchangia vizuri kwenye pato la Taifa. Kwanza, tume-*ignore* sana sekta ya umwagiliaji. Nitaonyesha, Bajeti yetu 2019/2020, Serikali ilitenga *only 32 billion (bilioni 32)* kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji; mwaka 2020/2021 Serikali ilitenga

9 NOVEMBA, 2022

only 12 billion (bilioni 12) kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji. Mwaka 2021/2022, mama yetu akaongeza ikafika *46.5 billion* kwenye sekta ndogo ya umwagiliaji. Mwaka huu, mama yetu akatupa bilioni 361.5 kwenye Sekta ndogo ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana na kumshukuru sana Rais. Tumetoka *46 billion* mpaka *361 billion* kwenye Sekta ya Umwagiliaji. Mama yetu ana maono kwenye Sekta ya Kilimo kama nilivyotangulia kusema. Kama tuta-*ignore* Sekta ya Kilimo, tusitegemee uchumi wetu utakua kwa kiwango ambacho tunakitegemea, kwa hiyo lazima tuwekeze kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo manne ambayo yanatusumbua. Jambo la kwanza *financing* hata hii *361 billion* ambayo tumeiweka mwaka huu, ukiongea na wataalam wa *irrigation* wanakwambia kama tunataka kilimo chetu kweli kijikite kwenye umwagiliaji *we need a minimum of 600 billion* (bilioni 600) kwa mwaka. Lazima tuchukue maamuzi magumu, tuwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tunahitaji *a minimum 600 billion* ili angalau tujikite kwenye umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo moja katika umwagiliaji, tuna miradi mingi ya umwagiliaji, lakini *traditional irrigation*, inasubiri mvua, mvua isipokuja zile *scheme* zote zinakufa. *We need to shift*, lazima tuhame kutoka huko. Tunahitaji kujenga mabwawa, najua mwaka huu Mheshimiwa Bashe amekuja na *plan* ya kujenga mabwawa, *we need to transform our agriculture*, lazima tubadilike.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tuna Tume ya Umwagiliaji, ukiangalia ile Tume, ipo Dodoma tu. Vile vile scope yake ni ndogo lazima tui-*transform* hii Tume. Nashauri upande wa Tume kwa nini tusi-*transform* iwe mamlaka. Nimepitia nchi nyingi, kwa mfano Kenya, Kenya wana *National Irrigation Authority*, Ghana wana *National Development Irrigation Authority*. Sasa sisi tuna katume kapo *confined* Dodoma, ukienda wilayani hukakuti, mkoani sijui ndiyo wana mtu mmoja na kadhalika, *no, we need to shift*. Kwa hiyo, nashauri hebu tuibadilishe hii tume yetu iwe na mamlaka kamili wawe na *manpower*. Tunahitaji kuona hii mitambo ipo *located* kule kwenye halmashauri zetu. Hiyo mitambo ya kujenga mabwawa, mitambo ya ku-*repair* hizo *schemes* zetu iwe kule, kuliko mtu anatoka Bukoba anakuja Dodoma kufuatilia mtambo uende ukafanye *maintenance* ya *scheme* iliyoko Bukoba. Kwa hiyo, niliona hilo ni eneo muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kama tunataka kubadilika kwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji Serikali ni lazima iwekeze kwenye *man power*. Tunahitaji vijana ambao ni *trained* kwenye masuala ya *irrigation system*. Tunahitaji watu wa cheti na diploma, hawa ndiyo watakaofanya kazi na wakulima kule vijijini, hatuhitaji *masters* na *degree* kule vijijini, tunahitaji watu wenye *certificate* pia wale wenye *diploma* ambao wataweza kusaidia huku, hilo ni eneo jingine ambalo niliona nilishauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo niliona nishauri ni kwamba, ukiangalia *scheme* zetu nyingi zimechoka sana na nyingi zinategemea mvua kama nilivyosema, tunahitaji kujenga mabwawa. Hatuwezi kujenga mabwawa kwa bajeti ambayo tunaweka, hata

9 NOVEMBA, 2022

hivyo tunamshukuru Mheshimiwa Rais ameliona hili mwaka huu ndiyo maana ame-*shift* bajeti *from 46 Bilioni to 361 billion* haijawahi kutokea, *nine times*. Kwa hiyo hilo ni eneo ambalo ninaomba bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Mwigulu, tunahitaji kuona bajeti angalau ni ya Bilioni 600. Tunataka watu wajikite kwenye kilimo cha umwagiliaji ili tuweze ku-*transform* kilimo chetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, pale Manyoni nina mradi wangu mmoja unaojulikana kama mradi kwa ajili ya ukaguzi wa magari wa pamoja. Mheshimiwa Mwigulu anaufahamu, ule mradi upo chini ya Wizara ya Fedha ulisimama tangu mwaka 2016. Sasa ninakuomba Mheshimiwa Mwigulu, hii ni miradi ya kimkakati ambayo inakuja kuchochea masuala ya uchumi. Hebu nalo liangalie ule mradi wa Muhalala ambao ulisimama pale tangu 2016, mradi wa zaidi ya Bilioni 35 na wenyewe tuufufue ili uweze ku-*stimulate* kwenye masuala ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zaytun, ajiandae Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Mkumbo ajiandae pia.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nikushukuru kwa fursa hii uliyonipa ya kuweza kutoa maoni yangu kwenye Mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2023/2024. Kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti nami nilishiriki katika uchambuzi huu na ninaunga mkono mapendekezo yote ya kamati yaliyotolewa. Nikianza na hali ya uchumi wa Taifa, naomba nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa juhudi

9 NOVEMBA, 2022

zake za kuendeleza ukuaji wa uchumi chanya na tuko kwenye mwelekeo sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hadi robo ya mwaka tulifikia ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.4 kutoka asilimia Tano kipindi kama hichi mwaka jana. Ukiangalia nchi nyingi katika ulimwengu huu sasa mwaka 2021 walikuwa na ukuaji wa uchumi kwenda kwenye uelekeo hasi wa hadi wastani wa asilimia 3.1. Kwenye hili utaona kabisa jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali yetu katika ku-*maintain* uelekeo mzuri wa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Hii yote imechangiwa sana na juhudi za Serikali katika kukabiliana na majanga makubwa na changamoto za kidunia ikiwemo UVIKO-19, kwa hiyo ninaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sheria ya Bajeti, Sura Namba 439 utaona uandaaji wa mapendekezo haya umetumia mambo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2020, vilevile tumeangalia mikakati mbalimbali ambayo tumejiwekea kama Taifa ya maendeleo. Nitaomba nizungumzie jambo moja la mikakati ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, juzi tu hapa, Rais wetu amezindua mkakati kabambe kwa ajili ya Taifa kuhakikisha Watanzania wote wanatumia nishati safi na salama kwa ajili ya kupikia. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huu na huu ndiyo mwelekeo wa kidunia. Ajenda hii ya nishati safi na salama kwa ajili ya kupikia ndiyo mjadala unaoendelea dunia nzima hivi sasa.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu alisema kwamba katika mkakati huo kama Watanzania basi Serikali itahakikisha kwamba Watanzania wote wanatumia nishati safi na salama hadi kufikia mwaka 2032. Kwa hiyo, hii ni dira ya miaka 10 kwa hiyo ninaimani kwamba mkakati huu lazima tuone kwenye mpango wetu wa mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais alienda mbali zaidi na kuzitaka taasisi zote zenye kulisha watu zaidi ya 300 kuweza kutumia nishati safi na salama ndani ya mwaka huu mmoja yaani 2023. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais aliahidi wananchi kwamba Serikali itatenga bajeti kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 zaidi ya Bilioni 23 kwa ajili ya Watanzania waweze kutumia nishati hizi safi na salama kwa ajili ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia mapendekezo haya ya mpango na hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa, lakini sijaona *reflection* ya maagizo haya ya Mheshimiwa Rais kwenye mapendekezo haya ya mpango huu. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri akileta mpango wake hapa wa mwaka 2023/2024, basi tuweze kuona mapendekezo haya ya matumizi ya nishati safi na salama kwa ajili ya kupikia yanaingizwa kwenye mpango huu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa tukiweza kutekeleza nishati safi na salama kwa ajili ya kupikia, basi tutaweza kuokoa maisha ya wananchi wetu wengi ambao wanafariki kwa ajili ya magonjwa ya mifumo ya afya. Vilevile tutaweza kuokoa fedha nyingi za kuwatibu wananchi hawa, pia tutaongeza nguvukazi kwa ajili ya kufanya maendeleo mengine ya Taifa. Vile vile tutaokoa

9 NOVEMBA, 2022

muda wanaopoteza wananchi wetu hususani kinamama wanaopoteza kwenda kutafuta kuni porini na hivyo watatumia muda huo kwa ajili ya kufanya shughuli zingine za maendeleo na kujenga nchi. Vilevile tutaokoa muda wanaopoteza wananchi wetu hususan akina Mama wanapoenda kutafuta kuni porini na hivyo watatumia muda huo kwa ajili ya kufanya shughuli zingine za maendeleo na kujenga nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tutaweza kutunza mazingira yetu ambayo mpaka sasa tathmini zinatambia kwamba tukihitaji tani moja ya mkaa lazima tutumie tani Saba za magogo. Hivyo, tunaona ni jinsi gani suala hili linavyoweza kuharibu mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe maoni yangu kwenye ushirikiano uliopo kati ya Wizara zetu za kisekta na Wizara yetu ya Fedha. Tumejionea hapa mara kwa mara tunaona hakuna *coordination* ya kutosha kati ya Wizara ya Fedha na Wizara hizi za Kisekta. Kama nilivyotoka kueleza hapa, suala la nishati safi na salama unaweza kukuta limebebwa kwa uzito wake na Wizara ya Kisekta lakini halijaweza kuingizwa kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vilevile kwenye suala la *Royal Tour* tumeona kazi kubwa iliyofanywa na Serikali yetu kwa ajili ya kuitangaza nchi yetu kwenye utalii, mpaka sasa hivi tunajivunia kuwa mahoteli yamejaa kwa sababu ya kulaza wageni wetu na *booking* mbalimbali za watalii tuliowapata lakini suala hili halijaingizwa kwenye mpango na ni suala ambalo hata Kamati kipindi kilichopita kwenye bajeti tulishauri Wizara. Kwa hiyo, *lack of coordination* ni jambo ambalo linazisumbua Wizara hizi, naomba sana Waziri

9 NOVEMBA, 2022

pamoja na Serikali tuweze kuwa na mahusiano mazuri ili basi mikakati yetu yote ya Kitaifa iweze kuingia kwenye mipango yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujaza mahoteli tu siyo suala ambalo tunatakiwa tujivunie sana. Mahoteli yakijaa ina maana watalii wetu wakifanya *booking* wanaweza wakaenda hata nchi jirani kwa sababu hoteli zetu zimejaa. Kwa hiyo, kama taifa naomba tuje na mpangomkakati wa kuweza kuongeza hoteli zenye hadhi ya kulaza wageni wetu na kwenye mpango wa 2023/2024, basi tuone mambo haya yakitekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona sekta hii ya utalii ilivyo na nguvu ya kunyanyua uchumi wa nchi na inachangia zaidi ya asilimia 17 ya Pato la Taifa lakini asilimia 25 ya fedha za kigeni, hivyo ni muhimu sana tuweze kujikita kwenye sekta hii ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Vilevile tuendeele kuongeza bajeti katika Wizara hii ili basi tuweze kuistawisha sekta hii zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Mpina, ajiandae Mheshimiwa Mkumbo na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae pia.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2023/2024 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya mwaka 2023/2024.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeze Serikali kwa hatua iliyofikia katika ujenzi wa Bwawa la Kidunda ambapo sasa wamepata Mkandarasi sasa tunaenda kupata majawabu ya tatizo la maji katika Mkoa wa Pwani, Morogoro pamoja na Dar es Salaam, lakini wahakikishe kwamba ule mradi wa Ziwa Viktoria kwa Mkoa wa Simiyu ambao karibia Wilaya zote za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa, Meatu zote zinahusika na huu mradi na wananchi wanausubiri kwa hamu. Wananchi wa Jimbo langu la Kisesa wanausubiri kwa hamu sana mradi huu kumaliza tatizo la maji ya kunywa, maji ya mifugo, maji ya kilimo na maji ya shughuli mbalimbali zingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la *scheme* za umwagiliaji, Wizara inayohusika isisahau kwamba hata huko Simiyu na hata huko Kisesa kuna maeneo mazuri tu kwa ajili ya shughuli za kilimo cha umwagiliaji, hata pamba inawezekana kufanyiwa *scheme* za umwagiliaji.

Mheshimiwa mwenyekiti, ili tuweze kuwa na mipango mizuri na tuweze kupiga hatua za maendeleo, tunahitaji sana uwekezaji mkubwa kwenye eneo la utafiti. Tunatakiwa tupeleke fedha nyingi *COSTECH, TARI, TAFIRI* na *TAWIRI* ili tuweze kupata majawabu ya maendeleo yetu kwa wakati. Mpango huu pia usisahau kutenga fedha za daraja la Mwamhuge kule Jimboni kwangu mpakani mwa Meatu na Maswa ni daraja la muda mrefu na limeahidiwa na Serikali pia daraja la Mto Sanjo ambao ni mpakani mwa Itilima na Meatu, hilo ni daraja la muda mrefu sana kwa hiyo Wizara inayohusika itenge fedha kwa ajili ya hilo daraja.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna daraja la Mwambuzo mpakani mwa Meatu na Igunga na Kishapu, hili daraja nalo litengewe fedha ili kuweza kupiga hatua za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na wenzangu wamezungumza hapa, Serikali imepiga hatua kubwa sana katika kutafuta masoko ya mazao yetu na huu ndiyo uelekeo tunaoutaka. Mazao ya korosho, parachichi, pamba na mpunga. Kwa kweli katika hili eneo, ninaishukuru sana Serikali kwa sababu wananchi wetu watakapofanya uzalishaji kwa wingi wanapata soko la uhakika. Hili tunaendelea kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuifungua nchi yetu na kutafuta masoko makubwa Tanzania, kuitafutia nchi yetu masoko makubwa ili kuiunganisha na dunia ili wakulima wetu waweze kulima na kuuza, waweze kuzalisha na kuuza mazao ya samaki, mabondo, tumeona mikataba ya mazao ya mabondo, tumeona mikataba ya samaki na mikataba mingine ambayo ni makubaliano ya masoko mapya. Hiyo ni hatua kubwa sana kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mpango umezungumza na Kamati imezungumza. Hapa kwenye Bunge lako nilipendekeza kwamba iundwe Kamati Teule ya Bunge ili kufuatilia ukweli juu ya jambo hili, kwa sababu mara nyingi tumekuwa tukiletewa taarifa ambazo zina mkanganyiko. Leo hii Kamati ya Bajeti imeenda kuthibitisha hilo kwamba taarifa zenye mkanganyiko zimewasilishwa. Mpaka sasa hivi mkataba baina ya TANESCO na Arab Contractors haujulikani kwamba huo muda uliyoongezwa ni

9 NOVEMBA, 2022

muda gani. TANESCO wanasema ni mwaka mmoja (miezi 12) wameongeza. Maana yake kufukia Tarehe 15, Juni 2023 mradi huu utamalizika lakini *Contractor* pamoja na Wizara na hapa Bungeni tumeambiwa huu mradi utaisha Julai mwaka 2024, miaka miwili kwa maana ya miezi 24, sasa Bunge lako lishike taarifa gani ya kufanyia kazi juu ya hili jambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeeleza kwamba, mkataba huu umeongezwa bila sababu za msingi, mkataba wa Bwawa la Mwalimu Nyerere baina ya *Contractor* umeongezwa bila sababu za msingi na bila kufanya tathmini, bila kubaini gharama za ongezeko pia gharama hizo za ongezeko la muda zitabebwa na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiyauliza haya lakini mara inaelezwa kwamba wako kwenye mvutano, hivi wanavutana jambo gani? Mradi umeshafikia asilimia 75 mnavutana nini? Ni hatari sana kwa mradi uliofikia hatua hiyo halafu mkaingia kwenye mvutano. Tumeuliza hapa mara nyingi hatuelezwi na Kamati nayo imelalamika, mkataba wetu unasema lazima walipe CSR Shilingi Bilioni 260, ailimia Nne ya mkataba mpaka sasa hivi tunaendelea kuwalipa hawa zaidi ya asilimia 70 sasa, lakini hizi fedha hazikatwi na maelezo hayatolewi, tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Kamati zote zimeshasema, Kamati ya Nishati na Kamati ya Bajeti, kwamba sababu za ucheleweshaji zimesababishwa na Mkandarasi mwenyewe kwa uzembe wake. Sasa kama sababu ni hizo, mkataba wetu unasema, ucheleweshaji wa uzembe ni asilimia 10 ya thamani ya mradi. Asimilia 10 ya trilioni 6.4 ni shilingi bilioni 650, anachelewesha kwa miaka

9 NOVEMBA, 2022

miwili ambayo ni trilioni 1.3, hizi fedha mbona haziombwi? Hakuna mahali popote ambapo Wizara utaiona hata hapa Bungeni ikizungumza kwamba tumeenda kumchaji hizo fedha hakuna hatuelezwi! Zaidi Wizara imekuja hapa inamtetea Mkandarasi, unajua zilikuwa ni sababu za UVIKO-19 lakini Kamati zote zimeshakataa kwamba sababu siyo UVIKO-19, huu ni uzembe wa Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini huyu Mkandarasi anabebwa kwa kiwango hicho? Sababu za kubebwa huyu mkandarasi ni nini? Sasa hivi kama tumefikia 70%, hizi fedha tutakuja kuzi-recover na nini? Tunamdai shilingi trilioni 1.3 kwa ucheleweshaji wa mwaka mzima, tunamdai shilingi bilioni 260 kwa ucheleweshaji wa miaka miwili, tunamdai shilingi bilioni 260 za CSR, hizi fedha hazijalipwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza *seriously* kwamba hili jambo kama Serikali kila leo imekuwa ikipiga danadana kulifanya, basi iundwe Kamati Teule ya Bunge tuende tukaujue ukweli. Jambo la pili, Bunge liagize Wizara ya Nishati ikazidai zile fedha, shilingi trilioni 1.56 tunazihitaji kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Deni la Taifa. Deni la Taifa takwimu zinaonesha hapa kutoka Aprili 2021 na kufikia Aprili 2022 limeongezeka kwa shilingi trilioni 8.7, hili ni ongezeko la asilimia 14.4. Hili ongezeko linaongezekaje kwa kiwango hicho wakati deni wakati huo tulili-service kwa shilingi trilioni 7.2, maana yake Serikali katika kipindi hicho imekopa shilingi trilioni 15.92. Hapa Bungeni tuliiruhusu Serikali ikakope shilingi trilioni 10.5, kwa nini Serikali imeenda kukopa zaidi ya kiwango kilichoruhusiwa na Bunge? Kama miradi iliyoidhinishwa na Bunge hapa kwa kasma ya

9 NOVEMBA, 2022

kiwango kilichoruhusiwa kwenda kukopwa pamoja na mapato ya ndani, hizi fedha za ziada zilizokopwa na Serikali zilienda kutekeleza miradi gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ukiangalia *trend* ya ongezeko la Deni la Taifa, Deni la Taifa lilikuwa linaongezeka kwa asilimia saba mwaka 2019/2020, lakini ilipofika mwaka 2020/2021, Deni la Taifa likaongezeka kwa wastani wa asilimia 13.7 na mwaka 2022 limeongezeka kwa asilimia 11. Ongezeko hili ni karibia mara mbili, sasa tumefikaje hapa na bahati mbaya sana niliuliza kipindi cha bajeti hili jambo sikupewa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili la Deni la Taifa kwa *speed* kubwa, uwezo wetu wa kukusanya mapato kwa Pato la Taifa ni 11.4%, nchi jirani ya wenzetu wa Kenya ni asilimia 13.7 lakini nchi ya Rwanda ni asilimia 15.9, madeni haya tumefikia hapa. CAG afanye uchunguzi kwenye hili eneo na Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu jambo hili. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Mkumbo, ajiandae Mheshimiwa Khadija Aboud.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba nami nichangie kwenye mpango huu, niongeze mambo matatu ambayo siyaoni kwenye mpango. Kabla sijaongeza hiyo, niseme kwamba mpango huu ni muhimu sana kwa sababu ndiyo mpango wa kwanza tangu tutoke kwenye janga la *COVID-19*, lakini ndiyo mpango ambao utatuambia ni kwa kiasi gani tunaenda kukamilisha au ku-*achieve our National Development Vision 2025*. Umuhimu wake ni mkubwa sana

9 NOVEMBA, 2022

na tunafahamu kwamba moja ya mafanikio ya jumla ambayo tuliyapata mwaka 2021 ni Benki ya Dunia kuitangaza Tanzania kwamba imefika uchumi wa kati (*Lower Middle-Income Country*) pamoja na kwamba suala hili itakuwa ni muhimu Mheshimiwa Waziri akalitolea msimamo baadae kwa sababu tunasikia takwimu zingine zinasema tumeshuka, nyingine tuko pale pale, ni muhimu Serikali ikaliweka vizuri jambo hili ni kubwa sana siyo jambo la kupita hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa nasoma taarifa za *World Bank* kwenye website yao na Waheshimiwa Wabunge, mnaweza mka-google, wana-update kila baada ya muda fulani. Kwa mujibu wa takwimu hizi za Benki ya Dunia, nchi yetu mwaka 2021 ilikadiriwa kuwa na pato la dola za Marekani bilioni 67.78 na siyo bilioni 62. Ukifanya hesabu kwa idadi ya watu wa sasa hiyo inatupa *GDP per capita income* ya dola za Kimarekani 1,135.5. Kwa hivyo, utaona kwamba tumepanda kidogo kuliko mwaka 2020. Kwa hiyo, ni hoja kwamba tumeshuka haiwezi kuwa kweli na ni muhimu tukalinda mafanikio yetu kwa wivu mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningepomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha utakapohitimisha hili jambo alitolee kauli nzito ya kueleweka ili nchi isibabaike. Tumeshuka au tuko pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo matatu ambayo ningependa kuyaangalia ambayo siyaoni kwenye mpango vizuri. La kwanza ni suala la umuhimu wa kuendelea kupambana na umaskini. Ukichukua mpango wetu wa maendeleo ukurasa wa kwanza kabisa kuna ujumbe

9 NOVEMBA, 2022

mahususi wa Mheshimiwa Rais pale. Na katika ujumbe mahususi huo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan alieleza kwa uzito changamoto ya umaskini, na alitumia maneno haya naomba ninukuu; "Tunapoanza utekelezaji wa mpango wa tatu sote tunatambua changamoto nzito mbele yetu, umaskini bado unaendelea kuwepo nchini licha ya jitihada kubwa, zinazowekwa katika kuimarisha maendeleo ya watu. Aidha utofauti wa kiwango cha kipato na matumizi unaendelea kuwepo katika jamii zetu, ikiwa ni moja ya kati ya viashiria vikubwa katika kufikia malengo kusudiwa ya Dira ya Taifa ya Maendeleo. Moja ya sababu za msingi za maendeleo hafifu wa upunguaji wa umaskini licha ya ukuaji imara wa uchumi ni kutokufanikiwa kikamilifu kwa Tanzania katika kuongeza tija na uzalishaji katika sekta za msingi".

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio maneno ya Mheshimiwa Rais kwenye utangulizi wa Mpango wa Maendeleo. Anatambua kwamba, bila kuwekeza katika sera za msingi za kuongeza tija hatuwezi kutoka. Kwa hiyo hilo ni jambo kubwa lakini ikifika Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, lengo namba 12 linazungumzia umaskini tu; na linasema, kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi jumuishi na shirikishi kupitia mikakati ya kupunguza umaskini. Hili ni jambo la msingi sana katika mpango wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti utafiti wa Benki ya Dunia unaonesha waziwazi kwamba kutokana na janga la Covid watu 140,000 katika nchi hii walipoteza kazi katika sekta rasmi. Watu milioni 2.2 walipoteza kipato. Utafiti unaonesha vilevile kwamba bila kuchukua hatua mahususi watu 600,000 watatupwa kwenye dimbwi la umaskini. Kwa hiyo ni

9 NOVEMBA, 2022

muhimu mpango wa maendeleo uoneshe jitihada za kushughulikia umaskini bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma mpango katika kurasa 161 nilikuwa na-set pale, katika mpango mzima neno umaskini limejitokeza mara moja tu, na limetajwa kwenye suala la kushughulikia kunusuru kaya maskini. Hii haitoshi, tuwaombe wataalam wetu warudi katika mapendekezo ya mpango watuletee mikakati ya kupunguza umaskini katika nchi hii, hili ni jambo la msingi sana. Katika mpango tutakaokuja kuupitisha mwezi wa pili tuone bayana mikakati inayoshughulikia umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo sijaliona ni suala la idadi ya watu. Nchi yetu sasa tunafahamu hatubahatishi tena, tupo milioni 61.7 na tumekua kwa kiwango cha asilimia 3.2, ongezeko kubwa kuliko miaka yote ya sensa. 1989 mpaka mwaka 2002 ilikuwa asilimia 2.9, 2012 ilikuwa asilimia 2.7 sasa hivi ni asilimia 3.2 ndiyo kubwa kuliko tangu tuanze kuchukua sensa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko kubwa la idadi ya watu lina sura mbili. Sura ya kwanza ni fursa, kwamba mpo wengi kwa hivyo nyie ni soko. Sura ya pili ni kwamba mna uhakika wa wafanyakazi wenye nguvu za kufanya kazi kwa sababu mko wengi. Pia uzuri ni kwamba kwa *structure* ya *population* yetu asilimia 70 wapo chini ya miaka 35. Kwa hiyo kwa kweli watu wetu wengi tulionao katika nchi hii ni watoto na vijana. Na ndiyo maana hata mimi mwenyewe mwenye miaka 50+ siku hizi vijana wananiita mzee. Mzee kwa sababu gani? nimekuja kugundua hata kama watu wengi ni watoto na vijana wewe miaka 50+ wewe ni mzee bwana, kwa hili ni sawa.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili uipate hiyo unahitaji nini? *population dividends* wanaita wataalam. Kwanza lazima uwekeze katika elimu sana. Lazima uwekeze katika mpango kupunguza umaskini, lazima uwe na chakula cha kutosha. Bahati mbaya sisi kwa sasa takriban kila kitu hakitoshi. Katika shule kama ni madarasa, kama ni waalimu, *everything you talk about* haitoshi, maana yake nini? lazima turudi katika miaka ya 1970, 1980, tuanze kuzungumzia suala la uzazi wa mpango, hili jambo haliwezi kukwepeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ilikuwa champion wa *family planning 1970's, 1980's* na ndiyo maana tukaweza kupunguza ongezeko la kasi kiasi hicho. Hapa tulipofika lazima hilo lifanyike, na mimi napendekeza kabisa kwamba tufanyie mabadiliko *Tanzania Commission for Aids* tuiongezee jukumu la *family planning*. Haya ni pendekezo langu ambalo nimeona kwamba ni muhimu kwamba ni muhimu yaingie kwenye mpango wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho, tumesema kwenye lengo namba 11 kuimarisha jukumu la Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kuleta maendeleo na kuongeza kipato katika ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye mpango huu, huoni chochote kuhusu kuimarisha *Local Government Authorities*. Nimeshasema na ninarudia tena. Itakuwa ni vigumu sana kwa nchi hii kudhani kwamba tunaweza kupinga kasi ya maendeleo *from the center*. Nchi hii ni kubwa, ina watu wengi lazima tuimarishe Serikali za Mitaa. Na katika kuimarisha Serikali za Mitaa tunazungumzia *income*, vyanzo vya mapato katika *Local Government Authorities* havipo. Tungetaka kuona mpango wa

9 NOVEMBA, 2022

maendeleo *deliberately* kabisa unaanzisha vyanzo vipya vya mapato...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkumbo kengele ya pili ahsante...

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Hadija Hassan Aboud, jiandae Mheshimiwa Mgalu, jiandae Mheshimiwa Sima.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha, kwa mpango wake mzuri aliotuletea kwa mustakabali mzima wa Taifa letu. Nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan. Pia nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ndugu yetu Hussen Ali Hassan Mwinyi kwa ushirikiano wao wa pamoja katika kuwaletea wananchi wa Tanzania maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo, na nitajielekeza kwenye sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi. Naipongeza Serikali kwa kuwekeza fedha nyingi katika sekta hizi za uzalishaji ambazo lengo lake ni kuimarisha sekta hizi kwa manufaa ya Watanzania. Ni vyema sasa uwekezaji huu mkubwa unaowekezwa na nchi yetu tuone matokeo

9 NOVEMBA, 2022

makubwa pia ya uwekezaji huu kwa sababu ni fedha nyingi sana zimewekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inategemea sana usalama, hasa usalama wa nchi kwa maana ya mipaka, usalama wa ndani ya nchi kwa maana ya wananchi na mali zao, lakini hapo hapo inategemea usalama wa nchi kwa maana ya chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuelekeze zaidi kuwekeza kwenye *NFRA*, kwa ajili ya kujiwekea usalama wa chakula ndani ya nchi pindi tutakapofikwa na majanga, maafa na maswaibu mbalimbali ndani ya nchi yetu ambayo yanasababishwa na mambo mengi ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi na mambo ya dunia yanayojitokeza. Kwa hiyo kwenye *NFRA* tukiwekeza vya kutosha ule usalama wa nchi utakamilika, kwa maana ya mipaka, raia, mali zao na usalama wa matumbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea hapo hapo kwenye sekta ya kilimo, tumeona kwenye mipango kwamba kuna mipango inafanywa kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo, kuimarisha tafiti, kuimarisha mambo ya mbegu bora. Pia kwenye suala la mbolea kuna watafiti wetu wamegundua kilimo ambacho kinaitwa kilimo hai na kilimo hifadhi. Hiki kilimo hai na kilimo hifadhi kinakwenda kulinda na kuhifadhi ardhi na udongo wa nchi yetu na pia kinatoa matunda bora ambayo hayana kemikali zozote za viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaunge mkono watafiti hawa ili elimu hii isambae kwa wananchi wetu waweze

9 NOVEMBA, 2022

kulima bila kutegemea mbolea ambazo wakati mwingine zinakwama kufika kwa wakati, wakajitengenezea wenyewe mbolea zao na mambo yao mengine ya ughani kwa kutumia kilimo hifadhi na kilimo hai. Tumeona matunda yanayolimwa kutokana na kilimo hai na kilimo hifadhi ni matunda mazuri na yana soko kubwa katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa kilimo, nashauri tujielekeze sasa kwenye mpango wa muda mfupi na mpango wa muda mrefu, kwa baadhi ya mazao. Tuna uhaba wa sukari, mafuta ya kula na ngano ndani ya nchi. Ni vyema sasa tukajipangia mipango kumaliza tatizo japo kuna zao moja la sukari, ama ngano, ama mafuta; ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, miwili au mitatu. Tuache tabia ya kuagiza nje mazao haya kwa sababu ardhi tunayo ya kutosha, wataalam tunao, fedha tushapata, mitaji kama hii kwenye kilimo. Basi tuseme ndani ya miaka mitatu au minne tutaachana na kuagiza sukari ama unga wa ngano, ama mafuta ya kula. Tujielekeze hivyo tuzalishe ndani ya nchi, tujitosheleze, pia tuweze kupata soko la nje kwa mazao tutakayozalisha ndani ya nchi huku tukiendelea na mazao yetu mengine ya biashara yakiwemo mazao ya bustani, mbogamboga na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitishwa sana kwa taarifa ya Kamati kuona kwamba Serikali imewekeza fedha nyingi kununua vitendea kazi vya Maafisa Ugani ikiwemo pikipiki, lakini kumbe kuna baadhi ya pikipiki zile hazifanyi kazi iliyokusudiwa eti kwa tatizo tu la kukosa mafuta. Tunawekeza fedha nyingi kwa Maafisa Ugani, tumewapa vitendea kazi, Serikali imetoa ili wawafikie wakulima lakini kweli inashindikana mafuta ya kuweza kuwafikia wakulima wale. Kamati imeelekeza kwamba halmashauri zitenge

9 NOVEMBA, 2022

fedha kwa ajili ya kugharamia mafuta. Lakini haya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuna kodi inachukuliwa pale kwa halmashauri sasa si ndio hapo pa kuwekeza ili ile kodi iwe kubwa zaidi tuongeze mapato kwa sababu kilimo kikikua na mapato yanakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye sekta ya uvuvi tumeona hapa kuna nchi zinaendeshwa uvuvi katika dunia. Tujielekeze zaidi kwenye uvuvi wa Bahari Kuu kama mipango ya Serikali na pia tiliimarisha Shirika la *TAFICO* na *ZAFICO* kwa sababu uvuvi wa Bahari Kuu ni chombo cha Muungano. Kwa hiyo kwa upande wa *TAFICO* zinawekezwa fedha lakini bajeti haikidhi kwa sababu *TAFICO* inahitaji uwekezaji mkubwa, kwa maana ya kuwekeza fedha pale *TAFICO* kulifufua. Shirika linahitaji gati na mitambo ya baridi ya kuhifadhia Samaki, shirika linahitaji kila kitu kwa maana na hata baadhi ya majengo tayari yameanza kumomonyoka kwakuwa yanaliwa na dahari. Pale uwekezaji wake ni mkubwa hivyo ni lazima tuwekeze fedha za kutosha ili kulifufua hili shirika kwa haraka, kwa sababu ni muda mrefu sasa tunazungumzia *TAFICO* lakini *TAFICO* yenyewe bado haijaanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye samaki hatuhitaji mbolea, ugani wala kupalilia. Samaki tunachokitaka ni kuhifadhi matumbawe na kuweka mazingira ya kudhibiti uvuvi haramu, tuvue, hakuna hasara nyingine pale inapayotikana, Mwenyezi Mungu katujalia ile baraka ya Samaki tunawaacha, na Samaki wanatembea kokote duniani, yeyote anaweza akamvua, huwezi kumwekea mipaka. kwamba mimi ninamzuia mpaka shirika langu la *TAFICO* liwe salama ndipo tuweze kufanya kazi ya kuvua Samaki. *TAFICO* ikifufuliwa ikapewa mtaji wa kutosha

9 NOVEMBA, 2022

tutaanza kuvuna rasilimali ya bahari kwa wingi zaidi na bila ya gharama kubwa. Gharama yetu ni uwekezaji kwenye TAFICO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nagusia sekta ya maji ambayo imezungumzwa sana, na mimi nashauri kwenye jambo moja. Kuna gharama kubwa ya uendeshaji wa maji katika visima kwa kutumia nishati ya umeme. Ni vyema sasa Serikali ikaona namna ya kupunguza kodi au ongezeko la thamani (VAT) au kutoa ushuru mwingine kuhakikisha hizi mashine za solar za kupandishia maji na kuendesha mitambo ya maji ili kupunguza gharama kubwa kwa wananchi kule vijijini ya kutumia nishati ya umeme...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante...

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Subira Mgalu, jiandae Mheshimiwa Sima, jiandae Mheshimiwa Stella Simon Fiyao.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuwa sehemu ya kutoa mchango kwenye taarifa iliyowalishwa na Mheshimiwa Waziri kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2023/2024.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwanza kwa kuwa taarifa ambayo amewasilisha imefanya tathmini imetutaarifu utekelezaji wa bajeti ya 2021/2022. Napenda niipongeze sana Serikali kwa mafanikio mbalimbali waliopata ikiwemo kwenye ukusanyaji wa mapato na kupeleka pesa nyingi za maendeleo kupitia mapato ya ndani, kwa hiyo naipongeza sana Serikali. Vilevile, kwa kuwa pia taarifa imeonesha utekelezaji wa bajeti wa 2022/2023 robo ya kwanza, kwamba tunaendelea vizuri naomba niipongeze sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango huu ambao umewasilishwa wa mapendekezo naomba nipendekeze mpango huo utakapokuja sasa uainishe na uweke bajeti ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Hali ilivyo katika dunia na nchini kwetu si nzuri. Tumeona ukame, tumeona shida ya maji na tumeona namna gani hata hali ambayo inakwenda kuwa tete. Kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri katika hili ni kulizingatia; na kwa kuwa tunajua hata sasa hivi Rais wetu yuko nchini Misri akihudhuria Mkutano wa Nchi kwa ajili ya mabadiliko ya tabianchi, kwa hiyo ninaomba sana jambo hili litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo nipongeze kazi nzuri inayofanywa kwenye miradi ya kimkakati hususan, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Katika ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kama ambavyo Kamati tumesema, kwamba kazi inaendelea vizuri na hata taarifa ya leo ambapo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekutana na Mheshimiwa Rais wa Misri inaonekana kazi imefika asilimia 77 na kwamba Maraisi hao wawili wameona kazi nzuri inayofanyika. Na kwa mujibu wa taarifa ya kwenye vyombo vya habari wamekubaliana kwamba bora

9 NOVEMBA, 2022

bwawa lichelewe lakini lijengwe kwa viwango vinavyokusudiwa na ubora wa hali ya juu. Kwa hiyo mimi nadhani kwa kuwa Marais hawa na kwa kuwa kazi inaonekana ni nzuri tuipe nafasi Serikali iendelee kutekeleza ujenzi wa bwawa hili kwa sababu mambo yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa ile CSR ya bilioni 260, kwa kuwa tangu mkataba umesainiwa tarehe 15 Desemba, 2018 mpaka leo CSR zile hazijatumika kwa kuwa kulikuwa na mabishano. Lakini sasa TANESCO imewasilisha miradi kama minne, ujenzi wa vyo katika Mkoa wa Lindi, Kigoma, Tanga na Dodoma. Lakini sisi Mkoa wa Pwani na Morogoro tumeomba kwa kuwa kwa mujibu wa mkataba CSR inatumika kwenye maeneo yaliyokusudiwa. Ninaiomba Serikali hili litazamwe kwa jicho la huruma Mkoa wa Pwani na Morogoro maeneo ya Mwaseni na Kisaki tupate miradi kutokana na bilioni 260.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwa kuwa hata taarifa ya leo imesema Mheshimiwa Rais Samia ameeleza kwamba bwawalinakaribia kuanza kujazwa maji. Vilevile, kwa kuwa kuna hali ya mazingira ya mito inayotiririsha kwenye Mto Rufiji Mito ya Ruegu, Ruaha Mkuu na Mto Kilombero kuwa na hali ya uchafuzi wa mazingira na ukame unaoendelea ninashauri Serikali sehemu ya bilioni 260 zitumike kupambana na mazingira ya maeneo hayo, upandaji wa miti, uondoaji wa mifugo kwenye mito yote hiyo inayopeleka maji Mto Rufiji ili zoezi likianza la kuweka maji kwenye bwawa letu lipate mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Wizara ya Nishati kwa Kongamano la Nishati Safi ya Kupikia. Jambo ambalo

9 NOVEMBA, 2022

kwa mara ya kwanza linaenda kutiliwa mkazo. Baada ya mafanikio ya kumtua mama ndoo kichwani Mheshimiwa Rais amekuja na kampeni hiyo. Sehemu ya bilioni 260 basi zitumike pia kama mchango katika kuhakikisha maeneo yaliyoharibiwa kwa kasi ya ukataji wa miti, zinatumika kurejesha mazingira mazuri katika maeneo hayo ili mradi wetu huu uweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Wilaya ya Rufiji, Wilaya ya Morogoro Vijijini, Wilaya ya Kibiti tukumbukwe kwenye Shilingi bilioni 260, na ni haki yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nipongeze; katika hali ya kupambana na mazingira ya ukame yaliyopelekea hali ya upatikanaji wa maji kuwa ngumu, naipongeza sana Serikali chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza kuanza kwa kutekeleza mradi wa maji wa kuyatoa Mto Rufiji. Jambo hili halikupata kufikiriwa, lakini ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita mmekuja na mradi huo. Maana yake maji yatatoka Mloka, yatapita Vikumbulu, yatakuja Kisarawe na Dar es Salaam. Maji yatatoka Mloka yatapita Mkongo, yatakuja Rufiji, Kibiti, Mkuranga na Dar es Salaam. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali na kuipongeza kwa kuanza ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Naomba miradi hii ionekane waziwazi katika mpango unaotarajiwa wa 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wowote unahitaji mapato. Nimeona matarajio ya Mpango wa 2023/2024 wa kukusanya zaidi ya shilingi trilioni 43 na matumizi ya hizo shilingi trilioni 43. Naomba niishauri Serikali kuendelea kutilia mkazo namna ya matumizi sahihi ya mashine za kutolea

9 NOVEMBA, 2022

risiti. Tumeona kwenye ripoti ya CAG kwamba baadhi ya *sampling* ya watu 3,594, waliyoifanya kwa baadhi ya wafanyabiashara kwenye mikoa 15 ya kikodi, wafanyabiashara 1,794 hawakuwa wanatumia mashine za kutolea risiti. Mheshimiwa Waziri hata kwenye taarifa zako umekuwa ukitoa. Sambamba na hilo, kuna baadhi ya wafanyabiashara *sampling* zaidi ya 10,000 hawakufikiwa hata kukaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mamlaka hii Mheshimiwa Rais ameitilia mkazo na kuipa kibali, kwa mara ya kwanza imeajiri watumishi 1,200 kwa mkupuo tangu Mamlaka hii imeanzishwa. Napongeza sana hatua hii. Naiomba Serikali iwatumie kikamilifu kuwafikia wafanyabiashara wengi wakaguliwe, watathminiwe hatua za kikodi, na tutumie takwimu za Sensa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Albina Chuwa alisema siku ile ya uzinduzi wa matokeo kwamba Sensa hii itabainisha wafanyabiashara wako wangapi na Shughuli zao mbalimbali. Natamani kuona mpango ujao uainishe ongezeko ya walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, tuna Muswada wa Bima ya Afya unaokuja Ijumaa, lakini kwenye Mpango huu haijaonekana wazi wazi. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, hilo lizingatiwe kwa sababu kwa kuwa wanawake tuko wengi tuna matarajio sana na hii Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Sima, halafu Mheshimiwa Stella ajiandae.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pia nakupongeza sana kwa namna ambavyo unaendesha mjadala huu kwa kutoa elimu ya namna ya kuujadili mjadala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze vijana wangu wa *Singida Big Stars*, leo katika uwanja wa nyumbani wameendelea kutunza heshima ya uwanja ule na kuwafanya watani zetu Simba kushindwa kufurukuta. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sima, kanuni zetu zinasema, mchango wako ujadili jambo ambalo lipo kwenye Meza. Hoja ya hapa ni Mipango *(Kicheko/Makofi)*

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea maelekezo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nizungumzie sana eneo la elimu. Kwenye elimu *vision* ya 2025 inataka tuwe na jamii iliyoelimika, ikiwa na maana ya *well educated and learning society* ambapo tunataka tuwe tumefikia kwenye *high level of quality education*. Serikali imefanya kazi kubwa sana. Nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kwa dhati kuanzia chekechea mtoto anaanza shule mpaka kidato cha sita anasoma bure, Elimu Bila Malipo. Hili ni

9 NOVEMBA, 2022

jambo kubwa sana. Naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, imeongeza *enrolment*, watoto wengi sasa wameingia shule na ninaamini mwakani wengi wataingia, na Serikali imeboresha miundombinu. Hivi tunavyozungumza, Serikali imetoa fedha nyingi za kujenga madarasa, na kujenga shule. Hili ni jambo jema sana, naipongeza sana Serikali kwa kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hapa tunazungumzia elimu. Elimu ina pande mbili; kuna elimu nyooofu na elimu ya kati (*alternative*). Leo mahitaji yetu ni nini kwenye Mpango huu? Elimu nyooofu maana yake, tunatarajia mtoto akianza darasa la kwanza, mpaka anamaliza Chuo Kikuu. Leo chukulia shule ambayo ina watoto wasiopungua 1,000 mpaka 4,000, wote hawa tunatarajia wamalize. Huko mbele wanakoendelea, maana yake watakuwa wanaenda wachache, wengine watabaki mtaani. Sasa Mpango unatuelekeza nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maelekezo ya Mpango, tumezungumzia hapa kuhuisha; naomba nisome hapa; mpango umesema, “kuhiiwisha mitaala ili iendane na soko la ajira.” Hapo lazima tufike mahali tuelewane. Kwanza, kuhuisha mitaala uendane na soko la ajira. Maana yake kuna tatizo hapa ambalo Serikali haijalibanisha moja kwa moja, nami nataka niwakumbushe, kuna ile Tume ya Mipango, iliyotoa taarifa hii mwaka 2014. Nilisema, Mwenyekiti wa wakati huo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Mpango ambaye ni Makamu wa Rais wa leo. Sasa kama tunatambua kwamba Tume ya Mipango ilifanya kazi nzuri,

9 NOVEMBA, 2022

tuna kila sababu ya kuihuisha ile tume ili ifanye kazi hii na kutuletea matokeo yaliyo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa nataka niongeze jambo moja jepesi sana. Kuanzishwa mtaala ni jambo moja, lakini kuhuisha ni jambo lingine. Hapa tuzungumzie mtaala ambao unaongelea *practical oriented*. Hatuwezi kuwa na mtaala ambao hauongelei suala la *practical*. Tunahitaji elimu yetu iwe *practical* zaidi. Sisi ambao tulimalizia malizia kusoma zamani, kuanzia shule ya msingi mpaka sekondari tulikuwa na karakana na shule za ufundi. Shule zote hizi zilimwezesha Mtanzania aliyemaliza shule aweze kukabiliana na maisha yake ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiishie hapo. Tunapotaka kujenga ujuzi na umahiri wa mwanafunzi ili aweze kukabiliana na maisha yake, tusiishie hapo. Mtaala huu lazima uzungumzie michezo *(sports and games)*. Una wanafunzi 4,000 kwenye shule moja, hawa wote wanatarajia kwenda kidato cha kwanza, hawa wote wanatarajia kwenda kwenye elimu nyoofu, tunahitaji na wengine waingie kwenye michezo waweze kujijiri. Hatuwezi kufanana wote tukawa wataalam, wapo wengine wanaweza kuwa sehemu ya michezo, na tumeona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Wizara ya Michezo, imefanya kazi nzuri sana. Vijana wetu wamefanya vizuri sana, wa kike na wa kiume. Sasa mpango huu hasa kwenye eneo la mitaala, lazima kuanzia shule ya msingi tuanze na utaratibu wa kuanzisha michezo na michezo hii tuajiri walimu wa michezo.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu walimu tumewakabidhi kujumu zito sana, jukumu ambalo ni la kimaadili. Mbali na kufundisha, ndiye ambaye anakaa muda mrefu na mtoto, na huyu mwalimu kwa kiasi kikubwa anaweza kuathirika kisaikolojia kwa sababu anahangaika na kundi kubwa la Watoto, lakini ukishakuwa na michezo, tayari unaweza ku-*manage* hili eneo la maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuiomba Serikali, suala la walimu la kwanza ni ajira, lazima tuongeze ajira ya walimu. Jambo la pili ni motisha kwa walimu. Kazi kubwa wanayoifanya pamoja na kujenga madarasa na vitu vingine, wanafunzi ni wengi mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ambalo tumelizungumza kwenye elimu, tumezungumza udhibiti ubora wa elimu. Hii ndiyo ngao kubwa. Hawa ndio wanaokagua ubora wa elimu yetu. Tukizungumzia elimu bora, ni hawa wadhibiti ubora wa elimu, lakini humu tulichozungumza tumesema kuimarisha mifumo. Mifumo ni jambo kubwa sana, lakini nataka kuishauri Serikali, tuimarishe mifumo ya *online*, yaani mifumo ya mtandao ili unapotaka kujua taarifa za udhibiti ubora kwenye shule yako, maana yake ni rahisi tu kuingia kwenye mtandao na kujua taarifa ya shule badala tu yakuzungumza mfumo. Mfumo unaweza ukawa umetufunga, nasi tutashindwa ku-access vizuri, lakini ukizungumzia mfumo wa mtandao (*online*) utakuwa umetusaidia ku-access vizuri maendeleo ya shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wadhibiti ubora, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Haya mazingira magumu ndiyo yanaweza kusababisha tusipate

9 NOVEMBA, 2022

takwimu nzuri ya kuzungumzia *quality education* kwenye nchi yetu. Jambo kubwa ambalo naiomba Serikali, fedha inayotoka Hazina badala ya kwenda TAMISEMI, iende shuleni, hii fedha itoke moja kwa moja iende kwenye Wilaya zao. Wadhibiti ubora wana ofisi kwenye kila Wilaya, fedha yao iende kule ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi mzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huo huo, ipo miradi inakuja mingi sana na miradi hii inafadhiliwa na *World Bank*, kwa mfano *TACTIC*. Mradi wa *TACTIC* una *component* kubwa. Una masoko, barabara, na kadhalika. Singida ni sehemu katika miji 45; tangu mradi umekuja, tumebaki kupiga danadana, lakini mradi huu ndiyo suluhu ya matatizo yetu, ndiyo utatusaidia kuongeza kipato katika kukusanya mapato na utasaidia kuongeza ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuiomba Serikali, tunapoweka Mpango wa Maendeleo, uendane na miradi mikubwa ambayo inaleta tija kwenye jamii. Hatuwezi kuishia kuzungumza tu, tuna mradi *TACTIC*, Miji 45, inabaki kuwa ni hadithi. Tufike mahali miradi hii ikija ndiyo miradi tunatakiwa tuisimamie ili ituwezeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida pale tuna uwanja mzuri wa Ndege, na sasa tunafahamu; nami nimekuwa nikiuliza swali mara nyingi, lakini bado majibu yanakuja yale yale. Kwenye Mpango huu hatujazungumza habari ya kuboresha viwanja vya ndege kikiwemo kiwanja cha Singida. Singida ni Mji unaokua, tuna bidhaa nyingi, mazao ukizungumza hapa mpaka kesho asubuhi na mikoa mingine hawana. Sisi tuna karanga, tuna alizeti, tuna samli, tuna kila kitu. Naiomba Serikali iweke mpango endelevu wa

9 NOVEMBA, 2022

kukarabati viwanja vya ndege kikiwemo kiwanja cha Singida, na hili jambo litatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna suala la *renewable energy*. Tuna umeme wa upepo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pili.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana...

MWENYEKITI: Na hupati huruma, kaa chini. *(Kicheko)*

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stella, mjiandae Mheshimiwa Jesca na Mheshimiwa Londo.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika mpango huu na hasa katika mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea mbele sana, kuna wakati ni vyema tukaenda sawa na Watanzania na tukatoa ufafanuzi mzuri ili Watanzania wakatuelewa, hasa tunaposema uchumi wa Tanzania umekua, tuwe tunawafafanulia wananchi, huo uchumi umekua kwa namna gani? Kwa sababu uhalisia wa kile tunachokisema

9 NOVEMBA, 2022

na ukienda kwa hali za Watanzania huko uraiani, ni mbaya kila kunapoitwa leo, zinazidi kuwa mbaya. Kwa hiyo, Watanzania hawaelewi wanaposikia uchumi umekua, wanajiuliza huo uchumi unakua kwa namna gani? Kwenye makaratasi au mifukoni kwao? Kwa hiyo, kuna wakati tuwe tunawafafanulia Watanzania ili wawe wanaelewa maana halisi ya uchumi kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda huko uraiani, sasa hivi hata Mtanzania aliyekuwa ana uwezo wa kula milo mitatu, sasa hivi hata kula mlo mmoja ni shida. Hali ni mbaya, biashara haziendi, hali siyo nzuri kiukweli. Kama Taifa, lazima tufike mahali tuwafafanulie Watanzania huo uchumi tunaosema umekua, ni kwa namna gani, ili tuwe tunaenda sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la nishati, hasa katika mpango huu. Katika mpango huu nataka kujua Mpango hasa wa Taifa ni upi katika suala zima la kukabiliana na changamoto kubwa ya umeme ambayo ipo huko mikoani kwetu? Naweza nikasema hata wa Mikoa kama Dodoma na maeneo mengine wanaweza wasinielewe, lakini uhalisia sisi tunaujua wananchi wa Mikoa ya Mbeya na Songwe, hali ya nishati ya umeme ni mbaya sana na kwa wakati mwingine unaua mpaka uchumi wa Wana-Songwe. Sasa katika kufuatilia mpango sijaona kabisa kwamba Wizara ina mkakati gani wa kukabiliana na changamoto kubwa hii ya umeme ambayo imekuwa ni shida kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia mpango, ni vyema tukaja na mikakati, lakini ukisoma katika ule ukurasa wa 122 kipengele (f), utaona wanasema, “kuongeza

9 NOVEMBA, 2022

uzalishaji wa umeme kutoka vyanzo mbalimbali, kujenga na kukarabati miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Hizi ni sababu za kawaida ambazo hata mtoto mdogo huko Songwe anazijua. Sisi Wanasongwe tunataka mkakati, kwa sababu kiukweli umeme umechangia kuzorotesha uchumi wa Wanasongwe isivyokuwa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Songwe tulianza mgao kabla ya mgao. Suala la kukatika umeme Songwe ni hali ya kawaida mpaka masaa 24 umeme hakuna. Uchumi wa Wanasongwe unakufa. Wananchi wadogo wadogo ambao wamejiwekeza wanashindwa kuendeleza maisha yao kwa sababu tu yakukosa umeme. Hivi tunawaweka kwenye kundi gani hawa wananchi wa Mkoa wa Songwe? Tunaua uchumi wa Wanasongwe. Hasa ukizingatia tunavyozungumzia Mkoa wa Songwe, ule Mkoa ni langu kuu la SADC; Mataifa mengi yanaingia kwa kupitia Mkoa wa Songwe hasa Mji wa Tunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria unaenda katika lango la SADC masaa 24 Mji ni giza. Hebu fikiria! Tunaposema Tunduma ama Songwe ni lango, tunamaanisha. Mwananchi yeyote au mgeni yeyote anapoingia kupitia mpaka wa Tunduma, anapofika Tunduma, tafsiri yake ile, ndiyo anaiona sura halisi ya Tanzania. Sasa kama sura halisi ya Tanzania ina uwezo wa kukaa giza masaa 24, tunaeneza picha gani kwa wageni ambao wanaingia katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haikai sawa. Kuna wakati najiuliza, hivi Serikali inapotuambia kwamba ina uwezo wakuzalisha umeme na kuuza nchi nyingine, inamaanisha

9 NOVEMBA, 2022

nini? Au tunawadanganya Watanzania! Kwa sababu huwezi kuzalisha umeme ambao una uwezo wa kwenda kuuza kwenye Mataifa mengine ikiwa watoto wako ndani tu umeme hauwatoshi. Hii tunamaanisha nini? Tuache kuwadanganya Watanzania. Tuongeele uhalisia, tatizo ni nini ambalo linapelekea umeme kukosekana kila kunapoitwa leo? Vingine tujiulize, kwamba Dodoma na Songwe imekuwaje? Hii si ni Tanzania moja! Mbeya na Dodoma si ni Tanzania moja! Sasa inakuwaje? Kwamba tumewaweka wananchi kwenye mataba! *(Makofi)*

Mheshimniwa Mwenyekiti, ukienda leo Mkoa wa Songwe kilio kikubwa cha wananchi ni umeme.

MBUNGE FULANI: Aaah!

MHE. STELLA S. FIYAO: Hawana amani, wananchi wanashindwa kuzalisha, wanashindwa kuendeleza biashara zao, wanashindwa kuendeleza viwanda kwa sababu ya umeme. Kwenye mpango huu nilitarajia Wizara, ituambie...

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji, kwamba huu mgao wa umeme ni nchi nzima, hata Nyang'hwale huwa tunakosa. Asiseme kwamba kuna ubaguzi na matabaka. Umeme mgao upo kwa nchi nzima.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa taarifa, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Stella, taarifa hiyo.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa ninaipokea kwa mikono miwili. Shida wanayokutana nayo wananchi wa huko Nyang'hwale, ndiyo wanayokutana nayo wananchi wa Mkoa wa Songwe kwenye lango kuu la SADC, ni ajabu. Tufike mahali tuambiane ukweli hapa. Wananchi huko hawatuelewi. Tuambieni kwa nini mnatuletea taarifa tofauti, kama tuna uwezo wa kuzalisha umeme wa kuuza nje ya nchi, kwanini ndani usitutoshe? Hii ina maana gani? Ina maana gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali za wananchi wetu ni mbaya, mbaya sana, tunaua uchumi wa Wanasongwe. Hatuwezi kuvumilia kuona hiki kitu kinaeandelea, lakini wakati huo kwenye mpango hatuoni ukija na mikakati madhubuti ya kukabiliana na hili tatizo la umeme. Ili tuende sawa, ni vyema Wizara ya Fedha ikatuletea mpango madhubuti wa kukabiliana na changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia viwanda. Hivi kiwanda kipi kinaweza kuendeshwa bila umeme? Kipi hicho kiwanda? Kiwanda kipi? Labda kama tutatumia *generator* na *solar* tuambiane hapa, lakini kama tunategemea huu umeme; ndiyo maana kuna wakati wananchi wanahoji kwamba hata hiyo reli ya SGR, hivi itategemea huu huu umeme uu kuna umeme mwingine? *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali tuambiane ukweli, na tuombe Wizara ya Fedha ije na mpango madhubuti ni namna gani imejipanga kukabiliana na changamoto kubwa ya umeme ndani ya Taifa letu? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca, halafu Mheshimiwa Londo ajiandae, na baada ya Mheshimiwa Londo atafuatia Mheshimiwa Bilakwate.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango duniani ni mpango kama ilivyo mipango yote na ina sifa zake. Tumeletewa mpango na tumeusoma na taarifa yake na jinsi ulivyo. Mpango huu una chanzo chake ambacho ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi; na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni mkataba kati ya Watanzania na Serikali wanayoenda kuiunda na mambo ambayo wanategemea kwamba Serikali itakwenda kuwafanyia. Serikali ni Mkandarasi ambaye amepewa tenda na CCM kutekeleza yale ambayo iliahidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mipango iweze kutekelezwa lazima kuwe na malengo. Malengo tumejiwekea na tunayaona yapo kwenye mpango, lakini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inatambua kabisa kwamba, Mpango huu ndio unakwenda kutekelezwa katika ule Mpango wa Miaka Mitano ambayo tumeupitisha, ambao ndio unakwenda kutimiza dira ya maendeleo ya Taifa ambao tumeanza kutekeleza tangu mwaka 2000 mpaka 2025.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, ninachoona shida kwenye Mpango wetu ile kutokuwa unasomana na ule Mpango Mkuu wa Miaka Mitano kwa sababu malengo yake kama tunasema kwamba, mpango wote unatakiwa kuwa na malengo yanayopimika, yanayokuwa na muda maalum, yanayoweza kufikika, maana yake kuna sifa za malengo. Mpango huu kuna mambo ambayo ukiangalia katika miradi yetu ya maendeleo tumeweka malengo kwamba tutakuwa na miradi ya maendeleo ambayo itakwenda kuchochea ukuaji wa uchumi ambayo ni ujenzi labda wa barabara. Barabara hizi zinakwenda kufungua fursa za kukua kwa uchumi, halafu barabara zile hazijawekewa muda lini zinakwenda kukamilika. Maana yake ni kwamba, yale malengo hayasaidii mpango huu wa muda mfupi kufikia mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuna barabara inajengwa kuanzia Itono – Ludewa kwenda Manda, kilometa 211. Serikali inasema barabara hii imeanza ujenzi na ujue tupo kwenye utekelezaji wa Mpango huu wa Miaka Mitano, maana yake tuko mwaka wa tatu. Tumeanza ujenzi wa kilometa 50 kuanzia Lusitu mpaka Mawengi na umekamilika kwa asilimia 95. Sasa swali langu ni hili hapa, huyu mkandarasi kapewa kazi ya kujenga barabara hii kwenye Ilani ya CCM yenye urefu wa kilometa 211. Anatupa kukamilika kwa kipisi cha kilometa 50 kwa asilimia 95 ina maana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo hajatuambia hizi asilimia 161 zinazobaki atakamilisha katika hii miaka miwili iliyobaki. Hapa ndipo kunakuwa na tatizo la mpango na tusipowekana sawa maana yake ni kwamba, tutakuwa

9 NOVEMBA, 2022

tunaweka hii mipango halafu haitimii. Sasa tumeshamaliza dira ya maendeleo ya miaka 25 na Serikali ya CCM inaitambua hiyo na imeeleza kwenye ilani kwamba, itaisimamia Serikali yake kuhakikisha inaandaa mpango mwingine wa dira ya miaka mingine 25, maana yake itakwenda mpaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najaribu kuuliza kama hatutawekeana malengo kwamba, ninyi mwaka huu mkiingia katika hii barabara jengeni kilometa 40, mwaka unaofuata tutajenga kilometa 42, mwaka unaofuata tutajenga kilometa 42, mpaka miaka mitano tufikishe zile kilometa 211 hii mipango yetu tutakuwa tunafikiaje? Kama watu watakuja tu ofisini, sisi tumejenga kwa asilimia 95 kilometa 50, ndizo ulizotumwa? Wewe umetumwa kutengeneza kilometa 211, tuambie hiyo asilimia uliyojenga katika hiyo kilometa 211, usituambie katika hizo ulizoamua wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sawa na unakwenda kumkagua mkandarasi mradi, halafu anakwambia nimekamilisha kwa asilimia 90 kipande hiki, wakati wewe unajua kipande kile ni kidogo sicho ulichompa. Kwa hiyo, tunataka mpango unaokuja sasa uwe una *time* ya kutuhakikishia kwamba, hizi barabara tunazosema zinafungua uchumi wa Taifa letu katika miaka mitano zinaishaje? Kwa mwaka wa kwanza zinajengwa kilometa ngapi, ngapi, kwa miaka inayofuata mpaka tutakapofikia kwenye zile ambazo tunajua kabisa kwamba, ndani ya miaka mitano tutakuwa tumekamilisha ile barabara yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea kujenga hizi barabara kwa kilometa moja, kilometa mbili,

9 NOVEMBA, 2022

tunafungua uchumi. Kwa mfano, barabara ya Iringa MR mpaka Itunundu kilometa 70, kila siku wanajenga kilometa moja moja miaka 70 watakua lini kwenda kwenye uchumi wa kukua kwa asilimia nane na watu watakuwa *answerable* vipi? Yaani unamuulizaje mtu kwamba, wewe Wizara yako ya Uchukuzi imefanya kazi nzuri kama hukumwekea lengo kwamba, lazima barabara hizi zinazofungua uchumi ujenge kwa asilimia 40 au 50?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndio kwenye shida ya mpango. Kwa hiyo, mipango tunayokuja nayo huku mbele ifanyiwe mapinduzi tuambiwe barabara hii uliyosema unaijenga kwa miaka mitano umejenga kilometa ngapi? Nimejenga kilometa 150; hizi zilizobaki unamaliza ndani ya hii miaka miwili iliyobaki na kama hujamaliza kwa nini? Hapo ndipo tutakuwa tunakwenda sawa na mipango mingine yote duniani, lakini tukienda hivi itakuwa kama ile michezo ya kuchezea vile viberiti chekundu cheusi, chekundu cheusi, kila mtu atakuja atatuambia hapa sisi tumejenga kilometa mbili kwa asilimia 90. Kilometa mbili kwa asilimia 90 *out of* kilometa ngapi? Haya ndio maswali ya kujiuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kikubwa ambacho kipo kwenye huu Mpango; pamoja na kwamba tunakusanya fedha, udhibiti wa fedha zetu umeendelea kuwa *weak*. Tumeelekeza sana kelele nyingi kwamba, Serikali za Mitaa ndiko fedha nyingi zinakopotea, lakini iko miradi hapa ambayo imewekwa na Wabunge wengine wameisema na yenyewe inapoteza tu fedha za Serikali, haina tija. Katika karne hii kuipatia taasisi fedha, unaipatia taasisi fedha bilioni moja, inakwenda kufanya ubunifu na ndio wanasema inakwenda kuwa ni kitivo cha kubuni zana za kilimo vijijini kama CARMATEC, unaipatia bilioni moja,

9 NOVEMBA, 2022

inakuja imekutengenezea mikokoteni ya kuvutwa na ng'ombe nane. Imetengeneza sijui mashine za kubangua korosho mbili, huu ni utani wa uwekezaji kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao tunatumia gharama kubwa tumewekeza, tunawafundisha, tunawapa mafunzo, *especially* vijana. Tunawapeleka katika majeshi, kwa mfano JKT, wanafanya kazi kubwa sana ya kuwafundisha wale vijana uzalishaji mali, uhodari, ushujaa na wale wanaweza kufanya kazi popote. Wao JKT lengo lao la kuanzisha si kwamba kutoa ajira kwa vijana, lakini sisi Serikali ya CCM imetutuma kuandaa ajira milioni nane. Hawa vijana wanaangaliwa vipi? Wanaachwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamwachaje mtu ambaye umesham-*train* anaweza kufanya kazi, anaweza kulima, anaweza kutengeneza, anaweza kupambana na mazingira ya Kitanzania, kulala popote akaweza kulima, akafanya nini, ukamuacha kama kijana wako, kama nguvukazi, kumwendeleza na wakati umeshatumia gharama kubwa ya uwekezaji kwake. *The same applies* tunafanya kwa watu tunaowasomesha, tunafanya kwa vijana ambao wanamaliza vyuo vikuu, hatuna mpango kabambe kwamba, vijana wamemaliza, hawa wana elimu hii, vijana hawa wamemaliza *SUA* wana elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunahangaika mpaka vijijini; China waliamua kwa pamoja wakasema sasa tunachukua vijana milioni tano, tunawapeleka vijijini na wengine tutawapeleka nje ya dunia wakajifunze namna ya kufanya kazi. Hawa nao waende vijijini kule, wakakae na wanakijiji, waangalie wanafanya nini, halafu watupatie njia mbadala za kufanya mambo wanayofanya kisasa zaidi. Sisi

9 NOVEMBA, 2022

tuna mpango gani kwa vijana wetu na hizi milioni nane? Hizi ajira milioni nane tulizopewa na chama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu na rasilimali vitu hatuweki vizuri. Leo tuna LNG, mradi wa gesi, taarifa imekuja hapa kwamba, mradi ule wa gesi tumejenga barabara kuzungushia eneo lile, ndio kazi zilizofikiwa kwa bilioni nne karibu na. Tumezungushia barabara kwenye ule mradi, halafu mambo mengine yaliyofanyika kwenye mradi ule tunaendelea na utafiti wa kisayansi, tunaendelea na utafiti wa kuweka mipango, sasa kipi kinaanza kati ya kuku na yai? Unaanzaje kujenga barabara na kuzungushia eneo ambalo bado unaendelea kufanyia utafiti wa kisayansi, hujajua kwamba, utatakiwa uweke mitambo ya kiasi gani? Kwenye hizo barabara hiyo mitambo itapita au haitapita?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Kengele ya pili.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba Mheshimiwa Waziri akija hii miradi mingine ambayo haina tija aitoa na taasisi ambazo zinachukua hela hazina tija zitolewe. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Bllakwate na wajiandae Mheshimiwa Njeza na Mheshimiwa Nolo.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango wetu ambao uko hapa mezani. Kwanza niishukuru Serikali yetu

9 NOVEMBA, 2022

kwa kazi kubwa ambayo inaifanya chini ya Rais wetu, mama yetu Samia Suluhu Hassan. Pia nimshukuru Spika wetu, dada yetu Mheshimiwa Tulia Ackson na wewe mwenyewe msaidizi wake kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu. Tumepata wakati wa kutosha wa kuchangia Mpango huu ambao naamini kabisa mchango wa Wabunge unaenda kuakisi katika ule Mpango Mkuu ambao utawasilishwa hapa kwenye Bunge la Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida kwetu kuchangia huu Mpango wa Miaka Mitano na sasa tuko kwenye Mpango wa Tatu. Bado sijaona ni kwa jinsi gani maoni ya Wabunge ambao tunajadili hapa yanaakisi katika mipango hiyo. Nilipenda sana kuona Mpango unapowasilishwa uelezee waziwazi ukiainisha mchango wa Wabunge umechukuliwa kwa kiasi gani katika bajeti, lakini pia katika utekelezaji wa Mpango huu ambao unawasilishwa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuna maendeleo chanya, ukuaji chanya katika uchumi wetu. Kwa mfano, ongezeko la asilimia 5.4 katika mwaka 2021, kwa sasa hivi tumeenda zaidi ya ongezeko la asilimia 5.5. Hii ni *indication* nzuri kwetu, lakini tunaona kabisa ongezeko hili limetokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika maeneo ya maji safi na taka, ambao ongezeko lake ni asilimia 11.9, fedha bima asilimia 10, uchimbaji wa madini na mawe asilimia 8.5, huduma za jamii asilimia 8.5 na umeme asilimia 8.3. Tunaona kabisa hapa maeneo yote haya ambayo yametajwa yanagusa sekta binafsi ambazo katika Mpango Mkuu wa Miaka Mitano, sekta binafsi ilikuwa inatarajiwa kuchangia uchumi wa Taifa kwa takribani trilioni 9.8 na kati ya hizo trilioni 5.1 zilikuwa zinategemewa kuzalishwa na

9 NOVEMBA, 2022

sekta binafsi za ndani wakati hicho kiwango kilichobakia kuchangiwa na sekta binafsi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa umakini ushirikishwaji wa sekta binafsi kwetu bado ni changamoto. Kwanza kabisa inaanza na *definition* ya sekta binafsi, sekta binafsi ni nini? Kwa sababu, inavyoonekana na jinsi tunavyoichukulia kiwepesi tunaona kabisa kwamba, sekta binafsi ni taasisi za watu binafsi ambazo hazina mahusiano na Serikali, lakini wenzetu walishaondoka huko, sekta binafsi ina mahusiano chanya na Serikali na sekta za umma. Sekta ya umma haiwezi kuendelea bila ya mahusiano chanya na sekta binafsi. Ndio maana wakati wenzetu wanajitahidi *ku-out source* kila kitu kushirikisha sekta binafsi, sisi tunakimbilia *Force Account* katika kila kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale Watanzania ambao walipata kufanya kazi nje wanafahamu. Kule wenzetu mpaka simu ya kampuni ambayo unatumia imekodishwa kutoka kwenye kampuni binafsi, *computer* unayotumia imekodishwa kutoka kwenye kampuni binafsi, *photocopy* ambayo unachapisha imekodishwa kutoka kampuni binafsi. Hivyo ndivyo wanavyoshirikisha sekta binafsi katika ukuaji wa Serikali, katika biashara za Serikali na ndivyo wanavyotengeneza matajiri wa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kila kitu tunaenda kwenye *Force Account*. Sina hakika tutaishia wapi, lakini nina hakika kwamba, kama tunaweza tukafanya *research* kuna maeneo ambayo tunaweza kabisa kuona tumeshindwa. Wakati umefika sasa kuangalia ni jinsi gani tuna-engage watu wetu katika uchumi mpana wa nchi yetu katika

9 NOVEMBA, 2022

kuwashirikisha aidha, moja kwa moja ama kupitia shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la sekta binafsi unaweza kuona kwamba, hata mikopo ambayo imetolewa kwa sekta binafsi, pamoja na kwamba, imeongezeka kutoka trilioni 20.6 mwaka 2021 mpaka trilioni 24.5 mpaka Juni, 2022, lakini tujiulize mikopo hiyo imekwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi kikubwa cha fedha ambazo zimekopeshwa sekta binafsi, asilimia 38 zimeenda kwenye shughuli binafsi. Unaposikia shughuli binafsi unashindwa kuelewa ni zipi katika uzalishaji. Hakuna kitu kinachoitwa shughuli binafsi katika uzalishaji. Asilimia 16 imeenda kwenye shughuli za kibiashara, asilimia 10.7 zimeenda kwenye viwanda, lakini ukienda kuangalia riba *on average* unakuta riba ni asilimia 16.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wa kisasa katika dunia hii ambayo tunaishi huwezi ukaenda kumlipisha riba mwananchi wako ya asilimia 16, ukategemea kwamba, inaenda kuchochea uchumi. Huwezi kwenda kumtoza riba mjasiriamali kwa asilimia 16, ukategemea kwamba, anaenda kuwa *competent* katika dunia ambayo inakimbia sasa hivi kwenye *single digits*. Ndio maana wawekezaji wote ambao wanatoka nje wanafanya vizuri sana hapa Tanzania ukilinganisha na Watanzania kwa sababu, taasisi zetu za kifedha hazijatimiza wajibu wake wa kuhakikisha kwamba, zinamwezesha Mtanzania katika kuhimili mikikimikiki ya kiuchumi, ya kibiashara na yeye anakuwa *full participant* badala ya kuwa *subordinate* wa wageni. (Makofi)

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukweli kabisa, jukumu la kuwatengenezea mitaji wananchi ni la Serikali, ku-*facilitate* matajiri, kutengeneza matajiri ni la Serikali na jukumu hili hatuwezi kulikaimisha kwa watu. Tunatengenezaje mitaji? Kwa kuwapa mikopo ambayo ina nafuu, kuwatengenezea ruzuku, kutengeneza miundombinu ambayo unamwachia mwananchi nafasi ya kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sasa umefika wakati wa Bunge lako, hii michango ya Wabunge kuichukulia kikamilifu na umefika wakati wa kuanza kutafakari kuwa hata na Kamati ya Bunge ambayo kazi yake ni kufuatilia maazimio ya Bunge na utekelezaji wa Serikali. Tukifanya hivyo tutajua tumetoka wapi? Tuko wapi na tunaenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishindwa kufanya hivyo ndio utakuta kwamba, tunapanga bajeti ya mwaka huu ya fedha. Kwa mfano, pale Dumila kuna barabara imetengenezwa mpaka Kilosa, Kilosa pale tunaizungumzia Mikumi, kuna Kiduku pale ambacho hatujui lini kimeshaka kwenye bajeti ya Serikali zaidi ya miaka mitano na hivi tunavyozungumza ipo kwenye bajeti ya Serikali na hatujui lini itatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Mpango wa bajeti, tunazungumzia jinsi ya kutengeneza *framework* ambayo inaweza kwenda kusaidia kutengeneza fedha za Serikali kwa ajili ya kuhudumia jamii nyingine. Kuna uwekezaji mkubwa pale Ilovo, bilioni 571 zinaenda kuwekezwa pale Ilovo, lakini kuna SGR ambayo inapita Kilosa, lakini kuna reli ya TAZARA kutoka pale Kidatu kwenda Mlimba kwenda mpaka Zambia. Kipande cha reli kutoka

9 NOVEMBA, 2022

Kilosa kuja Ilovo kimekufa na sasa hivi tunawekeza bilioni 571 pale Ilovo lakini hakuna *mechanism* ya kusafirisha sukari tukikamilisha kile kiwanda kutoka Ilovo kuja Kilosa kuungana na SGR kupeleka nje ya nchi na mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili hatuhitaji mawazo ya wageni kuja kutuambia, linaonekana kwa macho, lakini hata ujenzi wa barabara ambayo itabeba bidhaa za sukari kutoka kwenye kiwanda hiki ambacho tunawekeza inahitaji kuingizwa kwenye mpango, sio tu kwa sababu, Mbunge amesema, lakini ni kwa sababu inaenda kwenye eneo la uzalishaji ambalo tunahitaji kwa ajili ya kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sasa inapaswa kujielekeza katika maeneo ya uzalishaji. Utalii Kusini ni jambo ambalo haliepukiki. Utalii kuunganisha Hifadhi ya Nyerere na Mikumi haliepukiki, kuna zaidi ya dola milioni 120 zimewekezwa pale, lakini ukiangalia nje ya zile hifadhi kuna uwekezaji gani ambao unaenda kulisimua wananchi kushiriki katika shughuli za kitalii, haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, kuna zile bilioni 260 za CSR ambazo zinatokana na Bwawa la Mwalimu Nyerere...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili sisi hatuna la kusema zaidi ya kusema *inna Lillah wa inna ilayhi raji'un*. Ahsante. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Mheshimiwa kengele ya pili ishagonga.

Mheshimiwa Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Njeza, wajiandae Mheshimiwa Nolo, Mheshimiwa Idriss Juma Abdulhafa. Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Salim Omar.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango wa Serikali 2022/23. Kwanza nipongeze kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais, kwa kweli ameonesha uwezo mkubwa kama Kiongozi wa Nchi, kila mmoja ni shahidi. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na timu yake kwa Mpango mzuri ambao wametuletea na leo tunaujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia ninalo swali kwa Mheshimiwa Waziri ambalo anaweza akatujibu wakati anahitimisha Mpango huu. Tumekuwa tukipitisha mipango, tumekuwa na Mpango Mkubwa wa Miaka Mitano, lakini leo hii tuna mpango wa mwaka mmoja ambao ni Mpango wa Tatu; swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, ni vizuri tukajiuliza mipango ambayo tumeipitisha hii miaka mitatu tumefanikiwa au bado hatujafanikiwa? Na kama hatujafanikiwa ni kitu gani ambacho tunatakiwa tukifanye ili Mpango huu tunaoujadili leo usije ukashindwa kama mipango mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipitisha mipango na tumekuwa na Mpango mkubwa wa miaka Mitano lakini leo hii tunao mpango wa mwaka Mmoja ambao ni mpango wa Tatu, swali langu kwa Mheshimiwa

9 NOVEMBA, 2022

Waziri ni vizuri tukajiuliza mipango ambayo tumeipitisha hii miaka Mitatu tumefanikiwa au hatujafanikiwa? kama hatujafanikiwa ni kitu gani tunachotakiwa tukifanye ili mpango huu leo tunaoujadili usije ukashindwa kama mipango mingine? Ninaamini hili ninalosema kila Mbunge analo jibu, kwa kweli kwa sehemu kubwa bado hatujafanikiwa kile ambacho tumekipitisha kwenye mpango uliopita. Kwa hiyo, Mheshimwa Waziri hilo ni suala ambalo naomba utujibu kama Wabunge kwa sababu tusiwe tunapitisha mipango mizuri, Wabunge wanatoa ushauri mzuri lakini mwisho wa siku majibu yanayotoka ni asilimia Thelathini, Hamsini hatufiki hata asilimia Sabini Tano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nipongeze sana Serikali, tumesoma kwenye mpango kwa habari ya SGR, SGR ni mradi mzuri sana kwa Taifa kwa sababu umeeleza unavyoenda kuunganisha nchi ya DRC na huko ndiko kwenye biashara kubwa. Ushauri wangu ni kwamba, ili SGR iwe na faida kubwa ni lazima tuwe na mzigo wa kutosha, hatuwezi tukajenga SGR Iwa mabilioni halafu hatuna mzigo ambao tutaweza kuupitisha na kurudisha fedha hii ambayo tumekopa. Ili tuweze kuwa na mzigo wa kutosha wakati tunaendelea na mpango wa kujenga kufika kwenye hizo nchi ni lazima tuje na mkakati wa kuboresha bandari yetu. Bandari yetu ya Dar Es Salaam ndiyo tunayoitegemea kwa sehemu kubwa ili tupate mzigo ambao tutapitisha kupeleka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kwa upande wa bandari, pamoja na uboreshaji unaoendelea bandari ya Dar es Salaam imezidiwa. Bandari ya Dar es Salaam hatuna eneo lingine ambalo tunaweza tukapanua na kuwa na

9 NOVEMBA, 2022

Bandari kubwa, lazima tuje na mpango kabambe wa kuhakikisha tunajenga Bandari ya Bagamoyo. Bagamoyo ndiyo Bandari muhimu itakayoenda kuinua uchumi wa nchi hii. Mimi naamini tukiwa *serious* tukakubali kukaa kwenye meza tukapanga mipango mizuri na tukaisimamia Bandari ya Bagamoyo itainua Taifa hili. Kwa hiyo niombe sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujenga Bandari ya Bagamoyo lazima tuongeze ufanisi, ni lazima wakati tunaboresha Bandari yetu ya Dar es Salaam tuangalie hawa washindani wetu ambao kwetu Mungu ametujalia, tunayo mazingira mazuri, tumezungukwa na nchi nyingi majirani, ni kitu gani kinachosababisha wengine wakimbilie Mombasa wengine wakimbilie kwenye nchi nyingine ambako ni mzunguko mkubwa kupeleka mizigo kwenye nchi zao? Hivyo ni lazima tuingie kwenye ushindani na biashara ni ushindani, lazima unapofanya biashara uangalie mwenzako ameboresha wapi ili na wewe uweze kufanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, niombe sana hilo tuliangalie kwa ajili ya kuboresha Bandari ya Dar es Salaam ili SGR isije ikawa ni mzigo umekaa tu, kwa sababu kama SGR tunategemea kupeleka abiria tu hakuna chochote ambacho tutafanikiwa, Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri hili mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee kilimo, kilimo ni biashara, kilimo ni maisha na kilimo ni uchumi. Mungu ameijalia nchi hii mpaka wakati mwingine huwa najiuliza hivi kweli tunaona hii fursa ambayo Mungu ametupatia na tunaitumia ilivyo? Ukiangalia nchi hii imejaliwa vipindi virefu vya mvua, pamoja na mvua bado tunayo maji ya kutosha kwenye maziwa na kwenye mito,

9 NOVEMBA, 2022

hizi fursa na hii neema ambayo Mungu ametupa tunaitumiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea COVID, imetokea vita ya Urusi na Ukraine kule hii fursa tumeitumiaje? Tungekuja na mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji, tukatenga Kanda. Nimpongeze Mheshimiwa Bashe kule kwetu ameanza na mazao haya ya kimkakati kuanza kuzalisha miche, lakini lazima tutenge kikanda, tuseme Kanda hii itazalisha mpunga, Kanda hii ni korosho na Kanda hii ni mahindi halafu haya mazao tunayoyapata ndiyo tuende kuyauza kwa majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, Kyerwa peke yake tunailisha Uganda ndizi, yaani ni foleni ndizi iliyokuwa inauzwa shilingi 3,000 leo ni 20,000! Sasa hizi fursa lazima tuziangalie na tuzifanyie kazi, siyo kila siku kinakuja hiki kinaisha, kinakuja hiki hakiishi tunakatia katikati tunakwenda. Kwa hiyo, niombe sana tutumie fursa hii ili tuweze kuboresha kilimo chetu kiwe na tija lakini ili tuwe na kilimo ambacho ni kizuri lazima wakulima hawa tuwaboresha mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeeleza kwenye mpango kuhusu kuboresha barabara zetu za TARURA, ni kweli barabara zimeanza kuboreshwa lakini bado lazima tujue wakulima wengi wako vijijini, unaongelea barabara 25,000 ambazo Serikali tayari imeshaziboresha. Sehemu kubwa barabara nyingi Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi ni za udongo. Serikali iwekeze kwenye barabara za changarawe ili hawa wananchi ambao ni wazalishaji wakubwa waweze kupeleka mazao yao sokoni na mazao yao yanapokwenda sokoni Serikali inaongeza kipato. Kwa

9 NOVEMBA, 2022

hiyo, ninaiomba sana Serikali kwenye mpango huu ili tuboreshe kilimo tunahitaji barabara nzuri, tunahitaji mazingira mazuri kwa wakulima wetu na ili tuboreshe kilimo kiwe kizuri na tuweze kupata kipato ni lazima tuwe na soko la uhakika. Kwa hiyo ninaomba sana Serikali ilianganalie jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilisemee, tunalo janga la Kitaifa sijui wenzangu mnaliona, mabadiliko ya tabianchi lakini pia na uharibifu unaoendelea tunaoufanya sisi kwa kuharibu vyanzo vya maji, kukata miti na kuchoma mkaa, nchi hii inaenda kuwa jangwa. Serikali lazima ije na mpango kwa kila Halmashauri kuzalisha miti na kuigawa kwa wananchi ili tuende kuboresha yale mazingira ambayo yameharibika vinginevyo tunakoelekea hali ni mbaya. Ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Njeza, ajiandae Mheshimiwa Nollo, Mheshimiwa Idrissa, Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Salim Omar.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata na mimi fursa ya kuchangia katika mapendekezo ya mpango wetu huu. Nianze kwa kuwapa pole wananchi wa Mbeya kwa ajali mbaya ya gari ambayo imetokea kwenye Mlima Iwambi mteremko wa kwenda Mbalizi, ambayo imesababisha vifo ikiwemo familia ya Katibu wa BAKWATA wa Mkoa, lakini hayo ni matokeo ya utekelezaji wa shughuli ambao unachelewa. Hilo eneo ilikuwa barabara ipanuliwe lakini mpaka leo haijapanuliwa. Kwa hiyo, tunapojadili hii mipango tuangilie vilevile athari

9 NOVEMBA, 2022

zinazotokea kutokana na kucheleweshwa kwa utekelezaji wa hii mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwape pole wananchi wa Kagera na Watanzania kwa ujumla kwa ajali ya *Precision Air* ambayo imetokea na kupoteza Watanzania wenzetu. Pia ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa utekelezaji wa Ilani. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa vizuri, maeneo mengi ukiangalia hata miradi ya kimkakati kwa kweli imeibadilisha nchi yetu kwa kiasi kibwa. Naweza kusema hata *brand* ya Tanzania kwa kweli imebadilika kwa kiasi kikubwa. Hata wageni wanapokuja tumeshuhudia wageni wanatoka nchi mbalimbali hata Wabunge kutoka Mataifa mengine wamekuwa wakisifia wanavyoiona Tanzania inavyobadilika kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo ukiangalia huu mpango wetu kwa kweli mapendekezo ni mazuri lakini yamekaa kinadharia mno. Ukiangalia uhalisia haupo kwa sababu haielezi ya kwamba tutajipima vipi? Dhima ya mpango ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu, hiyo dhima ibebeba vyote hivyo lakini ukianza kuangalia huu mpango huoni sisi ya kwamba je tumeji *position* vipi kwenye ushindani kwenye Ukanda huu wa *East Africa*, kwenye ukanda wa *SADC* na kidunia, na hiyo ndiyo inatakiwa mpango ukae namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kama walivyosema wenzangu kuna upungufu mkubwa wa *governance structure* ya Wizara ya Fedha, ni bora ikarudishwa Tume ya Mipango ili iwe nje ya Wizara ya Fedha iweze ku *coordinate* Wizara zote, ili mipango ya Wizara zote iweze kupitia sehemu moja. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia leo sidhani kama kuna *coordination* ya aina hiyo, inawezekana kama ipo lakini haionekani na bila kuwa na hiyo na bila kurudisha ile *BRN (Big Results Now)*, kwa kweli tutakuwa tunapanga mipango hapa na hakuna anayeifuatilia na hatujui ni nini kinachotokea. Tutampa wakati mgumu sana Mheshimiwa Rais kujua Serikali yake ina *perform* vipi, hata Chama cha Mapinduzi kurudi kwa wananchi nachi itakuwa ni kazi kubwa mno. Nayasema haya, tumekuwa tukizungumzia *monitoring and evaluation* kwa muda mrefu iko wapi? Bila kuangalia nini tulichokipanga na tunafanya nini inatuletea changamoto kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tunazungumzia Deni la Taifa, tunasema Deni la taifa ni himilivu, kwa kiasi kikubwa utazungumza ndiyo kwa kuwaambia watu kwamba Deni la Taifa ni himilivu, kwa sababu hata *modes* naye kasema ni *positive* kwa hiyo ametu-*evaluate* vizuri. Lakini ukiangalia kwenye ripoti hii ya leo ule ukomo wa deni ukilinganisha na mauzo ya nje tumefikia kwenye mstari wa njano tunaenda kwenye mstari mwekundu. Maana yake nini? Maana yake ni nini? Ni kwamba tunakopa lakini uwezo wa kulipa hii mikopo ya kigeni inawezekana ikatushinda, sasa hili siyo jambo zuri kwa nchi yetu! Tilitaka tuone katika huu mpango *measures* gani umechukua ili ku-*address* hilo pesa za kigeni zipatikane nyingi ili nchi iweze kuendelea. Hizo fursa zipo lakini kwa sababu hatuna Tume ya Mipango hizo fursa huwezi kuziona. Kwa vile, mtu wa Madini fursa zipo anafanya yeye mwenyewe, mtu wa maliasili anafanya yeye mwenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata kwenye kilimo bajeti imeenda nzuri sana lakini je, Wizara ya Kilimo ndiyo

9 NOVEMBA, 2022

itaenda kulima? Hapana ni binafsi! Ile bajeti kubwa ungeiweka benki, watu wakaenda kuchukua mikopo wakajenga mabwawa badala ya Serikali kuanza kufanyakazi ambazo zinatakiwa zifanywe na sekta binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia yote hayo, Mheshimiwa Rais katoa Trilioni Moja zikakopeshe wakulima; Je, zimekwenda? hazijaenda Trilioni Moja! Kama kungekuwa na ubunifu, Je, kuna watu wabunifu hakuna! Ilitakiwa kuwe na watu wabunifu ya kwamba hii Trilioni Moja tuitumie namna gani na siyo ametoa fedha taslimu Hapana! Yeye inakuwa ni *window* ili watu waweze ku-access zile pesa ziende kwenye sekta ya kilimo tuweze kuzalisha na kilimo kitaibadilisha Tanzania kwa kiasi kikubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kwenye kilimo ni kwamba tungeondoa masoko kwenye Kilimo. Masoko ikiwezekana yakajitegemee tusichanganye uzalishaji na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii bei ya kahawa haiendi vizuri kwa sababu gani, kahawa Tanzania siyo kwamba tunashindana na Brazil Hapana! Bali kahawa ya kwetu tunashindana kwa ajili ya ubora wa kahawa ya Tanzania. Lakini ni nani amekwenda kuuza huo ubora? Hakuna! Kwa hiyo, mtu anaenda sokoni hajui atauza kwa kiasi gani. Wakulima walijaribu wasiende sokoni lakini bei ya kahawa inaendelea kuporomoka, hiyo maana yake nini? inapunguza uwezo wa Taifa kwenye pesa za Kigeni. (Makofi)

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana Bunge lako liielekeze Serikali iweze kutatua matatizo haya kwa haraka na haya matatizo yanaweza kutatuliwa kukiwa na *checks and balances* kwenye Wizara zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia suala la mikopo kwa watu binafsi. Makusanyo ya ndani kwa Halmashauri ni Bilioni 860, asilimia 10 ni Bilioni 86, hizo asilimia 10 ni kwa ajili ya kuwakopesha vijana na wakina mama, siyo pesa ndogo! Mtaji wa Benki ni Bilioni 15. Hizi pesa zingepelikwa kwa wataalam tukaangalia tukawasaidia wakina mama pamoja na vijana Tanzania inaweza kubadilika ndani ya miaka Mitatu na wewe ukashangaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bilioni 86 ni leo, mwaka kesho tena zipo zingine zitaenda kwenye hiyo Mfuko. Changanya na hiyo Mifuko mingine ambayo iko kwenye Wizara zingine, kwa kuwa Mkopo siyo kumpa mtu hela! Mkopo ni kumsaidia mtu aweze kuzalisha, mkopo ni kumsaidia mtu aondoke kwenye umaskini awe tajiri. Sasa hatuwezi kuwasaidia vijana wetu, wamekuwa wakichukua hizi fedha za mikopo lakini unakuta siku ya marejesho wanakimbia na sisi tunaotoka mipakani wengine wanakimbilia mpaka nchi jirani. Kwa hiyo, ningepomba hili lichukuliwe kwa uzito wake na tusianze mambo mapya wakati mambo mazuri yapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *innovation* haina maana uanze na kitu kipya. TAZARA inafanya nini! *Trillions of money* zimelala ardhini! TAZAMA *pipeline*, Tanzania ina asilimia 33 imelala inafanya nini! Magari yanaua watu wetu barabarani badala yake mafuta yangesukumwa yakaenda Nyanda za Juu Kusini, kukawa na *Dry Port* pale Mbeya

9 NOVEMBA, 2022

wakachukua mafuta kutoka hapo! Lakini unaweza kuyasafirisha hayo mafuta yakaenda mpaka Malawi na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na mtazamo wa namna hiyo ndiyo sababu ni bora tukawa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Njeza muda wako umekwisha,ahsante.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nollo, jiandae Mheshimiwa Idrissa Juma, jiandae Mheshimiwa Getere na jiandae Mheshimiwa Salim Omar.

MHE. KENNETH E. NOLLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mpango huu wa maendeleo wa mwaka mmoja. Awali ya yote nami niseme yapo mambo ambayo Serikali imeyaainisha inataka kufanya katika kipindi hiki cha mwaka mmoja lakini jambo kubwa ambalo tunalo pia ni tatizo ni katika hali ya usimamizi wa mipango yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue maneno aliyoyasema Profesa Kitila, lengo la mipango yetu iwe ni kuondoa umaskini. Jambo hili ukiliangalia, nimeisoma hotuba ya Waziri kwa kuirudia, nimesoma mpango wenyewe, unaona kabisa baadhi ya maeneo tunatoka

9 NOVEMBA, 2022

katika kuondoa umaskini. Umaskini kwa maana ya *the object poverty* bado hatujau-address vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijikite katika Mkoa wa Dodoma. Kwanza naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuhamia katika Mkoa wa Dodoma, Dodoma sasa imekuwa Jiji na Mji wa Dodoma unakua. Ukilinganisha maisha yaliyopo katika Jiji la Dodoma na nje ya Dodoma kwa maana ya Wilaya zake na wananchi wake bado kuna umaskini wenyewe ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nataka niseme, kuna Mheshimiwa Mbunge alisema bado sera zetu tunachanganya, Sera ya Mkoa wa Njombe ya Kilimo inakuwa sawa sawa na Mkoa wa Dodoma, Sera ya Mkoa wa Mbeya inakuwa sawa sawa na Mkoa wa Dodoma. Sera ya Kilimo ya maeneo ambayo mvua inanyesha sana inakuwa *the same treated* na Dodoma. Sisi tunasikia habari ya ruzuku ya mbolea, kwetu sisi hapa hakuna. Kwa hiyo, Ukiangalia maeneo ya Kanda ya Kati, hebu naiomba Serikali iunde sera mahususi kwa maeneo kame, iwe ni sera ya kilimo katika maeneo kame. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna umaskini mkubwa kwa sababu mvua hainyeshi. Mvua inanyesha mwezi wa kwanza, mwezi wa pili imekatika. Hata hivyo pamoja na mvua hii kunyeshi, maji yanayopatikana Dodoma kipindi cha mvua ni mengi. Sasa Serikali tengeni basi hata shilingi bilioni 200 au 500 mtuchimbie bwawa kubwa la uhakika la umwagiliaji. Ile Farqwa imepigwa danadana mpaka leo. Kwa hiyo, umaskini wetu sisi umekuwa mkubwa kwa sababu hatupati mvua ya kutosha.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Serikali hamlifanyi, inakuja falsafa ya Waziri wa Kilimo kwamba wanaanzisha *block farming*, zile ni vitone vidogo lakini kwa maana ya kuondoa umaskini katika Kanda ya Kati bado Serikali haijawekeza. Sisi mbegu hatuna, sasa hivi tunatafuta mbegu, ASA (Wakala wa Mbegu) hana mbegu ya kustahimili hapa Dodoma, hatuna. Kwa hiyo, mnavyoongea habari ya ruzuku ya mbolea sisi hapa hatuna ruzuku ya mbegu na hatuna mbegu yenyewe. Mlituletea alizeti mwaka jana yenyewe inarefuka mara tatu, yaani Dodoma bado inashida na Kanda ya Kati bado ina shida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema Mkoa wa Singida unalima alizeti, leteni kiwanda kikubwa cha shilingi bilioni 200 au bilioni 300 tuweze kuweka kiwanda cha maana pale, ili tuweze kuzalisha mafuta ya uhakika. Bado hatuja *address* mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliongea hili na nataka niseme, jana ulisema na si umwagiliaji ule ambao unakuja wa kukinga hivi vibwawa vya umwagiliaji vinavyotengenezwa, tunataka umwagiliaji wa matone. Tunataka tulazimishe kwamba kila mkulima awe na heka mbili za umwagiliaji wa mtama ili tuwe na uhakika wa chakula nyumbani. Maji yanatoka mengi niliwahi kusema kuanzia Kongwa shuka yote Mpwapwa ile, njoo kwetu Bahi tuna *swamp*, ina maji lakini nani wa kufanya utaratibu wa maji yale tuweze kuyatumia? Kwa hiyo, bado kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni katika ufugaji; nchi hii tumeamua kuchunga na sio kufuga, nchi za wenzetu Kusini mwa Afrika wale wanafuga, maana yalke

9 NOVEMBA, 2022

mchungaji anataka afuate ng'ombe zake zinakokwenda naye anaenda huko huko, zinampeleka Kusini, Mbeya anaenda huko huko, mashamba ya watu yeye anachunga humo humo, ndio tatizo ambalo bado tuko nalo nchi hii. Wizara ya Ardhi hii iliyopo ukiiuliza mwaka huu imepima mashamba mangapi kwa ajili ya wafugaji? Hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kongwa nayo mnataka muanze kuilimisha alizeti, yaani ile ranchi tena tuibadilishe iwe kwa ajili ya alizeti. Kwa hiyo, bado hau-address. Watu wameacha kulisha nyasi sasa wanalisha mifugo *concentrate* na mahindi utaweka humo humo na kila kitu, ng'ombe anapata kilo moja kila siku. Sasa umaskini tutauondoa namna ipi? Hata hivyo tukijinasibu tunasema Tanzania ina ng'ombe 45, ng'ombe wa aina gani? Ng'ombe ambao wamekomaa, wameshupaa misuli, hawezi kula mtu kimataifa. Kwa hiyo tu-address sera zetu, ng'ombe kweli tunao, lakini tunachunga karne hii! Bado kuna tatizo, bado sera zetu...

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kingine ambacho tumeshindwa kuelewa, tumepata Awamu ya Kwanza Mwalimu Nyerere alituwekea *base* nzuri sana zilikuwepo ranchi alizianzisha, kiwanda kile cha *Tanganyika Packers* na maeneo mengi, lakini kwa nini tunashindwa ku-copy mambo ambayo yamefanyika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme Serikali ifanye mambo machache ya kuonekana. Zimbabwe walipata shida sana ya kiuchumi, wameyumbishwa, lakini Zimbabwe mwaka jana wameweza kulima ngano ya kuwatosheleza wao na ziada wamepata, nchi ya Zimbabwe, mfano mdogo kabisa. Zimbabwe sasa upande wa Kusini mwa

9 NOVEMBA, 2022

Afrika ndio wanaozalisha maziwa kwa uhakika, laikini wanafanyaje? Walima nyasi na wanalisha pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme bado tuna tatizo, kwanza hatuamini katika kuendelea kupitia kilimo. Tunajinasibu kwenye madini, kwenye nini, lakini kilimo ndio kinabeba watu wetu. Asilimia 65 ya Watanzania wapo kwenye kilimo, sasa nilikuwa naangalia hapa kwenye Mpango kwa mfano, kama nilivyosema Kanda ya Kati anasema kwamba kuangalia maeneo ambayo yana tatizo la mabadiliko ya tabianchi. Vinakuja vile viprogramu vidogo vidogo vile vya kimazingira na mnaitaja Bahi kwamba tutawapelekea viprogramu vya kuhifadhi, kupanda miti, tunahitaji mtuondelee umaskini. Huko mnakotupeleka viprogramu ambavyo niseme havina maana muda wake umepita sana. Tuna umaskini mkubwa tunataka kuondoa umaskini kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa dhati kabisa; reli hii imejengwa lakini unaangalia hivi reli hii ni kwa ajili ya kupeleka mizigo Congo tu au na nchi zingine? Sisi tunabeba nini kutoka hapa kwa ajili ya ku-export? Tatizo kama nilivyosema mipango yetu ni mingi, lakini je, mipango ya kuondoa umasikini iko wapi? Ziko nchi zingine ambazo tulikuwa nao sawa, nachukulia kanchi kama Bangladesh kametoka kwenye uchumi wa kilimo sasa kako kwenye uchumi wa viwanda. Hata hivyo asilimia kubwa sasa ya Wabangladesh wengi wako mjini kwa sababu ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Mawaziri wetu na viongozi wetu wengine jitahidini kwenda kwenye nchi hizi nyingine mkaone wamefanyaje? *What is the success story?* Hata hivyo nchi tu kama ya Zimbabwe kama nilivyosema

9 NOVEMBA, 2022

wenzetu wamepiga hatua kubwa kwa maana ya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka nimalizie; wenzangu wameongelea habari ya *Presidential Delivery Bureau*. Malaysia ndio nchi ambayo imefanikiwa kwa kutumia *Presidential Delivery Bureau* na kwetu hapa kuna shida ya ufuatiliaji. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaenda nje ya nchi, anaingia mikataba, anarudi, lakini nani wa kufuatilia ile mikataba? Utekelezaji wake unasuasua. Tulikuwa na *Presidential Delivery Bureau* baadhi ya maeneo ambayo yalifanikiwa ni namna ya kuibana Serikali katika *quarterly*, kwamba kulikuwa na maelekezo ya Rais haya hapa mmeyafanyanje? Sisi nchi hii tunajuana, jambo likishakuja mnaliweka mezani wale wenzetu tulioingia nao mkataba watatuma *email* na haijibiwi na jambo hilo tumekuwa wazito wa kujibu ndio linakuwa limetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachoomba na niungane na wenzangu, tunataka *Presidential Delivery Bureau* irudi ili kuwe na chombo cha ufuatiliaji na kukumbusha Wizara zetu kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliingia mkataba China, sasa jambo hili Wizara ya Mifugo mmefikia wapi na hatima yake imefikia wapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, kinachokosekana ni namna gani masuala ambayo viongozi wakuu wa kitaifa aidha wanaingia mikataba wanavyokuwa nje na wakirudi hapa utekelezaji wake na ufuatiliaji wake ni kidogo. Jambo hili sasa linafanya kwamba tunaingia mikataba na watu, utekelezaji ni jambo lingine. *(Makofi)*

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana.
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Idrissa Juma, ajiandae Mheshimiwa Getere, ajiandae Mheshimiwa Salim Omar.

MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika mpango huu wa Serikali. Kabla ya kukushukuru wewe namshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeusikiliza mpango na nimeusoma kwa umakini na nimeurejea mara kadhaa. Naomba nijiridhishe kwamba Mpango huu umeakisi yale ambayo tuliyaelekeza katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2020/2025. Ni chama chetu ndicho ambacho kimemuweka Rais madarakani na sehemu kubwa ya Wabunge tuliomo humu ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo yale yaliyoandikwa kwenye mpango nimeona dhamira ya kuendelea kukamilisha madaraja yale ambayo tumeyaahidi, nimeona dhamira ya kuendelea kuboresha sekta ya afya, nimeona dhamira ya kuendelea kutoa ruzuku kwa wanufaika wa TASAF zaidi ya milioni moja nchi nzima. Kwa hiyo, yale yale ambayo tuliyaahidi kwenye Ilani yetu yanaendelea kutekelezwa na Mama Samia katika Awamu yake ya Sita na kweli kazi inaendelea. Kwa hiyo, hili nimejiridhisha na kwa nafasi hiyo naunga mkono mpango huu. (Makofi)

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja, mpango wowote ni kukusanya na kutumia. Mpango wa kutumia umekaa vizuri sana, mpango wa kukusanya unaelekea kukaa vizuri, lakini usimamizi wa yale yaliyokusudiwa kutumiwa bado tuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naweza nikarudia Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za miaka takribani miwili au mitatu iliyopita. Kila mwaka katika Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, fedha za wananchi zinapotea katika mazingira tofauti. Fedha hizo tukiweza kuzizuia, tunao uwezo wa kufanya mengi makubwa kwa ajili ya wananchi wetu na hivyo tukaisaidia Serikali yetu kuweza kufanya vizuri zaidi huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetolewa mfano wa marejesho ya fedha zinazotolewa kama kukopesha wananchi 10% ile ambapo 4% kwa vijana, 4% kwa akina mama na 2% kwa walemavu zaidi ya shilingi bilioni 80 nchi nzima. Shilingi bilioni 80 kama ikisimamiwa vizuri inaweza Kwenda kwa vijana na ikaleta matokeo na kila mwaka fedha zinaongezwa. Lakini tumeona kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali namna fedha hizo wakayi mwingine zinakwenda, zinapotea na hazionekani nini zimefanya. Hatuwaoni vijana waliotajirika kwa fedha hizi katika Halmashauri zetu, hatuwaoni akina mama waliotajirika na wala wenzetu wenye ulemavu waliotajirika. Kuna umuhimu Wizara ya Fedha katika mpango huu mhakikishe mnakwenda kuweka macho katika nafasi hii na maeneo mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumze jambo lingine kuhusiana na Muungano. Taifa letu ni la

9 NOVEMBA, 2022

Muungano, nchi hii ni Tanzania ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Mpango huu umezungumza masuala ya kimuungano katika masuala ya tabianchi. Kuna manufaika na umeelekeza kwamba kutapelekwa fedha na sehemu nyingine iliyozungumzwa ni katika kujenga au kuboresha nyumba ya Makamu wa Rais, Tunguu, napongeza kwa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu wa kutenga fedha maalumu za kufanya utafiti za Muungano wetu mara kwa mara kutokana na mahitaji yake. Katika mpango huu tukiweka fedha maalumu, tukazitenga ambazo zitakuwa kazi zake ni kufanya tafiti tu ya Muungano wetu. Kuna watu wanahoji kwa nini kuna Muungano wa Serikali mbili mpaka leo? Lazima tuwe na tafiti ambazo zitasaidia kuboresha na kuondosha manung'uniko ya kimuungano. Kwa sababu bado wafanyabiashara wa Zanzibar wanaendelea kunung'unika kuhusiana na mambo wanayotengenezewa katika bandari. Sijaona mpango huu ukielekeza ni kipi kifanyike katika kuhakikisha manung'uniko ya wafanyabiashara hasa wadogo wadogo wa Zanzibar wamaweza wakaondolewa vikwazo ili wanufaike na fursa za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wakati akija kufanya majumuisho Mheshimiwa Waziri atambue kwamba miongoni mwa fursa ambazo wafanyabiashara wadogo...

MHE. SALIM MUSSA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

9 NOVEMBA, 2022

T A A R I F A

MHE. SALIM MUSSA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza kwa kukazia ukweli juu ya suala la manung'uniko ya wafanyabiashara kutoka Zanzibar hususani kwa kadhia wanazozipata katika bandari ya Dar es Salaam. Hata juzi kuna mfano wa haluwa ya shilingi laki moja tu raia amebanwa pale na kutakiwa kuilipia nusu ya ile bei aliyonunulia. Kwa kweli ni kilio na lazima liangaliwe kwa jicho pevu kabisa, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Idrissa.

MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo na nimeipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya tunayaondoaje? Ni kwa kufanya tafiti tu, ndio maana nashauri Mheshimiwa Waziri akija kuleta majumuisho atuambie na aone umuhimu wa kuwa na fedha maalumu zitakazopelekwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kufanya utafiti wa hali ya Muungano wetu kwa sasa, changamoto zilizopo na kutafuta ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado najjuliza labda kukiwa na utafiti utaniletea uthibisho mzuri. Kwa nini mpaka leo kama suala la afya sio suala la Muungano? Lakini tukiwa na utafiti unaweza ukatusaidia labda tukiendelea kuwa suala la afya sio suala la Muungano kunaweza kukawapa fursa nyingi zaidi Watanzania, lakini kama likiwa la Muungano litaleta fursa nzuri zaidi.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoshauri ni umuhimu wa uwepo wa fedha maalumu za utafiti juu ya Muungano wetu, wala tusione aibu kufanya hivyo kwa sababu ndio Muungano pekee, kielelezo cha umoja katika bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Getere, jiandae Mheshimiwa Salim Omari.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nianze kwa kumpongeza Waziri ambaye ametuletea mpango. Mpango wake ni mzuri sana na unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ambao tunajadili sasa hivi hapa ni kamnofu/kakipande kamoja ka miaka mitano tuliopitisha kwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilipopitisha ulikuja mpango mrefu wa miaka mitano. Sasa hapa tunajadili kakipande tu kale ka miaka mitano ndio maana tunaona miradi mingi iliyoko humu ni ile ile ambayo inakuwepo, miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema miradi mingi tuliyonayo, tuna Bwawa la Nyerere, tuna reli ya umeme, tuna bandari zinajengwa na tuna miradi mingi ya kimkakati inajengwa. Kama kweli tuko tayari, nchi hii watu walihangaika sana kutafuta uhuru na bahati nzuri viongozi wetu watangulizi wa nchi hii walianza kwa kutengeneza utaifa na sio kutengeneza uchumi. Nchi nyingine zilianza

9 NOVEMBA, 2022

kutengeneza uchumi bila kutengeneza utaifa. Sisi tumetengeneza utaifa upo na leo tunafahamiana vizuri sana. Kwa hiyo, kutengeneza uchumi na kupanga mipango sisi sio shida kwa nchi hii ya Tanzania, shida yetu ni kusimamia mipango, ndio shida tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi najiuliza, kama miaka mitano iliyopita tumepanga mipango ya miradi ya kimkakati ,hatukuimaliza na leo ni mpango wa tatu tunaenda unaisha mwaka 2025. Bwawa la Nyerere litakuwepo, labda reli itakuwepo, labda bandari kwenye mkakati itakuwepo, hivi hii mipango itakwisha lini? Kwa hiyo, nafikiri kwamba Mawaziri wote na hasa Waziri mwenye mpango mwenyewe tuhakikishe kwamba miradi mikubwa tuliyopanga inaisha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema jambo moja tu, hii nchi hata tungepata Rais ananuka mafuta, hakuna. Kwa sababu watu wetu tunaowategemea huko chini hawapo. Sasa nchi hii imebaki kila Rais anayekuja Rais anafanya nini? Je, ninyi mmefanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna chama kikubwa cha CCM, tuna viongozi mahiri, tuna vijana tumewafundisha, ni makada na wazalendo, kwa nini hawafanyi mambo Rais amewaagiza? Leo kuna miradi inaliwa tu sasa tunasema tunatafuta hela, ipi sasa? Maana miradi yote ninayoiona ni ile ile na kusema kweli ndiyo tulivyopanga na huwezi kuleta mpango mpya. Cha msingi ni kukusanya fedha ili miradi iende kutengenezwa. Hicho ndicho cha msingi tulicho nacho. Tukusanye fedha miradi itengenezwe.

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nilikuwa nasikia jambo wanasema, bwana Bwawa la Nyerere lina hela ambayo imekuwa *ringfence*. Sasa sijui Kiswahili cha *ringfence* ni nini? Kwamba kuna fedha ipo kiasi kwamba hatuhitaji fedha nyingine kutengeneza hilo bwawa. Tutakuwa tunatoa humu tunajenga. Kuna hela za *ringfence* ya SGR zinakuwepo na mimi najiuliza kama ipo au haipo kwa nini tusikope sasa hiyo fedha tukaifungia, tukasema hiyo fedha imalize huu mradi? Kwa nini tusifanye hivyo? Mara tunaambiwa fedha tunakusanya tunalipa, mara tunaambiwa fedha tunakopa, tuambiwe wazi sasa fedha za mradi wa Bwawa la Nyerere ziko wapi? Ziko tayari au tunazikusanya? Fedha za bwawa, reli na miradi mingine ya kimkakati. Mimi nafikiri hili ndilo jambo la msingi tulifanye.

Kwa hiyo, naishauri Serikali tuhakikishe tunakusanya mapato na tuyatumie ipasavyo, vinginevyo itakuwa ni mchezo wa kuigiza. Nchi yetu iko salama kabisa, tatizo ni namna ya kusimamia miradi yetu iende, tatizo ni namna ya kusimamia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza jambo moja, jana nimesikia wanasema Mto Ruaha hakuna hata tone la maji. Mimi nimewahi kutembelea ule mto, sehemu kubwa ya ule mto hakuna kina kirefu. Sasa najiuliza hivi tukipeleka pale tukawa kila mita 500 au kilometa 15 tunachimba kina kirefu kwenye huo huo mto tunachimba mpaka tukaumaliza, hivi maji yakiisha si yatabaki mle ndani? Tumekuwa na mvua zinanyesha kila siku kwenye nchi hii, lakini maji yote yanatoroka yanaenda ziwani. Sasa najiuliza hivi tunafanyaje? kama hatuna uwezo wa kukinga maji kukabiliana na suala la *climatic change* tutafanyaje?

9 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia habari ya Bunda, Mheshimiwa Mwigulu mpango huu ni msingi wa bajeti ijayo. Sasa najjuliza hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha wewe ungekuwa Mbunge wa Jimbo la Bunda ungefanyaje? Kama leo ndoo ya maji ni shilingi 1,000 mpaka 2,500 wakati kutoka ziwani ni kilometa 25. Leo maji yanakuja mpaka Dar es Salaam, mnasema maji yaje Dodoma, yaende Tabora, Shinyanga sijui yaende wapi, lakini Bunda kilometa 25 hatuna maji. Wanachi wangu, wananchi wa Mama Samia wanachota maji kwa ndoo shilingi 1,000 hadi 2500. Hivi wewe ungekuwa Mbunge wa Bunda ungefanyaje? Hivi wakikwambia hauwatetei hawana maji unafanyaje?

Kwa hiyo, nakuomba kwenye mpango ujao wa bajeti uhakikishe kwamba maji yanaenda kwa babu zako, usiwaache kwenye hii hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante nashukuru Mheshimiwa Lucy yupo salama hapo. Mheshimiwa Salim Omar.

MHE. SALIM MUSSA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuweka baraka yangu katika mpango huu wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Kwanza kabisa na mimi kwa niaba ya wananchi wa Gando natoa zangu pole kwa wote wahanga waliofikwa na *issue* hii ya *Precision Air*, lakini kwa wale waliotangulia mbele ya haki tunasema *Allahumma ghufilahum warhamni*

9 NOVEMBA, 2022

maskanahum fil Jannah (Mwenyezi Mungu aende awape pepo na mapumziko mema na sisi atujalie hatima njema).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitachangia mambo matatu katika mpango huu ambayo naona kidogo hayakuzunguziwa sana kwa mujibu wa nilivyosoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza uchumi wa nchi ni lazima tuweze kukuza teknolojia ndani ya nchi yetu. Nimeangalia miongoni mwa *means* ya kukusanya kodi ni pamoja na kuliongezea Jeshi la Polisi uwezo wa kiteknolojia. Leo Mheshimiwa Bonnah alisimama hapa kazungumzia suala la kamera za barabarani, jambo hili ni la msingi sana. Wengi ambao hawana taaluma na masuala ya kamera wanaona kwamba labda ni kumulika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamera hizi zitakapowekwa barabarani zinaweza kuwa *integrated* na *system* za kileo ambazo zina uwezo wa kuweza *ku-capture plate numbers* na kuweza kupiga *automatic fine* na mwisho wa siku Taifa hili likakusanya fedha nyingi kuliko *traffic* kutembea na *gadgets* ambazo *traffic* unaweza uka-*bargain* naye barabarani, bwana nipige faini ama la na akakuacha, lakini teknolojia haina *bargaining*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeshauri katika Mpango huu Mheshimiwa Waziri wa Fedha uchukue suala hili la *CCTV camera* tuweze kuweka walau kwa kuanzia *first phase* tuweke katika *junctions* za barabara zetu. Wapo wanaopita taa nyekundu, wanao *overtake* hovyoy, wako wanaofanya mambo ya hovyoy kabisa barabarani ili wakumbane na *system* hii mwisho wa siku tuweze kuweka

9 NOVEMBA, 2022

nidhamu bora barabarani na kukusanya mapato kwa kutumia digitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda mbali zaidi teknolojia hii hii iende *i-apply* katika kulinda heshima, mali na utu wa Mtanzania na kwa wale wenzetu wanaotoka nje ya Tanzania wanaokuja hapa Tanzania. Nasema hivi kwa sababu lipo janga kubwa ndani ya Taifa letu sasa hivi na mimi naliona na tiba yake inaendeshwa lakini kidogo kidogo sana likisimamiwa na Jeshi la Polisi, suala la kuchafuliwa majina ya watu kupitia mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwapatia uwezo askari polisi na tukawajengea *unit* maalum ya *cybercrime* iliyo ya kweli kabisa kwa kila kituo cha mkoa, tukawapa na *equipment* na *skills* ili waweze kuwakamata hawa watu ambao wanachafua watu ambao wamejenga heshima zao kwa miaka mingi, basi Taifa hili tutaweza kwenda mbali zaidi. Lakini sio tu kuchafuliwa majina, lakini pia mtandao unatumika kwa ajili ya kufanya *fraud* ya kuwaibia watu fedha. Wapo watu wanatapeliwa wengi, kuna zile namba utasikia tuma kwa namba hii. Kuna watu wanasikiliza *information* za watu halafu mara tu wana-*dump in* na wanakuja kuchukua fedha pasipo na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba Wizara ya Fedha walichukue hili tuliwezeshe Jeshi letu la Polisi kwa *skills* pamoja na *equipments*, kwa kila mkoa iwepo kweli *cybercrime* na sio tu maneno. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika kituo cha mkoa wetu Wete pale simuoni askari hata mmoja ambaye ana *iPad* ya inayoshughulika na masuala ya kwenda ku-*extract*

9 NOVEMBA, 2022

information kwa ajili ya kuweza kutupa majibu haya. Jambo hili linapelekea polisi kuweza kupewa lawama kubwa. Kesi ni nyingi lakini watuhumiwa hawakamatwi mpaka polisi waende wakaangukie taasisi nyingine, wakapigie watu magoti sjiu *TCRA, mobile providers* hao. Polisi wenyewe waweze kutengenezewa *unit* na waweze ku-*extract information* kiukweli hasa ili tuweze kuendelea zaidi ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa ningependa pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie suala la kuongezea nguvu Jeshi letu la Uokozi (*Fire*). Kwa mfano wa Jiji la Dar es salaam, juzi hata mimi nilipata kadhia ya kuunguliwa gari langu moto, lakini gari la zimamoto mpaka lisukumwe au liwe *boosted*. Sasa hadi liwe *boosted* tayari watu watakuwa wamefariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliunguliwa na soko letu la Kariakoo, hivi ukiangalia *distance* ya kutoka kwenye Ofisi ya *Fire* pale hadi Kariakoo, soko lile ni la kufikia mpaka likaangamia namna ile? Ipo haja ya Serikali kuongeza magari ya kisasa, yaliyopo ni chakavu, yana umri sawa na Salim miaka 34 na kwenda mbele. Ukiangalia matukio yanatokea *frequently*, lakini kubadilisha *equipment* hizi imekuwa ngumu ndani ya Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nitoe mchango wangu huo *In Sha Allah* uende ukatekelezeke. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Fedha uko hapa, ni kweli *safety and rescue* Tanzania sasa hivi tuna hali ngumu sana na kutokana na maendeleo yanavyozidi

9 NOVEMBA, 2022

kwenda bila ya kuwa na *tools and equipments* za *safety and rescue* tutapata matatizo. Mpango wa Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo Waziri aliyeondolewa siku za nyuma ulikuwa ni mpango mzuri, tatizo hakufuata utaratibu. Hii moto siku hizi watu wanazima na *drones* tu basi.

Kwa hiyo, nafikiri hizi *CCTV* miji mikubwa yote ya Tanzania inastahili kupata *CCTV*, ni kitu muhimu kwa usalama na inaleta *confidence* kwa *investors* vilevile, kuna *investors* wakija wakiona kuna *CCTV* wanawekeza. Kwa hiyo, mimi naona Mheshimiwa Waziri hili mlitazame na mlipe kipaumbele katika mipango yenu hata hizo *SGR* pamoja na bwawa vinahitaji *proper surveillance equipments* kulinda *equipments* hizi.

Katibu.

NDG. LAWRANCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.26 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 10 Novemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)